## BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA PILI

## KIKAO CHA TATU – TAREHE 9 FEBRUARI, 2006

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jana majira ya alasiri Mheshimiwa Waziri wa Elimu wa Serikali ya Zanzibar alituletea hapa mezani taarifa ya kusikitisha sana ya msiba uliowakuta kule Zanzibar Mjini, watoto wa Kitanzania kumi na mmoja ambao wamefariki jana katika ajali ya kuogelea.

Kwa kuwa Bunge limepewa taarifa ya msiba huu tukiwa hapa Dodoma, nawaombeni tusimame kwa dakika moja. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi na tunaomba pia Mwenyezi Mungu awajaalie wafiwa wote wawe na subira katika hali ngumu hii iliyowakuta. *Amin.*

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walisimama kwa dakika moja kuwaombea watoto 11 wa Zanzibar waliofariki kwa ajali ya kuogelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla sijamwita Mheshimiwa ambaye anauliza swali la kwanza kwa asubuhi hii, naomba nitoe taarifa kwamba nimekubaliana na Mheshimiwa Waziri Mkuu kuwa hoja yake ya kujadili hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania badala ya kukamilishwa siku ya Ijumaa wiki hii iendelee hadi Jumanne asubuhi wiki ijayo.

Waheshimiwa Wabunge, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hili na hii inatupa fursa ya Waheshimiwa Wabunge wengi zaidi kuweza kuchangia hoja hii muhimu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tusingefanya hivyo takribani Wabunge sabini wasingechangia. Kwa hiyo, limekuwa ni jambo muhimu na nashukuru kwa hilo. Sasa swali la kwanza kwa leo Mheshimiwa Janet Kahama.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 25

**Msaada kwa Wajane wa Viongozi wa Taifa**

**MHE. JANET B. KAHAMA** aliuliza:-

(a) Je, ni vikundi vingapi vya wajane vilivyokwishatambulika katika Mkoa wa Dar es Salaam na ni misaada gani na mingapi ya hali na mali imeshatolewa na Serikali na mashirika ya huduma mbalimbali na ni kwa vikundi vipi?

(b) Je, ni misaada gani inatolewa kwa wajane wa viongozi wakuu wa Taifa mathalani wake za Marais na Makamu wa Rais wa Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na wajane wa Mawaziri Wakuu?

(c) Kama misaada hiyo ilitolewa, je, ilitolewa chini ya sheria zipi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janet Kahama, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na mgawanyo wa majukumu, ofisi yangu inashughulikia watumishi wa umma na hivyo haina takwimu zinazohusiana na wajane wanaotokana na vikundi vingine vya wafanyakazi ambao si watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wajane wanaotokana na watumishi wa umma, misaada wanayoipata imefafanuliwa katika Sheria ya Mafao ya Hitimisho la Kazi katika Utumishi wa Umma (*Public Service Retirement Benefits Act*) Na. 2 ya mwaka 1999. Aidha, utaratibu wa malipo hayo umewekwa bayana katika sheria hiyo hususan vifungu 10(i) na 11 (i)-(iv). Chini ya vifungu hivi mtumishi anayefariki na kuacha mjane au wategemezi kabla ya kustaafu, mjane au wategemezi wake watalipwa fedha sawa na malipo ya mkupuo *(Commuted Pension Gratuity)* au Pensheni ambayo angelipiwa mtumishi katika kipindi cha mwaka mmoja kama angestaafu kutegemea ni kiwango kipi kati ya hivyo ni kikubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, wajane wa viongozi Wakuu wa Kitaifa yaani Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu wanahudumiwa kwa mujibu wa Sheria ya Hitimisho la Kazi kwa Viongozi wa Kisiasa Na. 3 ya mwaka 1999 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 11 ya mwaka 2005. Huduma zinazotolewa kwa wajane hao ni pamoja na:-

(i) Fedha za matunzo kwa kiwango cha asilimia arobaini ya mshahara wa kiongozi husika aliyeko madarakani kwa mwezi;

(ii) Gari moja linalotolewa na Serikali ambalo mjane humiliki moja kwa moja baada ya miaka mitatu;

(iii) Mshahara wa kiwango cha kima cha chini cha Serikali kwa ajili ya kuwalipa dereva na mtumishi wa ndani;

(iv) Usafiri kwenda mahali ambapo yatakuwa makao yake ya kudumu;

(v) Matibabu kwa gharama za Serikali; na

(vi) Gharama za mazishi ya wajane hawa.

Aidha, napenda ieleweke kuwa stahili zinazotolewa chini ya sheria hii zinawahusu viongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano tu. Utaratibu wa huduma kwa Viongozi Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar umeelezwa katika sheria ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, *The National Leaders Act, No*. 10 ya mwaka 2002.

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri bado ningetaka kujua kuhusu hawa wajane ambao ni wananchi wa kawaida. Ninavyojua ni kuwa wengi wamekwishajiunga katika vikundi mbalimbali, je, sasa Serikali baada ya kujua hivyo kuwa hakuna mtu anayewasaidia ni lini watakaa walifikirie eneo hilo la kuwasaidia wajane kwa kuwapatia mafunzo ya kibiashara, kwa kuwasaidia mitaji na kwa kusaidia mafunzo ya kuweka na kukopa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi ni kwamba Wizara yangu inashughulika na wajane wa watumishi wa utumishi wa umma. Kwa upande wa vikundi vingine vya wajane Serikali za Mitaa, Taasisi za Umma na sekta binafsi zinawasaidia kupitia mifuko mbalimbali ya hifadhi ya jamii kama *NSSF, PSPF,* BIMA, *LAPF* ambayo hutoa misaada ya wajane mbalimbali kwa kuzingatia sheria zinazounda Mifuko hiyo.

Aidha, yapo Mashirika yasiyo ya Kiserikali na ya Kidini ambayo pia yanatoa misaada mbalimbali kwa wajane kwa mfano *TAWLA, TAMWA, TANGO* na *CARITAS.* Mashirika hayo yamekuwa yakisaidia wajane katika matatizo mengi ya kisheria, mirathi na ustawi wa jamii. *(Makofi)*

Na. 26

**Maji ya Mabwawa**

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa mara nyingi maji ya mabwana si safi na salama kutokana na namna binadamu na wanyama wengine wanavyoyatumia kwa kunywa, kuoga, kufua na wakati

mwingine hujisaidia humo haja kubwa au ndogo na wakati mwingine wanyama kucheza ndani ya maji hayo:-

Je, Serikali ina mikakati wowote wa kuyafanya maji hayo yawe safi na salama kwa matumizi ya binadamu na hata wanyama?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mbunge wa Kibaha Mjini, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa umakini wake katika kufuatilia na kuhakikisha kwamba wananchi wa Jimbo lake wanapata huduma ya maji yenye ubora unaotakiwa na ambayo ni salama kwa matumizi ya binadamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mabwawa ni chanzo muhimu cha maji hususan katika maeneo yenye ukame. Ili kukabiliana na matatizo ya ukosefu wa maji kwenye maeneo hayo, Serikali kwa kushirikiana na wananchi pamoja na wadau wengine imejenga mabwawa na malambo kwenye maeneo hayo ambapo Wilaya ya Kibaha ina jumla ya mabwawa ishirini na moja.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kwamba ujenzi na uendeshaji wa mitambo ya kusafisha maji ili yawe safi na salama unahitaji utaalam mkubwa na gharama kubwa, mitambo kama hiyo inatumika kwenye mabwawa makubwa yanayohudumia watu wengi kwa pamoja. Hivyo kwa upande wa mabwawa madogo na malambo ili kuhakikisha kwamba matumizi ya maji ya vyanzo hivi hayaathiri afya za wanayoyatumia Serikali ina mikakati ifuatayo:-

(i) Usanifu na ujenzi wa mabwawa na malambo unazingatia kuwa na maeneo tofauti ya kuchotea na kunyweshea mifugo.

(ii) Kuelimisha wananchi kuhusu utunzaji wa mabwawa na malambo pamoja na matumizi yake.

(iii) Kuhamasisha wananchi kuchemsha maji yao ya kunywa.

(iv) Usanifu wa mabwawa na malambo unaozingatia kupunguza kiwango cha uchafuzi ikiwa ni pamoja na yafuatayo:-

- Kuchagua eneo la ujenzi nje ya makazi, mashamba na shughuli nyingine za wananchi.

- Kuweka mifumo ya kupungu za uchafu kama vile machujio ya kokoto na mchanga *(roughing filters/ infiltration galleries)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuzihimiza Halmashauri za Wilaya na Taasisi nyingine zinazohusika katika ujenzi wa mabwawa na malambo

kuzingatia mikakati hyo niliyoitaja hapo juu, kwa kuweka sheria ndogo kwa ajili ya kulinda na kusimamia matumizi ya mabwawa hayo. Sheria hizo zikitumika ipasavyo, zitadhibiti uchafuzi wa vyanzo hivyo vya maji unaotokana na vitendo visivyostahili kama alivyovianisha Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza namshukuru kwa kunipongeza na namwahidi tutakuwa pamoja mimi na yeye katika kusaidiana kwenye Wizara hii.

Swali, je, badala ya kuwaomba Halmashauri waweke sheria ndogo au wafanye hivi kwa mikakati ambayo ameisema, kwa nini tusiwe na sheria inayosema ni marufuku kuwa na mabwawa ya watu kuweza kuingia, tuweke *design* ya mabwawa ambao watu watakuwa hawaingii kwenye mabwawa bali wanachotea maji nje ya bwawa lile?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, swali lake ambalo amependa kujua kuwa kwa nini tusiweke sheria maalum kwa ajili ya jambo la uchafuzi wa maji, hilo tumelipokea na tutalifanyia kazi. Swali lake la pili, napenda kujibu kwamba, katika Wilaya ya Kibaha kuna baadhi ya mabwawa ambayo sasa hivi yanafanya vizuri na ningependa kutoa mfano wa mabwawa mawili, kuna bwawa katika Kijiji cha Kumba ambalo bwawa hilo limewekewa utaratibu mzuri na maji yanachunjwa na kuna bwawa katika Kijiji cha Lukenge ambapo pia wameweka utaratibu mzuri na utaratibu huo una njia mbili tofauti. Njia moja ni kwa ajili ya kunywa binadamu na matumizi yao na njia nyingine ni kwa ajili ya kutumia mifugo na zimehakikishiwa kwamba zina senyenge maalum ambapo uchafuzi haufanyiki. Kwa hali hiyo, ningependa kukubali ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na pia kuna mifano mizuri katika mabwawa yao ambayo ningemhimiza kwamba atusaidie kushirikiana na Vijiji vingine ambao hawana utaratibu kama huo na wenyewe wauanzishe. (*Makofi*)

Na. 27

**Tatizo la Maji Mantare na Ishingisha**

**MHE. RICHARD M. NDASSA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Mji wa Mantare na Ishingisha kuna chanzo cha maji ya kisima kirefu kilichokuwa kikiwahudumia wakazi wa Miji (Vijiji) hivyo ambapo palikuwepo na mtandao mzuri wa mabomba lakini sasa mabomba yake yamechakaa na kwa kuwa katika hotuba ya Rais wakati akizindua Bunge alisema Serikali ya Awamu ya Nne inakusudia kulikabili tatizo hilo kwa ari mpya na kasi mpya kuwawezesha wananchi wengi zaidi Mijini na Vijijini kupata maji safi na kwa kuwa taarifa za mradi na maombi yapo Wizarani:-

Je, ili kutekeleza usemi wa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya ni lini sasa Serikali italitatua tatizo la maji katika Vijiji hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve, kwa kuanza na kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji wa Mantare na Ishingisha ulijengwa mwaka 1976. Chanzo cha maji ni kutoka kisima kirefu chenye uwezo wa kutoa maji mita za ujazo 204 kwa siku sawa na mita za ujazo 8.5 kwa saa. Maji kutoka kwenye kisima hicho hutumiwa na wakazi wa Mantare na Ishingisha wanaokadiriwa kufikia 5,300 kutokana na sensa ya mwaka 2002. Mahitaji yao ya maji ni mita za ujazo 159 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, vyanzo vingine vya maji vinavyotoa huduma katika maeneo hayo ni visima vifupi vitatu vinavyofanya kazi eneo la Mantare na visima vifupi vitano katika eneo la Ishingisha. Hata hivyo upatikanaji wa maji katika Vijiji hivyo sio wa kuridhisha kutokana na uchakavu wa miundombinu na mtambo wa kusukuma maji. Aidha, mradi huu hauna tanki la kuhifadhia maji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Richard Ndassa, kama ifuatavyo:-

Kwa kutambua tatizo la maji kwenye Vijiji vya Mantare na Ishingisha, Serikali kwa kupitia Wizara yangu imetenga 30,000,000/= katika mwaka wa fedha wa 2005/2006 kwa ajili ya ujenzi wa tanki na ununuzi wa mabomba kwa ajili ya mradi wa maji wa Mantare Sumve. Aidha, kupitia Programu ya Taifa ya Usambazaji Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira, Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba imependekeza kuingiza Vijiji kumi vikiwamo vya Mantare na Ishingisha katika utekelezaji wa programu hiyo utakaoanza Julai, 2006.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa mradi huu wa Mantare na Ishingisha kwa manufaa ya Vijiji vitakavyohusishwa kama jinsi alivyosimamia kikamilifu utekelezaji wa miradi ya maji ya Malya na ule wa Sumve. (*Makofi*)

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwa sababu Serikali imeshatenga shilingi 30,000,000/=, sina swali bali naipongeza Serikali. *(Makofi)*

Na. 28

**Shamba la Kuzalisha Mitamba Songea**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika Kijiji cha Hanga, Kata ya Gumbiro, Jimbo la Peramiho, Wilaya ya Songea, kwa muda mrefu Shamba la Kuzalisha Mitamba *(SKMH)* limekuwa halifanyi kazi kwa sera ya ubinafsishaji na kwa kuwa wananchi wa Kijiji hicho na Kata nzima wanahitaji kukabidhiwa eneo hilo jambo ambalo halijafanyika mpaka sasa na kwa kuwa

katika mkutano wa *T.V.A.* Arusha Desemba, 2003 iliamuliwa kuwa shamba hilo likabidhiwe kwa *DED* Songea kitu ambacho hakijafanyika mpaka sasa:-

Je, ni lini Serikali itakabidhi shamba hilo kwa Halmashauri kwa maandishi ili shamba hilo litumike kwa shughuli nyingine kwa maendeleo ya wananchi wa Kijiji, Kata na Wilaya nzima?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa, naomba nitoe shukrani kwa kifupi kabisa kwa wafuatao. Kwanza, kwa wananchi wa Jimbo la Shinyanga Mjini kwa kunichagua kuwa mwakilishi wao. Pili, kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa kuniteua katika nafasi ya Naibu Waziri na tatu na mwisho kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kufanya ziara yake ya kwanza kikazi Mkoani Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, shamba la kuzalisha mitambo la Hanga lipo kilometa 60 kutoka Songea Mjini kando kando ya barabara ya Songea-Makambako. Shamba hili limepimwa likiwa na namba ya uandikishwaji *330531, Plan No. E 20 – 63/4* ya tarehe 3 Oktoba, 1997 na lina jumla ya hekta 6,610. Shamba hili lilikuwa ni mojawapo kati ya mashamba 11 ya uzalishaji mifugo yaliyokuwa yameanzishwa nchini katika miaka ya 1980 kwa ajili ya kuzalisha mitamba chotara wa maziwa kwa lengo la kuwauzia wafugaji wadogo wadogo. Mashamba hayo ni Hanga (Ruvuma), Ibaga na *Sao Hill* (Iringa), Nkundi (Rukwa), Kibaha (Pwani), Nangaramo (Mtwara), Nachingwea (Lindi), Mivumoni (Tanga), Mabuki (Mwanza), Kahama (Shinyanga) na Lugufu (Kigoma). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shamba la Hanga pamoja na mashamba ya Nachingwea na Nangaramo yaliendelea kuzalisha mitamba kwa ajili ya Mikoa ya Kusini hadi miaka ya 1990 wakati Serikali iliposimamisha shughuli za uzalishaji mifugo katika mashamba ya Hanga na Nachingwea. Hili lilifanyika kufuatia mabadiliko ya sera ambapo Serikali iliamua kujitoa katika uzalishaji ili kuipa nafasi sekta binafsi kuchukua jukumu hilo. Kutokana na umuhimu wa kuendeleza mifugo katika Mikoa ya Kusini shamba la Nangaramo lililoko Mtwara liliachwa kwa makusudi ili kusaidiana na juhudi zingine za Serikali, kuongeza kasi ya uendelezaji mifugo katika Mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, shamba la Hanga pamoja na mashamba mengine ya uzalishaji mifugo yalitangazwa kwenye magazeti ya tarehe 16,18 na 20 mwezi Machi, 2000 kwa dhamira ya kubinafsishwa kupitia *Central Tender Board*. Matangazo haya hayakuzaa matunda kwani hakuna mwekezaji aliyejitokeza. Hivyo mwaka 2002, Baraza la Mawaziri lilitoa uamuzi wa kukabidhi shamba hili kwa Halmashauri ya Wilaya ya Songea ili liweze kupangiwa matumizi ya kuendeleza mifugo Mkoani.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekabidhi shamba la Hanga kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Songea tarehe 3 Februari, 2006 ili shamba hilo liweze kupangiwa matumizi ya kuendeleza mifugo na Halmashauri hii. Makabidhiano haya yamechelewa kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ilikuwa haijafikia muafaka wa namna bora ya kutumia shamba hilo. Vile vile Wizara na Halmashauri ya Wilaya zilikuwa zikifanya taratibu za kuwaondoa wananchi waliokuwa wamevamia eneo la shamba hilo.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Halmashauri ya Songea katika kutoa uamuzi wa namna bora ya kutumia eneo hili katika kuendeleza mifugo sio tu kwa manufaa ya Wilaya ya Songea bali pia kwa Mikoa ya Kusini.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa suala la maendeleo ya wananchi wa Jimbo la Peramiho, kwanza lipo mikononi mwa wananchi wenyewe na pili lipo mikononi mwa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Serikali za Vijiji husika na kwa kuwa shamba hili sasa limekabidhiwa mara baada ya kuona swali hili na Halmashauri kuendelea kufuatilia, je, Serikali ipo tayari kukubali kutoa maelekezo kwa Halmashauri yetu kwamba shamba hilo liweze kutumika kwa matumizi mengine zaidi ya kuendeleza mifugo kulingana na uwezo mdogo wa Halmashauri kuendeleza sekta hiyo ya mifugo peke yake?

Mheshimiwa Spika, pili, je, Serikali bado ipo tayari kuendelea kushirikiana na wananchi wa Halmashauri ya Songea Vijijini katika suala lolote litakalohusiana na uendelezaji wa mifugo badala ya kuiachia Halmashauri yenyewe peke yake? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, maamuzi ya Baraza la Mawaziri Na. 2 ya mwaka 2002 ni kuwa mashamba haya yaliyokuwa yanatumika katika uzalishaji wa mitamba kwa ajili ya uzalishaji wa maziwa iliamuliwa mashamba hayo yatumike kwa ajili ya shughuli za ufugaji tu. Kwa hiyo, matumizi yanayotarajiwa katika shamba hili kwa mujibu wa maamuzi ya Baraza la Mawaziri ni kwa maendeleo ya mifugo. Nadhani hili tutakubaliana wote kwa kuwa Mheshimiwa Rais amezungumzia haja ya kuendeleza sekta ya mifugo na ndio maana akaona ni busara hata kuanzisha Wizara inayojitegemea.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Jenista Mhagama, kuwa Wizara yangu ipo tayari kushirikiana na Halmashauri zote zenye nia ya kuendeleza matumizi ya ardhi kwa nia ya kuendeleza sekta ya mifugo. *(Makofi)*

Na. 29

**Kituo cha Watoto cha Kititimo**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa Kituo cha Watoto waliotokea kwenye mazingira magumu cha Kititimo (mfadhili alikwishajiondoa) na sasa kinalegalega sana kiasi cha kushindwa kujiendesha ipasavyo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kubeba jukumu hilo?

**NAIBU WAZIRI MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Watoto cha Kititimo kipo katika eneo la umbali wa kilometa tano kutoka Singida Mjini. Kituo kilianzishwa mwaka 1992 kwa lengo la kuwapokea watoto wanaoishi katika mazingira magumu kwa muda, kuwaandaa na baadaye kuwaunganisha na familia zao. Hata hivyo madhumuni hayo yalibadilishwa baada ya kupata wafadhili ambapo watoto waliweza kuhifadhiwa kituoni hapo kwa muda mrefu. Watoto waliohusika ni wale ambao walikuwa wanaishi katika mazingira magumu na watoto wa mitaani.

Mheshimiwa Spika, kituo hicho kilipata mafanikio makubwa baada ya kuwapatia baadhi ya watoto elimu ya msingi na sekondari, ufundi na stadi mbalimbali za maisha kama vile useremala, kilimo na malezi bora. Baadhi ya watoto wamefanikiwa kufika kidato cha tano na sita na mmoja amefika Chuo Kikuu.

Aidha, wapo waliofanikiwa kufanya kazi za kujiajiri wenyewe na wengine kuajiriwa katika Taasisi mbalimbali na watu binafsi. Kituo hicho kilikuwa kinaendeshwa na wananchi wa eneo hilo wakisaidiwa na wafadhili.

Baadhi ya wafadhili waliopata kusaidia kituo hicho ni pamoja na Shirika lisilo la Kiserikali liitwalo *Oxfarm Tanzania* ambalo lilikuwa likisaidia kutoa fedha za kununua vifaa vya mafunzo na vitendea kazi pamoja na kugharamia mradi wa ng’ombe wa kisasa na kutoa utaalam wa kuendesha miradi mbalimbali chuoni. Shirika la Kikristo la Kuhudumia Wakimbizi (*The Tanzania Christian Refugees Services*) Mradi wa Singida, lilisaidia zaidi shughuli za ufundi ambapo watu binafsi na Makanisa walisaidia kutoa chakula cha watoto.

Mheshimiwa Spika, baada ya ufadhili huo kusita, kituo kilishindwa kuendelea kutoa mafunzo kwa kukosa uwezo wa kuendesha mafunzo. Kwa sasa watoto wanasoma katika shule za msingi zilizopo jirani na kituo kwa kusaidiwa na uongozi wa Chama cha Malezi cha Singida.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwezekano wa Wizara kusaidia kituo hicho, Wizara yangu inaangalia uwezekano wa kukisaidia kupitia (MKUKUTA). Kwa hiyo basi, napenda kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba mara tutakapomaliza mkutano huu wa Bunge. Mimi pamoja na Mheshimiwa Mbunge tutakwenda kwa ari mpya, nguvu

mpya na kasi mpya, kwenda pamoja Singida ili kuona hali halisi ya mahitaji ya kituo hicho ikiwa kama zoezi la jumla litakalohusisha vituo vingine vya namna hiyo. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda kuuliza swali moja dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa idadi ya watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu ama wanaoishi mitaani inaongezeka siku hadi siku katika miji yetu ya nchi nzima ukiwepo Mji wa Singida. Je, Serikali ina mkakati gani wa kudumu kuhakikisha kwamba zoezi hili wanachukua jukumu la moja kwa moja badala ya kutegemea wahisani ama vituo kuwa na tabia ya kuombaomba kama ilivyo sasa hivi kituo cha Singida kinaomba Wabunge, wafanyabiashara na kadhalika hali ambayo inasikitisha sana?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara yangu na Wizara inayoshughulikia Masuala ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji iko katika jitihada za kuanzisha Mpango wa Hifadhi ya Jamii *(Social Protection Plan).* Mpango huu utaangalia pamoja na masuala mengine matatizo ya watoto hao wa mitaani pamoja na wale yatima kwa nchi nzima. *(Makofi)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Katika kipindi cha Bunge lililopita wakati ambapo mimi nilikuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii tulipelekwa uwanja wa fisi Dar es Salaam na Dr. Flora tukifuatana na Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya. Tulikuta wasichana wadogo kabisa wakijishughulisha na dawa za kulevya pamoja na biashara ya ngono. Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya alitoka na machozi na alilia pale. Sasa je, ... *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Utulivu. Naomba utulivu!

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Sasa je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kwamba Wizara yake nayo inahusika sana. Atakubali kufuatana na Kamati yangu ya sasa ambapo Mwenyekiti wangu ni Mheshimiwa Jenista Mhagama, ili tuwatembelee eneo lile tukatazame njia za kuwasaidia wasichana wale wadogo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inakubali kushirikiana na Kamati yetu ya Maendeleo ya Jamii kuweza kutembelea maeneo hayo pamoja na mwakilishi kutoka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwenda kuona matatizo hayo na hatimaye kuyatafutia ufumbuzi. *(Makofi)*

Na. 30

**Utekelezaji wa Masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki**

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa Jumuiya mpya ya Afrika Mashariki imejengwa kwenye msingi tofauti na Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyopita kwa msingi kwamba utekelezaji wa masuala yote ya Jumuiya kwa sasa ni jukumu la nchi wanachama na kazi kuu ya Jumuiya kama taasisi ni uwezeshaji tu *(facilitation);* na kwa kuwa, mgawanyo huo wa majukumu umezifanya nchi wanachama kupendelea zaidi kutumia *Protocols* kuendeshea shughuli za Jumuiya na mara nyingine kukiuka kwa makusudi baadhi ya sheria zilizopitishwa na Bunge la Afrika Mashariki, kama Kenya ilivyofanya mapema mwaka jana kwa kufuta ushuru wa dawa kinyume na makubaliano ya pamoja na ushuru *Common External Tariff (CET).*

(a) Je, Serikali haioni kuwa mgawanyiko huo mpya wa majukumu kati ya Jumuiya na nchi wanachama unahitaji muundo tofauti na Bunge la Jumuiya ili Bunge hili litokana na Wabunge wa nchi wanachama kwa nia ya kurejesha imani kati ya Jumuiya na watendaji wa nchi wanachama?

(b) Je, Makampuni yanayozalisha dawa nchini yameathirika kwa kiasi gani kwa uamuzi wa Kenya na baadaye Uganda mapema mwaka jana wa kuondoa ushuru wa dawa bila mashauriano na Tanzania kinyume na Makubaliano ya *CET?*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mbunge wa Kyela, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyopo sasa ni tofauti na ya awali ambayo ilivunjika. Jumuiya ya sasa imeundwa kwa msingi wa ushirikishwaji wa wananchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, tahadhari kubwa ilichukuliwa katika kubuni muundo na mfumo wa kuendesha na kusimamia masuala ya Jumuiya mpya ili kuepuka athari zilizojitokeza katika Jumuiya ya awali. Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Masharika ndiyo sheria kuu inayoongoza utekelezaji wa mchakato wa mtangamano wetu wa Afrika ya Mashariki. Mkataba unaziwezesha nchi wanachama kufikia makubaliano ya utekelezaji wa maeneo ya ushirikiano kwa njia zinazohusika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mbunge wa Kyela, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Jumuiya ya Afrika Mashariki ni changa sana lakini imejengwa kwa msingi imara wa maelewano. Aidha, kifungu 49 cha Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kinabainisha shughuli za Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki, mojawapo ikiwa ni

kuwa kiungo baina ya Mabunge ya nchi wanachama na lile la Jumuiya. Kifungu 50 cha Mkataba kimeainisha sifa na uteuzi wa Wabunge wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mbunge wa Jumuiya anatakiwa awe na sifa ya kuchaguliwa Mbunge wa nchi wanachama, lakini kwa namna yeyote ile hatatoka miongoni mwa Wabunge wa nchi wanachama pia hatakiwi kuwa mtumishi wa umma au wa Jumuiya na wala asiwe Waziri wa Serikali ya nchi wanachama. Mfumo huu wa Bunge la Afrika Mashariki unafaa kuendelea kutumika kwa maana unakidhi shabaha na malengo ya kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hapana shaka mfumo huu unaweza kubadilika baadae hususan utakapofikia katika hatua ya Shirikisho la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(b) Serikali imepokea malalamiko kutoka makampuni yanayozalisha madawa kuhusu kuathirika kwao kutokana na hatua iliyochukuliwa na Kenya ya kubadilisha viwango vya ushuru wa nje. Aidha, zoezi la kufanya tathmini ya athari hizo linafanyika kwa kuwashirikisha wadau husika ili kujua viwanda vinavyozalisha madawa hapa nchini vimeathirika kwa kiwango gani. Hatua hii itaiwezesha Tanzania kufanya majadiliano kupitia vyombo halali vya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri.

Kwa kuwa sasa hivi Tanzania, Kenya na Uganda ipo kwenye Umoja wa Forodha *(Customs Union)* na kwa kuwa tayari hivi sasa tuna *Common External Tariff,* lakini bado Tanzania ni mwanachama wa *SADC* na sasa hivi inajiandaa kuingia katika *free trade* na *SADC.* Vile vile Kenya na Uganda bado ni wanachama wa *COMESA* na wao pia wanaingia kuwa na *Common External Tariff,* huoni kwamba ni wakati sasa kwa nchi zote hizi kubakia kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki?

**NAIBU WAZIRI WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli baadhi ya nchi zinazoshiriki katika Afrika Mashariki wengine ni wanachama wa *SADC* na wengine ni wanachama wa *COMESA.* Tulipokuwa tunaunda Jumuiya hii tulikubaliana kwamba kama uko kwenye Jumuiya ya *SADC* au *COMESA* unaweza ukaendelea kwa maslahi ya nchi yako kama unaona inafaa. Lakini vile vile inatakiwa uzingatie maslahi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vile vile Mkataba wa Kuanzisha kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki unatoa nafasi Jumuiya kama Jumuiya kuzungumza kwa pamoja na hizi Jumuiya nyingine kama *SADC* na *COMESA* ili kulinda maslahi ya makubaliano ya ndani ya Afrika Mashariki.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Hivi karibuni kumekuwa na ripoti katika vyombo vya habari hasa kutoka kwa wenzetu wa Uganda zikisema kwamba Rais Yoweri Museveni wa Uganda yuko tayari kuachia Urais wa Uganda ili awe Rais wa Afrika Mashariki. Sasa je, hivi makubaliano hayo yapo kwamba yeye aje atutawale Afrika ya Mashariki? *(Makofi)*

**SPIKA:** Naona kama swali liko kidogo nje ya swali lililopo kwenye *Order Paper.* Ningeshauri Mheshimiwa kwa kuwa tuna nafasi basi aweze kuleta swali lake kwa maandishi.

Tunaendelea. Ahaa, samahani kuna majibu ya nyongeza?

**WABUNGE FULANI:** Hakuna !!!!!!

Na. 31

**Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere - Zanzibar**

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa Chuo cha Kumbukumbu cha Mwalimu Nyerere kimepewa eneo la kutosha Bububu ili kuongeza majengo ya Chuo hicho:-

(a) Je, ujenzi wake utaanza lini?

(b) Je, ni hatua gani za mwanzo zilizochukuliwa ili kuhakikisha kuwa nia ya ujenzi ipo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mbunge wa Mkwajuni, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kimekuwa chini ya Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia Kisheria kuanzia Aprili, 2005. Mimi mwenyewe nimepata fursa ya kukitembelea Chuo katika Kampasi zake za Kivukoni na Maisara, Zanzibar na katika eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi huko Bububu Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kinakabiliwa na matatizo mengi yakiwemo ya uchakavu wa miundombinu, uhaba wa wafanyakazi, kukosa uzio wa kulinda eneo, mmomonyoko wa udongo pamoja na uhaba wa vitendea kazi. Kutokana na hali hiyo, Chuo kwa sasa kinaandaa Mpango Kabambe wa Maendeleo *(Strategic Development Plan)* ambao utakapokamilika utaainisha mpango mzima wa ukarabati, upanuzi na ujenzi wa chuo katika Kampasi zake za Kivukoni na Zanzibar. Utekelezaji wa mpango huo unatarajiwa kuanza kwa kukarabati miundombinu iliyopo Makao Makuu yaani ya Kivukoni kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Zanzibar, Chuo kimefanya ukarabati ambapo darasa moja lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 20 umekamilika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchakavu wa miundombinu na upungufu wa wafanyakazi kama nilivyoeleza, Chuo kwa sasa kimeelekeza nguvu zake katika kuajiri wafanyakazi pamoja na kufanya ukarabati ili kuwezesha mafunzo kuendelea kutolewa bila usumbufu wowote.

Mheshimiwa Spika, aidha, kukamilika kwa ukarabati wa jengo la darasa huko Maisara Zanzibar kutawezesha chuo kuanza kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa Kampasi ya Zanzibar kuanzia mwezi Machi, 2006.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa ya Bunge lako Tukufu kozi hizo fupi ni pamoja na *Project Analysis and Management, Human Resource Management, Entrepreneurship* na *Guidance and Counselling.*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa wito kwa wananchi wa Zanzibar kujitokeza kutumia fursa ya mafunzo ya muda mfupi kujipatia taaluma katika tawi letu la Zanzibar. Nia ya kujenga chuo katika eneo la Bububu ipo na imezingatiwa katika mpango kamambe wa chuo. *(Makofi)*

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii kuuliza masuala mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Mheshimiwa Naibu Waziri ameyataja matatizo mengi, mimi nilikuwa sina haja ya kuyataja matatizo, nilikuwa nahitaji ni lini utaanza ujenzi au mpango huu utaanza lini wa ujenzi wa chuo au ardhi ile itatumiwa lini kuhakikisha kuwa chuo kinajengwa?

Swali la pili, ameyataja na amehakikisha kuwa chuo kile kina matatizo ya ukarabati wa majengo na mmomonyoko wa ardhi ambao hivi sasa bahari inakula sana eneo lile, je, hizo programu alizoziweka zikoje? Kwa sababu programu ya mwanzo wametenga shilingi milioni 100 lakini kwa ukarabati haitoshi kwa chuo kile.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, maelezo yangu ya awali yalikuwa yanajenga hoja kuonyesha kwamba si vyema kuanza kujenga eneo jipya wakati *main campus* ina matatizo makubwa na kuna kozi zinazoendelea pale. Kwa hiyo, ni vizuri kwanza ukarabati eneo hilo, kozi ziendelee bila matatizo kwa sababu eneo lipo, fidia ilishalipwa na linalindwa, sana sana katika mpango kabambe wa chuo tunataka tujenge uzio ili kuendelea kulinda hilo eneo. Kweli liko salama kwa sababu liko jirani na wanajeshi ambao wanatusaidia kulinda na sisi tumeshaweka mfanyakazi aliyestaafu wa chuo analilinda. Ujenzi nimesema nia ipo na iko katika mpango kamambe wa chuo.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili sikulisikia vizuri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, ungependa kurudia swali la pili la nyongeza?

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, nilimwuliza swalo la pili wanataka kufanya ukarabati wa chuo kile lakini ametaja programu tatu na programu ya kwanza imetengewa shilingi milioni 100 ambayo haitoshi kwa ukarabati wa chuo kile kilivyo hivi sasa. Hizo programu nyingine zitaendaje?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANASI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, mambo yote yanaenda kibajeti. Ni kweli katika mwaka wa fedha unaoishia sasa hivi 2005/2006 hizo shilingi milioni 100 zimetengwa. Ukienda pale chuoni sasa hivi kuna ukarabati mkubwa umefanyika ikiwemo na hilo darasa la Maisara Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, katika awamu hii 2006/2007 Serikali itaomba fedha nyingine zitengwe kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa chuo. Ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 32

**Tatizo la Kivuko cha Kigongo - Busisi**

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA** aliuliza:-

Kwa kuwa Kivuko cha Kigongo - Busisi licha ya kwamba kimekuwa kiungo kati ya Wilaya ya Misungwi na Sengerema pia ni kiungo kati ya nchi yetu na nchi jirani za Burundi, Rwanda na Kongo *(DRC)* kimekuwa kikiharibika mara kwa mara na kuwa kwenye hali ya hatari hasa katika kipindi cha mwezi Desemba 2005 na Januari 2006 kwa abiria na mali zao; na kwa kuwa mapato yatokanayo na kivuko hicho yangeweza kusaidia matengenezo ya mara kwa mara kuepusha ajali kwenye kipindi cha Desemba 2005 na Januari 2006; na kwa kuwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 imeeleza wazi juu ya upatikanaji wa kivuko kipya cha Kigongo - Busisi na kwamba Serikali ilishatenga fedha kwa ajili ya kutengeneza kivuko hicho kipya na Mkandarasi wa kufanya kazi hiyo alishapatikana:-

(a) Je, Serikali inaweza kutoa maelezo ya kina kwa wananchi husika kupitia Bunge hili sababu zilizofanya kivuko hicho kuhatarisha maisha ya wasafiri katika kipindi cha Desemba, 2005 mpaka Januari 2006?

(b) Je, Serikali haioni kuwa matengenezo ya kivuko hicho pamoja na vingine yanachelewa kutokana na mzunguko mrefu wa kufikia maamuzi juu ya fedha za matengenezo hayo; hivyo ione kuwa ni busara zaidi kama mamlaka zinazosimamia vivuko hivyo zikaruhusiwa kutumia moja kwa moja sehemu ya makusanyo kwa ajili ya ukarabati kuliko kuendelea kusibiri kibali na maelekezo toka kwenye Wizara husika;

(c) Je, Serikali inaweza kuwaeleza wananchi wa Sengerema na Watanzania kwa ujumla hatua zilizochukuliwa kuhakikisha kuwa matengenezo ya kivuko hicho ni ya uhakika na kwamba hali iliyotokea Desemba 2005 hadi Januari, 2006 haitatokea tena na kwamba utengenezaji huo utakamilika lini?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, Mbunge wa Sengerema, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kivuko cha Kigongo - Busisi chenye ukubwa wa tani 170 kina uwezo wa kubeba magari makubwa 14 na abiria 400 kwa mara moja. Kivuko hiki hutoa huduma kuanzia saa 12 asubuhi hadi saa tatu usiku. Kivuko hiki huunganisha baadhi ya Wilaya za Mkoa wa Mwanza na Mkoa wa Kagera na ni kiungo kikubwa kwa barabara iendayo nchi jirani za Rwanda na Burundi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, Mbunge wa Sengerema, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa muda wa wiki tatu kati ya Desemba 2005 na Januari 2006, Kivuko cha Kigongo - Busisi kilikuwa kinafanya kazi kwa kusaidiana na Boti ya Uokoaji (*Rescue boat)* kutokana na moja ya mtambo wa uendeshaji *(propulsion system)* kuharibika. Matengenezo ya mtambo huo yalichukua muda mfupi kukamilika na hatimaye kivuko kilianza kutoa huduma kama kawaida. Aidha, kwa kipindi chote hiki magari na abiria walivushwa kwa usalama na hapakuwepo tukio la kuhatarisha usalama wa abiria.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kuboresha ufanisi wa uendeshaji wa vivuko nchini, Serikali ilianisha Wakala wa Ufundi na Umeme *(TEMESA)* tarehe 26 Agosti, 2005 ambao unajiendesha wenyewe kutokana na vyanzo vyake mbalimbali vya mapato. Wakala huu hufanya matengenezo ya vivuko vyote nchini kwa kutumia mapato yatokanayo na vivuko bila kusubiri kibali na maelekezo ya Wizara.

(c) Mheshimiwa Spika, matengenezo ya kivuko hicho yaliyofanyika katika kipindi cha Desemba, 2005 na Januari, 2006 ni ya uhakika kwani mpaka sasa kivuko hicho kinafanya kazi vizuri. Aidha, kutokana na umri wa kivuko hicho kuwa mkubwa, Serikali iliweka kivuko hicho kwenye mradi wa ukarabati wa vivuko vitano unaogharamiwa na Benki ya Dunia. Mradi huu utaanza mwaka huu baada ya kumpata mzabuni kufanya ukarabati huu.

Aidha, Serikali katika Bajeti yake ya mwaka 2004/2005, ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 3.7 kwa ajili ya ununuzi wa kivuko kipya cha Kigongo - Busisi. Kazi ya ujenzi wa kivuko hiki inategemea kuanza mwishoni mwa mwezi huu. Vifaa vya kuunganisha

kivuko tayari vimefika Dar es Salaam vikiwa katika *containers 15* kutoka Uholanzi tangu tarehe 10 Januari, 2006 na utaratibu wa kusafirisha vifaa hivyo hadi Mwanza kwa njia ya reli umeshaanza. Kivuko hicho kipya kinategemewa kuanza kutoa huduma mwezi Septemba, 2006. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa matatizo ya vivuko yanafanana nchi nzima kikiwepo kivuko cha Pangani.

Je, Serikali inasema nini endapo inapotokea kuhatarisha maisha ya wananchi na mali zao na gari ikatumbukia mtoni likiwa tatizo ni la kivuko, Serikali inasemaje kuwafidia vifaa au bidhaa zilizopotea katika kivuko hicho wakati wa ajali? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, sio nia ya Serikali kuona kwamba wananchi wake na mali zao zinahatarishwa kutokana na vivuko ambavyo ni vibovu. Kwa sababu hiyo Serikali imekuwa ikijitahidi sana kwa kupitia Bajeti yake na za wahisani pamoja na hata kukopa fedha kutoka kwenye taasisi za fedha kama Benki ya Dunia kuhakikisha kwamba vivuko vinakuwa katika hali ya usalama.

Mheshimiwa Spika, ajali ni ajali na sio kwenye vivuko tu ajali inaweza kutokea mahali popote. Lakini kama inavyojulikana katika masuala ya fidia nadhani sheria katika suala la fidia la ajali inajulikana.

Kwa swali kama kuna watu wameweka Bima, Sheria ya Bima itatumika. Lakini hakuna utaratibu wa Serikali kufidia pale ambapo kunatokea matatizo kama hayo. Lakini nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itajitahidi kuhakikisha kwamba vivuko vyake vinakuwa katika hali nzuri na ndiyo maana kuna huu mpango wa kukarabati na kununua vivuko mpya nchi nzima. *(Makofi)*

Na. 33

**Kuboresha Usafiri wa Reli**

**MHE. MHONGA SAID RUHWANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa ni ukweli usiofichika kuwa njia pekee ya usafiri kuelekea Mikoa ya Kanda ya Magharibi kwa wananchi wengi ni reli; na kwa kuwa nauli ya treni imepanda kwa asilimia kumi na tano wakati huduma katika treni hizo inatisha hasa kwa daraja la tatu, kwa mfano viti havina sponji, madirisha hayana vioo, hakuna taa na vyoo vimechoka, pia maji si ya uhakika:-

Je, Serikali ina mikakati gani katika kuhakikisha kuwa usafiri huo muhimu unaboreshwa ili kuondoa adha wanazopata wasafiri?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Hali ya mabehewa ya abiria wa treni sio nzuri sana kutokana na uchakavu, uchache na uhaba wa vipuri ambao vimesababishwa na uwezo mdogo wa Shirika letu kifedha na pia kupanda kwa gharama za mafuta maradufu na hivyo kuongeza kupanda kwa gharama za uendeshaji na kupungua kwa uwezo wa shirika.

Kutokana na ukweli huo, Shirika lililazimika kuongeza nauli kwa asilimia 15% kupunguza tu pengo na siyo kukidhi mahitaji halisi ya matengenezo na uendeshaji.

Mikakati ya Serikali kuhakikisha usafiri huu muhimu unaboreshwa na huduma zinaboreka zaidi ni kama ifuatavyo:-

- Kuendelea kutengeneza mabehewa na kuyaweka katika hali nadhifu;

- Kununua injini mpya za treni kuwezesha kuwepo usafiri wa uhakika zaidi na kuongeza kipato;

- Kununua mabehewa mapya ya abiria ili kukidhi mahitaji ya usafiri na kuruhusu matengenezo kwa kiwango kinachohitajika; na

- Kukarabati njia ya reli.

Shirika letu la Reli Tanzania *(TRC)* linategemewa kukodishwa kwa mwendeshaji binafsi ambapo tunategemea kuwa hivi punde atawekeza na hivyo kuongeza idadi ya mabehewa na injini mpya kama mkakati wetu ulivyo ili kuweza kuongeza huduma na kuleta ufanisi zaidi. *(Makofi)*

**MHE. MANJU S. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Spika, lakini Shirika hili lilikuwa linaongeza nauli mara kwa mara na Mheshimiwa Naibu Waziri ametueleza kwamba nauli hizi zinaongezwa ili kuziba pengo lakini huduma bado ziko duni na nauli inaongezwa mara kwa mara. Ni lini pengo hili litazibwa ili huduma iweze kupatikana nzuri? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, naamini Mheshimiwa Manju Msambya, atakubaliana na mimi kwamba kuna kupanda kwa mafuta ambako huko kunaongezea gharama za uendeshaji wa treni. Kuongezeka kwa bei za treni si kwa treni tu peke yake hata katika mabasi bei za safari za mabasi zimeongezeka.

Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kuboresha huduma za reli kila wakati ili kuona huduma hizi zinaboreka zaidi. Lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wakati tunaboresha Shirika la Reli na usafiri kuboreka tuwaombe wananchi wetu waaminifu wawe waaminifu kwa sababu wanaendelea kukata masponji, kutoa mafeni ndani ya treni, viungio vya kufungia madirisha haya nayo hayahitaji fedha za kigeni lakini yanalitia hasara Shirika na kulifanya lisiwe na uwezo zaidi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Namwomba radhi Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, ningemtambua yeye kwanza. Kwa hiyo, tafadhali uliza swali la nyongeza.

**MHE. MHONGA SAID RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri, ninaomba niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa usafiri wa treni umeonekana kwamba una matatizo. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba barabara inayounganisha Nyakanazi na Kigoma inatengenezwa ili kurahisisha usafiri na wananchi wa Mikoa hiyo waweze kupata usafiri mbadala? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ya kutoka Nyakanazi hadi Kagoma na pia kuunganishwa na nyingine ya kwenda Kigoma imeanza katika *phase* mbalimbali. Ile ya kutoka Kagoma, Biharamulo hadi Nyakanazi imeshapata *contractor* na anatakiwa aanze mara moja katika mwezi huu gharama zake ni zaidi ya shilingi bilioni 48 na Kampuni iliyoteuliwa kuanza ni Kampuni ya Kichina. Kutoka Nyakanazi, Kasulu hadi Kigoma lile eneo linafanyiwa *feasibility study* kwa fedha zilizotolewa na Serikali, baada ya *feasibility study* baadaye ndipo tenda zitatangazwa kwa ajili ya kumpata mkandarasi kwa kujenga kwa kiwango cha juu. *(Makofi)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nilitaka kujua barabara ya Nyakanazi - Kigoma ni kweli iko kwenye *feasibility study.* Lakini ukishafanya *feasibility study* haina hakika kwamba utakuwa umepata fedha za kujenga barabara hiyo. Naomba atuhakikishie tukishamaliza *feasibility study* fedha za kujenga barabara hiyo ziko tayari? **(Makofi)**

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, wakati wowote hakuna mradi wowote ulio na fedha zilizo tayari zikisubiri mchakato wa kazi. Katika ujenzi wa barabara kwanza tunaitambua barabara, tunaipima, tunaifanyia *feasibility study* na hiyo *feasibility study* yaani mchanganuo ndio unaosema ni shilingi kiasi gani au dola kiasi gani ili ziwekwe kwenye Bajeti. Huwezi kununua nepi kabla mtoto hajazaliwa. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 34

**Tatizo la Ugonjwa Sugu wa Kipindupindu**

**MHE. LUCY F. OWENYA** aliuliza:-

Kwa kuwa tatizo la kipindupindu kilichoingia katika Jiji la Dar es Salaam kwa zaidi ya miongo miwili kimerudia tena wakati huu wa ukame:-

(a) Je, ni kitu gani kimesababisha ugonjwa huo kulipuka tena sasa?

(b) Je, Serikali ina mikakati gani ya kudumu ya kuhakikisha kuwa Jiji letu linaondokana kabisa na ugonjwa huo wa aibu kwa Taifa?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali lililo mbele yetu naomba nitoe salaam nyingi za shukrani kwa wananchi wa Jimbo la Rungwe Magharibi kwa heshima waliyonipa kwa kunipa kura nyingi na kuniwezesha kurudi hapa Bungeni. Vile vile namshukuru sana Rais wetu kwa kunipa wadhifa huu ili niweze kumsaidia katika Wizara hii ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Lucy Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Kwanza napenda nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kuwa ugonjwa wa kipindupindu ulikuwa umetoweka katika Jiji la Dar es Salaam kwa takribani miezi 10. Tangu uibuke mwezi Desemba, 2005 tulipokee wagonjwa 145 na kati ya hao wawili walipoteza maisha.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Chanzo cha milipuko ya kipindupindu katika Jiji la Dar es Salaam ni kwamba maeneo mengi ambayo wagonjwa wanatokea yanakabiliwa na tatizo la msongamano wa nyumba na maeneo hayo hayajapimwa yaani *squatter areas*. Kukosekana kwa huduma muhimu kama vile vyoo, uzoaji taka ngumu na taka maji kutoka vyooni na kwenye makaro husababisha maji taka kutitirika hovyo na hivyo kuchafua vyanzo vya maji na vyakula. Aidha, maeneo hayo yako karibu na Mto Msimbazi ambao maji yake hutumika kwa shughuli mbalimbali zikiwemo za umwagiliaji wa bustani za mboga mboga.

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa kwa sasa ambazo zimechangia kuendelea kwa milipuko wa kipindupindu ni ukosefu mkubwa wa maji safi na salama kutokana na ukame mkubwa uliotokea na hii imesababisha upungufu mkubwa wa maji katika maeneo mengi ya Jiji la Dar es Salaam.

Hii imesababisha wakazi wengi kutumia maji kutoka katika vyanzo ambavyo maji yake si salama na hasa kwenye visima vifupi na kama tunavyoelewa maeneo mengi maji yake yako juu yaani *high water table* na hivyo kuwepo uwezekano mkubwa wa kuchafuka kwa vyanzo hivyo vya maji. Aidha, wote ni mashahidi tunaona kumekuwa na uuzwaji holela wa vyakula bila kuzingatia kanuni za afya.

(b) Mikakati ya kudumu kuhakikisha kuwa Jiji letu linaondokana na ugonjwa huu wa kipindupindu ni kama ifuatavyo:-

- Jiji limetunga sheria ndogo ndogo za usimamizi wa usafi wa mazingira na kuzuia uuzaji holela wa vyakula. Tunashirikiana kwa karibu na Wakuu wa Wilaya na viongozi wa Manispaa kusimamia sheria hizi.
- Utoaji wa elimu ya afya na hili ni zoezi la kudumu na tunawashirikisha wananchi katika usafi wa mazingira na utumiaji wa maji safi na salama ikiwa ni pamoja na kuwafundisha kwamba lazima wachemshe maji wanayotumia kwa kunywa.

- Kimeundwa kikosi cha kudhibiti kipindupindu ambacho kinashirikisha sekta mbali mbali yaani *Multisectoral Cholera Task Force.* Wajumbe wanatokana na sekta mbalimbali na hiki ni cha nchi nzima kinakutuna mara kwa mara hata kusipokuwa na kipindupindu, lakini vile vile kinakutana kwa dharura kunapokuwa na tukio la kipindupindu.

- Tuko karibu na *DAWASCO* ili waboreshe upatikanaji wa maji katika maeneo haya tunayoyazungumzia lakini vile vile katika maeneo mengine ya mji wa Dar es Salaam.

- Tunajitahidi kuongeza ikama ya Maafisa wa Afya ili wawe karibu na maeneo haya na vile vile ningependa kuliarifu Bunge lako kwamba kuna mradi ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia ambao katika maeneo yaliyochaguliwa tutabomoa maeneo ambayo yamejengwa vibaya tuwe na njia za kupitisha magari ya kunyonya maji machafu na huu mradi kwa nyumba zitakazobomolewa watalipwa fidia, sio kama wenzetu wa Harare. Kwa hiyo, huu mradi umefikia hatua ya kutoa *tender* na watu sasa hivi wanaandika, wale ambao wanadhani wanauwezo wa kutusaidia katika hili.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na maji mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo kubwa la miji yetu, sio Dar es Salaam tu ni miji mingi kuna tatizo kubwa la ukosefu wa magari ya kunyonya maji machafu pamoja na kuzoa takataka; na kwa kuwa chanzo cha ugonjwa wa kipindupindu ni uchafu. Sasa je, Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii atakubaliana na ushauri wangu kwamba washirikiane na TAMISEMI ili kuhakikisha kwamba miji yetu yote inapata magari ya kuzoa taka na magari ya kunyonya maji machafu, atakubaliana na mimi hilo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, nakubalina na ushauri huo na tutauchukua na kuufanyia kazi. (*Makofi*)

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kumuuliza Waziri swali la nyongeza.

Kwa kuwa Wizara inafahamu fika matatizo yanayosababisha kuwepo kipindupindu nchini; na kwa kuwa hayajashughulikiwa, je, Waziri haoni kama ni jambo la fedheha na aibu kipindupindu kuendelea katika nchi?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, samahani sikusikia vizuri swali lake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, naomba urudie swali la nyongeza.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nasema hivi, kwa kuwa Wizara inafahamu sababu fika zinazosababisha kuwepo kipindupindu nchini, Mheshimiwa Waziri haoni kama ni fedheha kuendelea kuwa na kipindupindu nchini wakati sababu zinaeleweka na hazijashughulikiwa?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuna magonjwa mengi ambayo yanatusumbua hapa ikiwa ni pamoja na kipindupindu. Suala la *malaria* tunalo kwa muda mrefu na ninadhani kwamba suala la msingi ingekuwa mnaitibu vipi lingekuja suala la namna hiyo, magonjwa yapo. Nadhani tuangalie juhudi ambazo zinafanyika ya kwamba tunapunguza na takwimu zinaonyesha kwamba tunapunguza. *(Makofi)*

Na. 35

**Janga la Ukimwi Nchini**

**MHE. ANNE K. MALECELA** aliuliza:-

Kwa kuwa janga la ugonjwa wa UKIMWI limekuwa ni janga la nchi nzima na limeenea Mijini na Vijijini; na kwa kuwa asilimia kubwa ya wananchi wa Tanzania wanaishi Vijijini.

Je, Serikali haioni kwamba inatumia fedha nyingi sana kwa kutoa semina na warsha Mijini na kusahau kwamba waathirika walio wengi wanaishi Vijijini, mabondeni na milimani?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, majukumu ya sekta ya afya na ustawi wa jamii katika kudhibiti ugonjwa wa UKIMWI yanalenga maeneo matatu:-

(i) Kutoa elimu ya afya kwa jamii nzima;

(ii) Udhibiti wa maambukizi; na

(iii) Kutoa tiba na matunzo kwa watu wanaishi na virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, majukumu haya yanatekelezwa kwa kuhakikisha usalama wa damu katika ngazi zote za utoaji huduma, kutibu magonjwa ya ngono, kutoa ushauri nasaha, udhibiti wa maambukizi ya virusi vya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto na kutoa dawa za kupunguza makali ya ugonjwa wa UKIMWI na kufuatilia mwenendo mzima wa mlipuko wa UKIMWI.

Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba semina na warsha kuhusu UKIMWI zinazoendeshwa na Wizara ya Afya na Ustawi na Jamii zinawajumuisha watumishi wanaofanya kazi Mijini na Vijijini bila kuwabagua wananchi wa vijijini. Kwa kufafanua zaidi suala hili katika mwaka 2005, mafunzo mbalimbali yalitolewa ili kujenga uwezo wa watumishi wa afya na ustawi wa jamii katika kuwawezesha kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, watumishi katika ngazi zote walipewa mafunzo kama ifuatavyo:-

(i) Ngazi ya Hospitali za Rufaa, watumishi 29;
(ii) Ngazi ya Hospitali za Mikoa, watumishi 97;
(iii) Ngazi ya Hospitali za Wilaya, watumishi 190;
(iv) Ngazi ya Vituo vya Afya, watumishi 354; na
(v) Ngazi za Zahanati, watumishi 148 . Jumla ya watumishi ni 818.

Mheshimiwa Spika, utaona kwamba katika mchanganua huo kati ya watumishi 818 waliopata mafunzo, ni watumishi 502 ambao ni sawa na asilimia 61.4 walitoka ngazi ya Vituo vya Afya na Zahanati ambavyo viko Vijijini. Kwa maana hiyo basi, mafunzo yaliyotolewa yalilenga kutoa upendeleo kwa watumishi wa Vituo vya Afya na Zahanati ambao wako Vijijini na wanatoa huduma kwa wananchi yakiwemo mabonde na milima ya Same Mashariki.*( Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea na utaratibu wa kuhakikisha kuwa watumishi wengi zaidi wanaowahudumia wananchi Vijijini ambako ndiyo watanzania wengi wanaishi wanapatiwa uwezo wa kitaaluma wa kutoa huduma hizo kwa ufanisi na usalama.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata majibu mazuri kutoka kwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii. Lakini naomba nimuulize swali moja la nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, mimi ninafahamu vizuri kwamba Serikali inapata pesa nyingi sana za kusaidia upande wa ugonjwa wa UKIMWI, na pia nashukuru kwamba Waziri anakubali kwamba wancnhi wengi wa Tanzania zaidi ya asiliamia 80 wanaishi vijijini.

Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuweka mpango wa mzuri sana ambao utatuhusisha na sisi Wabunge wa zile pesa zinazopatikana, asilimia 80 tuhakikishe zinafika vijijini kusaidia tatizo la UKIMWI? *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali lake la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunapata fedha nyingi na Serikali inatenga fedha nyingi. Lakini nadhani vile vile unajua kwamba wakati tunaanza kupambana na huu ugonjwa tulikuwa hatuna dawa za kurefusha maisha. Kwa hiyo, tulichokuwa tunafanya zaidi ilikuwa ni semina kuwaelimisha watu wasipate maambukizi na ni kweli sasa mikakati iliyopo ni kuwafikia wananchi siwezi kusema asilimia 80. Lakini tungependa kuwafikia wananchi wote. Sasa hivi mikakati tuliyonayo ni kwamba tuwe na vipimo ambavyo vinaweza vikabainisha wagonjwa mpaka ngazi ya Zahanati. Sasa hivyo ni aghali kidogo. Lakini mpango upo nia yetu ni kumfikia mwananchi wa kawaida katika Vijiji.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, mimi naitwa Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri napenda kumuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa janga hili la UKIMWI ni la Taifa zima la Tanzania. Je, ni mpango gani uliowekwa kusaidia wagonjwa wa UKIMWI na watoto yatima walioko katika Kisiwa cha Pemba?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la afya sio la Muungano, huku Bara tuna *National Aids Control Programme* na wenzetu upande wa Visiwani wana Zanzibar *Aids Control Programme.* Kwa hiyo, wana mipango yao na sisi tuna mipango yetu lakini tunafanya kazi kwa karibu sana. *(Makofi)*

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa katika jibu lake la msingi la amesema moja ya sababu ya kudhibiti UKIMWI ni pamoja na kutoa tiba. Sasa kwa muda mrefu vipimo vya kupima UKIMWI vimeweza kusogezwa mpaka kwenye kiwango cha Zahanati mpaka Wilaya na tiba

imekuwa ikitolewa kwenye vituo tu ambavyo viliweza kuchaguliwa na Wizara kwa miaka ya nyuma iliyopita na sehemu hizo ni mbali sana na sehemu ambazo wananchi hao ambao wamepima wanaweza wakafika kupata dawa; na ukianza kutumia dawa hizi ni lazima uendelee kutumia na zinatolewa kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, sasa kutokana na matatizo ya wananchi wanaoishi vijijini imekuwa ni tatizo kubwa kufikia sehemu ambazo zinatolewa dawa.

Je, sasa Wizara ina mpango gani, pamoja na mkakati ambao imejiwekea kwa sasa na kwa juhudi za haraka sana iweze kusaidia kufikisha dawa hizi kwenye Hospitali za Wilaya ambayo itakuwa ni rahisi sana kuwafikia waathirika waendelee na tiba?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mbunge wa Mbarali, kama ifuatavyo:-

Swali alilouliza linafanana kidogo na nililolijibu hapo awali kwamba vipimo ni aghali. Lakini tunania ya kufikisha hii huduma kwa watu wote, lakini tunakwenda kwa hatua, kwamba maeneo mengine ni makubwa, kuweza kutembea masafa marefu mpaka Makao Makuu ya Wilaya ni mbali, lakini nadhani tuangalie tulikotoka na hapo tulipofika. Kuna maeneo ambayo tumeshafika hata ngazi ya Vituo vya Afya na azma yetu ni kwamba tuwafikie wananchi kwa karibu kwa kusambaza hizi huduma za vipimo pamoja na dawa mpaka vijijini.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha, kuna matangazo. La kwanza nimeombwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu nitangaze kwamba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano atahutubia wananchi wa Dodoma katika Uwanja wa Jamhuri saa 9.00 alasiri leo. Tunawaomba Waheshimiwa Wabunge wote wafike pale na wawe wameketi saa 8:30 mchana. Usafiri umeandaliwa kutokea sehemu mbili kutokea hapa na pia kutokea *Kuu street,* pale nje ya Jengo la CCM au karibu ya pale.

Nimehakikishiwa kwamba shughuli hii itakuwa imekwisha kabla ya muda wa Bunge saa 11.00 jioni. Kwa hiyo, tunaweza kushiriki na bado tukarejea kwa usafiri wa aina mbalimbali pamoja na usafiri wa mabasi ya Bunge na tukawepo hapa tukaendelea na shughuli zetu za Bunge kama kawaida kwa jioni.

La pili, Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mwenyekiti ameniomba nitangaze kwamba kutakuwa na mkutano saa 5.00 asubuhi chumba namba 428 Jengo la Utawala, ghorofa ya nne. Ni muhimu wajumbe mhudhurie kwa sababu ni kwenda kuzingatia Muswada wa *EPZ* ili tuweze kuuweka kwenye *Order Paper* wiki ijayo

Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira nayo itakutana chumba namba 219 ghorofa ya pili, saa 7.00 mchana.

Lingine ni kwamba Waheshimiwa Wabunge wote wa CCM, wanaotoka Zanzibar wanaombwa kukutana saa 7.00 mchana leo, chumba namba 231, jengo la Utawala, ghorofa ya pili.

Waheshimiwa Wabunge, lingine kuhusu msiba ambao nimeutangaza hapo mapema, Katibu atapitisha karatasi ili tuweze kuchangia ubani, yeyote atakayejisikia, hivyo tunakuombeni sana tuweze kufanya hilo. Hili ni pamoja na kama Mbunge angependa kukatwa katika posho yake basi pia inaweza kuandikwa. Lakini vizuri tengeweza kuchukua tu katika bahasha kadri itakavyoandaliwa.

La mwisho, katika uchangiaji wa Hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuhusiana na hotuba ya Mheshimiwa Rais pamoja na lile lililokwisha kubalika ambalo ni kuongeza muda wa kijadili hoja hiyo hadi Jumanne bado watakaoongea kwa hesabu walionipa wataalam mezani ni Wabunge 63 tu kati ya 90 waliojiorodhesha.

Kwa hiyo, si vema tukafanya mabadiliko yoyote hadi saa saba, kwa sababu itakuwa ni ghafla mno. Lakini tunapoanza Kikao cha jioni natarajia kumwomba Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, atoe hoja ili kupitia Kananu ya 124 kutengua Kanuni ya 49(a) ili uchangiaji sasa uwe ni dakika 10. Itakuwa ni hoja mtaiamua, hii ni taarifa tu hakuna haja ya kulalamika sasa.

Hii ni taarifa ya hoja ambayo nitamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, uzuri wa hii ni kwamba itawezesha Wabunge wote walioko kwenye orodha waweze kuchangia, ndiyo uzuri wa hii. *(Makofi)*

Ahsante, baada ya matangazo haya sasa Katibu shughuli zinazofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Hoja ya Kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa Bungeni Tarehe 30 Desemba, 2005

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, labda nisubiri kidogo Waheshimiwa Wabunge watoke.

**SPIKA:** Nadhani, na wengine wanavunja Kanuni kwa sababu wamesimama kati yako na Spika. Sasa ungegonga kengele kwanza ili tumpe haki yake Mheshimiwa Jackson Makwetta.

Kwa faida ya wenzetu Waandishi wa Habari, Waheshimiwa Wabunge wengi hivi wanatoka ni kutokana na matangazo ya zile Kamati ambazo zinahitajika kukutana. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nakushukuru wewe mwenyewe kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kutoa ushauri na maoni yangu kuhusiana na hotuba hii ya Rais ya ufunguzi wa Bunge la awamu ya nne ya Bunge letu Tukufu. Hotuba ina mambo mengi na mazito na kwa sababu ya muda itabiti tuchague maeneo machache na kuyapa uzito unaostahili.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii pia kuwashukuru wananchi wote wa Jimbo langu la Uchaguzi kwa imani waliyoionyesha kwangu kwa kunichagua ili niweze kuwepo hapa.

Mheshimiwa Spika, kabla ya uchaguzi kulikuwa na malumbano mengi ambayo yalitugawa katika makundi kama kawaida ya uchaguzi, lakini kwao wote nasema yaliyopita si ndweli tugange yajayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa ningependa kutumia nafasi hii vile vile kutoa shukrani zangu kwa Mama Salma Kikwete, Mzee John Malecela, Philip Mangula, Katibu Mkuu wa Chama, Mheshimiwa Zakia Meghji, Hilda Kibacha**,** Lucy Mayenga na viongozi mbalimbali wa Kitaifa, Mkoa, Wilaya na Vijiji kwa kufanikisha ushindi wangu, huenda bila wao nisingekuwa hapa leo. *(Makofi)*

Tatu, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa kwenu na wananchi kuwawakilisha ndani ya Bunge hili. Ninyi ni jicho na sauti ya watu *volks day, volks populis*, sauti ya watu wengi ni sauti ya Mungu. Kwa hiyo, sisi wawakilishi wa watu ndani ya Bunge hili lazima tuheshimu uamuzi wa watu na uchaguzi wa watu bila kujali wanatokea wapi.

Mheshimiwa Spika, nne ningependa kutumia nafasi hii kumpongeza Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi na wananchi wa nchi hii, kura zile zinampa motisha kufanya kazi; na hakuna heshima kubwa duniani kama kuitwa na wenzako uwaongoze kwa hiari, unaweza ukateuliwa lakini hizi kazi za kuchaguliwa na watu nadhani hakuna kielelezo kingine kwa sababu haki ya kutawala ni ya kila raia. Kila raia ana haki ya kutawala na kujitawala, lakini anakubali kukabidhi haki yake ya kujitawala kwa mtu mwingine kwa hiari. Kwa hiyo, tunawashukuru wananchi kwa imani hiyo na ni motisha kubwa kwetu. *(Makofi)*

Mwisho ningependa kutumia nafasi hii kuwapongeza Dr. Ali Mohamed Shein, Waziri Mkuu na wewe rafiki yangu Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Mawaziri na Manaibu Waziri, Wakuu wa Mikoa na viongozi wengine wote waliochaguliwa hivi karibuni kushika nafasi mbalimbali za uongozi katika nchi yetu. Kwao wote nawatakia afya njema na mafanikio katika kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo ningependa sasa niingie kwenye hotuba. Hotuba inasema mengi lakini nitachagua mambo matatu hivi na kuyatilia mkazo.

Kwanza kabisa Mheshimiwa Rais nampongeza kwa unyenyekevu wake na uungwana wake wa kutambua kazi iliyofanywa na wenzake waliomtangulia. Ukurasa wa 12 wa kitabu hiki anaelezea kazi nzuri iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Tatu kuhusu Elimu, Afya, Maji, Umeme, Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, vile vile ameelezea hali ya kifedha kwamba hatukurithi mzigo mkubwa wa madeni na pale chini ningependa kunukuu anasema: “Mapema mwaka huu Benki ya Dunia nayo ililinganisha nchi za Kiafrika kwa vigezo vya utawala

bora na Tanzania ikaibuka nchi pekee ambayo ilifanya vizuri kwenye vigezo vyote vilivyotumika katika kupima utawala bora."

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumeanza vizuri na ni vizuri tukatumia mafanikio haya kufanikisha baadhi ya mipango yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyowahi kumnukuu Isaac Newton wakati fulani, Isaac Newton aliwahi kusema hivi: "Kama mimi katika kufanya kazi hii ya umma nafanya vizuri kuliko wenzangu walionitangulia basi ni kwa sababu nimesimama katika mabega ya wenzangu walionitangulia." Naamini haya ndiyo anayosema Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Rais wetu kwa kuwanukuu hawa wenzake waliomtangulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kurasa nyingine ukurasa ule wa nane na wa tisa ambao nitatumia muda mrefu na ninaomba wenzangu tuwe pamoja, Mheshimiwa Rais ameelezea mengi labda kabla ya hapa niende mbele zaidi. Amezungumzia mpasuko katika Visiwa vya Pemba na Unguja katika ukurasa wa 18. Sijui kama ni mwiko kuzungumzia baadhi ya mambo ambayo kwa sababu nadhani hapa anaomba mawazo

Mheshimiwa Spika, Pemba na Unguja ni kama donda ndugu na baadhi ya matatizo yanayotokea kule sasa yanaanza kuenea Tanzania Bara na hatuwezi kuvulia. Kwa hiyo, ni lazima tuyakabili ikiwezekana kule kule yaliko. Ninapojaribu kuulizia wenzangu wanaotoka kule wanasema hivi, moja, kuwe na mgawanyo sawa wa mali inayopatikana ndani ya Zanzibar na kwamba mali nyingi inatoka Pemba lakini katika kutumia haitumiki zaidi Pemba. La pili, kwamba kuwe na Serikali ya Mseto kwa sababu historia inaonyesha kwamba haiwezekani hata wakati mmoja wa Uchaguzi, Kisiwa kimoja kikaongoza kwa kura nyingi zaidi kuliko kingine. Sasa sijui kama hii ni mwiko kujadili. Lakini ukiwa unazungumzia mpasuko, basi ni vizuri nalo hili tukaliona kama ni eneo moja la kuzungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kuna kitu ambacho ni cha urithi katika Visiwa vyote duniani. Watu wote wa Visiwani duniani ni watu wagumu sana kuwatawala kama Uingereza vile. Kwa hiyo, labda niachie hapo, lakini nadhani *psychology* ya mtu mfupi ni sawa sawa na mtu anayeishi kwenye dogo, wakati wowote anadhani anaonewa na vile vile lazima ajaribu kuonyesha kwamba siyo mdogo kama alivyo mdogo. Ni tofauti kama mnyama ngamia. Ngamia ni mnyama mzuri, ana nguvu lakini ni *docile,* lakini paka ni kanyama kadogo *very aggressive.* Kwa hiyo, nilitaka kusema na ndiyo maana Waingereza waliwahi kutawala dunia kutokana na hiyo *psychology* ya udogo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Zanzibar hata wasingekuwa na matatizo kati ya wao wenyewe, bado kungekuwa na hiyo tabia, hiyo siyo tu kwa sababu ya Zanzibar, ni dunia nzima. Tabia ya mdogo popote duniani inafanana. Ukimuona mtu mfupi sana, huna haja ya kuuliza. Ujue tu huyu mtu ni manunda, ni jeuri, mtashindana tu. Kwa hiyo, nasema hiyo moja. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, katika hili la mpasuko, hivi kwa nini tatizo hili linakuwa gumu namna hii? Tumelazimisha umoja, je, umoja siyo wa lazima? Nani anamhitaji mwingine? *We need each other,* lakini nani anamhitaji mwingine zaidi! Ndugu zangu katika haya mambo ni lazima tukomae. Jana mimi nimesikiliza pale katika siasa hutakiwi kuwa na adui wa kudumu na lazima ukubali kubadilika na wakati. Lakini kama unaweka mstari kwamba huyu ni adui wa kudumu na huyu wa kudumu, basi hii siasa ni kazi ngumu sana.

Kwa hiyo, nasema hii hali inakatisha tamaa. Wakati tunajaribu kutafuta suluhu, lakini imekuwa kama ni utamaduni kwamba kubadilika hapana, huyu ni *permanent CUF,* huyu ni *permanent* CCM, mpaka wajukuu na vizazi vijavyo wanabaki hivyo hivyo wanarithi hata siasa. Nadhani hili ndilo tatizo moja, sasa sijui namna gani, mimi nilidhani katika hili, Rais kama unavyoona hapa huu mpasuko huenda itabidi kuwe na Kamati ndogo ya kuchambua zaidi, vinginevyo kila Rais ataliacha hivi hivi na baadae litakuwa kubwa zaidi na litaenea. Pale Dar es salaam pale Temeke pana utamaduni mpya unafanana na ule wa kule.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka ninukuu zile sehemu za ukurasa wa 8. Pale Mheshimiwa Rais amemnukuu Rais aliyetangulia. Anasema hivi kuhusu maadili: "Tuwe na maadili yatakayotawala shughuli za kisiasa maadili ambayo hayategemei hiari ya viongozi wa kisiasa waliopo madarakani. Yatakuwa ni maadili ya miiko ya lazima yatakayobana kila chama cha siasa na wanachama na viongozi wake kikiwemo Chama tawala." Nilitaka ninukuu pale, lakini muda hauniruhusu.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa pili, kuhusu fedha tunazotumia kwenye uchaguzi, Mheshimiwa Rais anasema hivi: "Tuanze mjadala wa Kitaifa na hatimaye kuelewane kuhusu utaratibu halali ulio wazi wa chama au mgombea kutafuta fedha za uchaguzi na utaratibu halali ulio wazi wa chama au mgombea kutumia fedha hizo."

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais anapendekeza. Yale mapendekezo mawili nadhani ni muhimu sana na Serikali ingefaidika kama Waheshimiwa Wabunge tungetumia muda mrefu kuchambua yale maombi, anaomba tuchangie mawazo gani pale?

Mheshimiwa Spika, kichafu hakiwezi kusafisha uchafu. Katika hizi nchi maskini, adui mkubwa wa *democracy* ni rushwa na hapa nazungumzia uongozi wa kununua kwamba mtu anatumia fedha kununua uongozi na watu kwa sababu ni maskini hawana uhuru mwingine. Sasa kama ni hivyo kuna haja ya kwenda kufanya kampeni, si ni kupeleka fedha tu. Castro aliwahi kusema kwamba katika nchi za kijamaa madaktari huwa wanatibu ugonjwa, lakini katika nchi za kibepari, daktari anatibu fedha. Akiona mgonjwa anatikisa fedha hivi ndiyo anachangamkia na kuulizia anaumwa nini. Katika nchi za kibepari ukiwa na fedha ndiyo unapata huduma.

Sasa leo katika nchi maskini, mtu maskini haki yake ni kuchagua tu siyo kuchaguliwa. Ananunuliwa, uongozi ni wa kununua. Mheshimiwa Rais hapa amesema kama ni kweli, amesema kama ni kweli ukurasa ule wa 9 anasema hivi: "Yameanza

kujitokeza mawazo pamoja na kuanza kujengeka utamaduni kuwa uongozi unaweza kununuliwa kwa fedha.” Kama ni kweli, nadhani ni kweli.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika mazingira haya ambapo wawakilishi wa watu wamenunua uongozi na wapo hapa na tupo hapa, mimi nasema kama ni hivyo, sijui kama kuna haja ya kuwa na vyama. Vyama nchi kama hii tuwe na vyama vingi au tusiwe na vyama vingi maadamu rushwa ndiyo inayotawala, *democracy* haina maana.

Mheshimiwa Spika, wenzetu walioendelea wanatumia kuwa na vyama vingi kama ni kigezo cha kuwawezesha watu kutoa mawazo kwenye njia mbalimbali na vyama vingi. *Suppose* katika mazingira ya kwetu tunakuwa na vyama vingi lakini vyote ni *corrupt* au vina-*practise corruption*, kuna haja ya kuwa na *democracy*. Hakuna haja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika kupendekeza hili napendekeza kwamba iundwe Tume, Tume ya Kitaifa chini ya Serikali kwa sababu ukichagua CCM, *CUF* watasema hii ni kazi ya CCM ambayo itapita dunia nzima kuangalia maadili kwa ngazi mbali mbali, Waamerika wanafanyaje, Wajerumani, wanafanyaje. Halafu tutakuja kutoka hapa tuta-*extract* na wananchi hawa wanaotaka kuchangia mawazo, watachangia kwenye ile Tume kusudi tu-*come up* na kitu ambacho kitasaidia kujenga nchi hii. Vinginevyo kwa sasa bila pesa, hupati uongozi. *Passport* ni fedha na *almost* imehalalishwa. Sasa nadhani taratibu hizi ziwe *beyond,* zisiwe za chama ziwe ni za Serikali, kusudi vyama vyote vitii, maana chama kimoja hakiwezi kutii kama mambo haya ni ya kwake, kinasema mwenzake atatumia vinginevyo, ataendelea. Lakini tukiachia mmomonyoko uendelee, *this is the beginning of the end. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. HERBERT J. MTANGI:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Muheza, kwa kunichagua kwa kura nyingi kuwa Mbunge wao na vile vile kwa kuwachagua Madiwani wote wa Kata 23 katika Jimbo la Muheza kutoka Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia kwa jinsi walivyompa kura nyingi Mheshimiwa Rais na katika baadhi ya vituo Mheshimiwa Rais alipata kura nyingi zaidi kuliko Wabunge na hata kuliko Madiwani. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kuwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Amani Abeid Karume kuwa Rais wa Zanzibar.

Naomba pia nichukue nafasi hii kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa katika nafasi yako na pia Naibu Spika wako katika kipindi hiki. Naomba vile vile kuwapongeza Wajumbe wote wa Baraza wa Mawaziri kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika nyadhifa hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba tu niseme machache kwamba Mheshimiwa Rais ameonyesha kasi mpya katika kazi yake ya utendaji na naamini amepata uzoefu mkubwa sana alipokuwa katika nafasi yake ya Uwaziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na vile vile amejifunza mambo mengi amechagua yale yaliyokuwa mazuri, ameanza kuyatekeleza kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nina imani kabisa ameongeza pia upeo wake na ubunifu mkubwa katika haya mambo mengine ambayo Watanzania wengi na dunia nzima inamshangaa katika utekelezaji wake. Tunamwombea afya njema, aendelee kuwa mbunifu na aweze kutekeleza mambo mengi zaidi hasa yale aliyoahidi katika mikutano yake ya kampeni. Kwa kuwatembelea Waheshimiwa Mawaziri Ofisini kwao, kwangu mimi natafsiri kwamba ni utekelezaji wa kuhakikisha kwamba ameingia mkataba na Mawaziri hao. Ninawaomba Waheshimiwa Mawaziri, muuthamini na mtekeleze mkataba huo wa utendaji. Katika kipindi kifupi tumeshuhudia hapa Mawaziri wakijibu vizuri sana maswali. Kwa muda mfupi, Mawaziri wengine ni wageni na Manaibu wageni lakini mmeonyesha uwezo mkubwa. Tunawatakia kila la heri katika kazi yenu mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie eneo ambalo linawakabili Watanzania wengi, eneo la matatizo ya maji. Alipokuja Rais kule Jimboni kwangu Muheza alizungumza na wananchi wa Muheza na aliahidi pale katika Uwanja wa Mpira wa Jitegemee kwamba atasaidia Wilaya ya Muheza kufanikiwa kupata maji. Katika jitihada ambazo mimi nimefanya kama Mbunge, katika kipindi kilichopita niliomba mradi wa maji.

Ninaomba sasa Waziri wa Maji, na ninamwona Naibu Waziri yupo hapa, nimkumbushe kwamba upo mpango wa kusaidia Muheza kupata maji, mpango unaoitwa *Ubembe Kwemhosi Water Scheme,* upo katika Bajeti ya mwaka 2005/2006. Ninaomba mumsaidie Mheshimiwa Rais katika kutekeleza ahadi aliyoitoa Muheza kwa kutekeleza mradi huo ambao sasa upo katika Bajeti. Hadi sasa sijaona hatua zozote ambazo zimechukuliwa, kwa hiyo, naomba nikumbushe na niiaombe Wizara ya Maji imsaidie Rais katika kutekeleza ahadi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba vile vile niseme, tumesikia nia ya kutaka kuhifadhi vyanzo vya maji. Pendekezo letu kama Waheshimiwa Wabunge ni kwamba tuendelee na fikra za kupima vyanzo vyote vya maji na vilindwe. Napendekeza kazi kwamba hii ifanywe na Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na Halmashauri ambao wataweza kutoa maelekezo ni wapi vyanzo hivi vya maji vipo. Tuvipime ili visivamiwe, tuvitunze kwa sababu ni muhimu kwa uhai wetu wote.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie eneo la pili ambalo pia Mheshimiwa Rais amelizungumza katika hotuba yake, eneo la umeme. Wakati Mheshimiwa Waziri alipokuwa akitoa taarifa yake ya hali ya umeme nchini, nilitoa mapendekezo kadhaa, lakini kwa sababu muda ulikuwa mfupi, Mheshimiwa Waziri hakuweza kuyajibu yote. Nayarudia leo.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Gesi ya Songosongo, *TANESCO* wamekuwa wakiilalamikia Kampuni ya *Songas* kwamba wako nje na nyuma sana ya utekelezaji wa mradi wao kimkataba. Ni hatua gani Serikali inachukua kuhakikisha kwamba *Songas*

wanatekeleza majukumu yao kufuatana na mkataba jinsi ulivyo. Katika hali hii ngumu ya matatizo ya umeme ni vema tukasimamia mikataba yote kikamilifu. Kuna upungufu wa umeme nchini, *Songas* katika mkataba wao wanatakiwa kuweka kituo cha umeme pale Ubungo. Hili wamelitekeleza, lakini ndani ya mkataba ule vile vile yapo maeneo mengine ambayo *Songas* wanatakiwa kimkataba waweke vituo vingine vya kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, je, tumefuatilia ni kwa nini bado *Songas* hawajatekeleza hayo mambo ambayo yatasaidia sana katika kupunguza tatizo la umeme kwa kuongeza uzalishaji wa umeme. Naomba Serikali ifuatilie hayo. Lakini vile vile *IPTL,* tumewaomba *IPTL* wabadilishe mfumo wao wa uzalishaji, badala ya kutumia mafuta, watumie gesi. Gesi ya Songosongo na mabomba ya Songosongo sasa yako nje ya milango ya *IPTL,* lakini bado kazi hiyo haijafanyika. Kwa nini majadiliano hayo yanachukua muda mrefu? Kuna matatizo gani ndani ya mkataba wa *IPTL* hata tushindwe kuwafanya *IPTL* watumie gesi badala ya kutumia mafuta ambayo yanalipa taifa hili gharama kubwa.

Ndugu zangu, katika mkataba wa *IPTL,* pamoja na kwamba anayeuza umeme na kuzalisha umeme ni *IPTL,* ndani ya mkataba ule, gharama zile kubwa za mafuta zinazotumika kuzalisha umeme, zinalipwa na *TANESCO* anayenunua umeme, siyo yule anayezalisha umeme. Sasa tuangalie, tuchambue mikataba hii, ndiyo mikataba ambayo inatuletea matatizo makubwa katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna Kampuni inayofanya utafiti wa kuzalisha gesi kule *Mnazi Bay*. Kampuni hii vile vile katika utaratibu wake imeomba ianzishe ujenzi wa kituo cha umeme. Tumefikia wapi kuiwezesha kampuni hiyo kuanzisha kituo hicho cha umeme wakati huu ambapo tuna matatizo makubwa ya umeme. Kama kuna matatizo, tujaribu kuyatatua, tutoe kibali, kampuni ianzishe uzalishaji wa umeme ambao umekusudiwa kuondoa tatizo kubwa la umeme katika eneo la kusini mwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie hali ya usalama. Hali ya usalama inatisha na ni kweli. Lakini jambo moja ambalo linatupa wasiwasi mkubwa zaidi ni kwamba Tanzania sasa imepewa nafasi kubwa ya kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Tutakaaje katika kiti hicho kama sisi wenyewe usalama ndani ya nchi yetu bado unatusumbua? Basi tujenge mazingira mazuri, tujenge mfumo mzuri, tuhakikishie wananchi wetu usalama wa mali yao ndiyo tuweze kukaa kwa kujivuna katika kiti kile cha Baraza la Usalama.

Naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza sana askari polisi wa Wilaya ya Muheza kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya kupambana na majambazi, wamefanikiwa sana. Muheza palikuwa ni eneo tulivu, lakini limeanza kuvamiwa na ujambazi kutokana na kupatikana kwa dhahabu ambayo sasa inachimbwa kiholela. Wamekuwa wakipambana na wahalifu na sasa majambazi wanawatafuta polisi. Tuwape zana za kutosha kama wenzangu walivyozungumza ili waweze kulinda maisha yao na kulinda maisha ya raia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa pia nizungumzie suala moja linalohusu gharama za Mbunge. Kwa muda mrefu mambo yamekuwa yakizungumzwa kuhusu mapato tu ya Mbunge, lakini kwa taratibu na kanuni ya fedha unapozungumzia mapato, lazima utizame vile vile gharama na matumizi. Sasa watu wamekuwa wakizungumza upande mmoja tu. Kanuni za fedha zinasema katika kila *transaction* moja kuna upande wa *debit* na upande wa *credit*. Sasa mtaalam anayejua fedha hawezi akazungumzia upande mmoja tu wa *debit* akaacha kuzungumzia upande wa *credit*. Huu siyo utaalam wa fedha, ni mapungufu. Kwa hiyo, mimi nitajaribu kuzungumzia gharama chache tu zinazoonyesha upande wa pili. Kama wao walikuwa wanazungumzia *credit* kama mapato, sasa nitazungumzia upande wa pili, *debit*.

Mheshimiwa Spika, katika kikao cha Bajeti kwa mfano, siku 60 ambazo Mheshimiwa Mbunge anakuwepo hapa Dodoma, analazimika kujigharimia yeye mwenyewe mahali pa kulala, kwa chakula na kila kitu. Kwa wastani wa nyumba au hoteli zilizopo kwa 10,000/= tu kwa siku kwa siku 60, Mbunge huyo atakuwa ametumia 600,000/= katika kipindi cha Bajeti kwa siku 60, laki sita na ukichukua tu wastani mdogo tu wa chakula, matumizi ya chakula kwa siku hizo hizo 60 kwa 10,000/= tu kwa siku, Mbunge atakuwa ametumia shilingi nyingine 600,000/= jumla milioni moja na laki mbili. Hapo hujaweka tatizo ambalo lazima tuliangalie kwa undani sana. Dereva wa Mbunge analipwa na Mbunge mwenyewe. Unapokuja na dereva hapa, basi lazima uhakikishe kwamba utamlipia malazi, utamlipia chakula. Chukua nusu tu ya gharama hizo za Mbunge 1,200,000/= kwamba dereva wake atatumia nusu ya gharama hizo ni 600,000/=, ukizijumlisha hiyo ni 1,800,000/= na zaidi. Lakini lingine ambalo lazima tulikumbuke ni kwamba kwanza Mbunge analipwa mshahara kufuatana na Kanuni ambazo zipo na mshahara wake ni mshahara ambao upo ndani ya *scales* za Utumishi wa Umma, mshahara huo ni *LSS(P)2. (Makofi)*

Kwa hiyo, siyo mshahara ambao haujulikani, ni mshahara ambao upo katika *scales* za Serikali. Lakini ni mshahara ambao unalipiwa kodi vile vile na nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba kodi anayolipa Mheshimiwa Mbunge kwa mwezi ni wastani wa shilingi 230,000/= Kwa mwaka kodi hiyo ni shilingi 2,760,000/=. Kwa hiyo, hizo ni sehemu za gharama. Lakini hebu mchukue mfanyabiashara ambaye kipato chake ni zaidi ya 15,000,000/=, Mbunge hajafikia 15,000,000/= hizo kwa mwaka. Huyu kodi yake ya mapato kwa mwaka ni wastani wa 500,000/=. Mbunge ambaye hapati zaidi ya hizo, analipa 2,760,000/=. Huyu kodi yake ya mapato haizidi 500,000/=. Hili halizungumzwi, linalozungumzwa ni mapato ya Mbunge.

Mheshimiwa Spika, ukichukua na gharama nyingine, sasa utaona kwamba kiasi kinachobaki mfukoni mwa Mbunge ni kidogo na kwa kweli hakistahili hata kuzungumziwa. Sasa zaidi sitakwenda huko, lakini naomba niseme hata Mheshimiwa Rais hivi karibuni amesema, hii mishahara tunayoizungumzia hapa iangaliwe upya. Maana yake ni kwamba mshahara huu wa utumishi ambapo vile vile Mbunge yumo ndani, maana yake ni kwamba wote tuangaliwe upya. Sasa sijui watamweka wapi Mbunge wakati wanaangalia mishahara hii ambayo ipo ndani ya utumishi na *scales* za umma na Mbunge ni mtumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, niseme machache kuhusu elimu, matatizo na gharama kubwa za walimu zinatokana na jinsi tulivyokasimu madaraka ya kuhamisha walimu. Kwa hiyo, gharama kubwa ni za madai ya kuhamisha walimu. Tuangalie sasa kwa makini, haya madaraka tuliyoyakabidhi kwa Maafisa wa Elimu ambao kila siku wanahamisha walimu. Mwalimu mmoja atapata uhamisho mara tatu kwa mwaka. Gharama zote za uhamisho zinabewa na Serikali.

Kwa hiyo, maana yake ni kwamba Maafisa Elimu hao wa Wilaya na Mkoa ndio wanaotengeza gharama hizi ambazo baadae zinabebwa na Serikali, hivi hatuwezi kuangalia tathmini, tukasimamia vizuri ili tukapunguza mzigo mkubwa huu ambao kwa kweli chimbuko lake ni Maafisa wa Elimu wa Wilaya ambao wanafanya kazi hizo walizokasimiwa madaraka na wanayatumia vibaya.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu muda unakaribia kuisha, basi naomba niseme kwamba nakushukuru sana kwa nafasi hii uliyonipa niweze kuchangia na kwa leo haya machache yanatosha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyeweza kunijaalia uzima na afya asubuhi hii nikaweza kusimama hapa na mimi nikasema mawili matatu kuhusu hotuba ya Mheshimiwa Rais. Baada ya shukrani hiyo, pia nichukue nafasi hii kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Ziwani kwa kukubali uteuzi wa chama chao mie kuwa mgombea wa Jimbo hilo na hatimaye wakanipitisha kwa kura nyingi za halali.

Mheshimiwa Spika, tatu, nakushukuru na wewe asubuhi hii kwa kunipa nafasi hii na mimi nikachangie katika hotuba hii. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama muda utaniruhusu, nakusudia kuzungumza mambo matano. La kwanza, ni la mpasuko kati ya Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuliona tatizo hili na akaona kwamba ni upungufu katika utawala wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nini historia ya mpasuko huu? Nchi yetu iliingia katika vyama vingi, uchaguzi wa kwanza wa vyama vingi tukaufanya mwaka 1995. Wapemba wakaupokea mfumo huu na kwa kweli ilikuwa ni haki kuchagua upande wanaoutaka wakachagua Chama cha Wananchi, hawakujua kuwa kumbe walifanya kosa kuchagua Chama cha Wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuanzia hapo, kilichofuata ni mateso, bughudha, unyanyasaji na kila namna juu ya Wapemba kwa kuwa tu hawakuchagua Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, kilichofuata baada ya kumalizika uchaguzi huo ni Wapemba kufukuzwa kazi, Wapemba kupigwa katika maeneo yao ya mazungumzo, Wapemba kufanyiwa kila namna ambayo kwa kweli hastahili binadamu wa kawaida kufanyiwa.

Hali ikaenda hivyo hivyo, pakafanywa Muafaka, nasikitika kwamba Muafaka ambao haukuleta manufaa yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukaenda katika kipindi cha pili, 2000. Hali ikawa mbaya zaidi na Serikali ya wakati huo ilifikiria labda kuwawekea ngumu Wapemba, inaweza ikawabadilisha msimamo wao. Lakini kumbe ilikuwa ni kuwanoa zaidi. Sisi tulitarajia kwamba kwa kuwa walishashinda, basi wangewafanyia mema Wapemba, lakini badala yake ndiyo wakawafanya maovu juu ya maovu na Wapemba nao wakaendelea kuikataa SMZ na kwa hivyo SMZ itaendelea kuwabagua Wapemba.

Mheshimiwa Spika, Wapemba hawajajibagua. Lakini Wapemba wanabaguliwa na bahati mbaya siyo CCM inayowabagua Wapemba, SMZ ndiyo inawabagua Wapemba na nitatoa ushahidi. Katika kipindi hicho hicho cha mwaka 2000 yakatokea mambo mabaya zaidi. Wapemba hao hao wakapoteza roho, wakapoteza mali na hali na wengine mambo waliyofanyiwa hayasemeki, sina haja ya kuyasema hapa. Lakini bado SMZ haikutanabahi katika kipindi hicho ikaendelea kuwawekea ngumu Wapemba.

Tukaenda katika kipindi hiki cha juzi cha uchaguzi wa mwaka 2005, hali kwa kweli ya uchaguzi ilivyokuwa ni ya kusikitisha. Kwa hiyo, Wapemba kwa kweli tukikataa SMZ tusilaumiwe, tuna sababu za msingi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama si kutubagua ni nini? Nitatoa mfano. Serikali ya sasa iliyopo ya Mheshimiwa Amani Abeid Karume ina Mawaziri zaidi ya 18, lakini katika hao Mpemba ni mmoja, tena mwanamke, yeye ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, anayeshughulikia Kazi Maalum. Hata hatujui kazi hizo maalum ni zipi! Maana hata ukiwa na shida wewe unataka kwenda kwa Waziri huyu hujui sasa uende kwa shughuli gani, maana ni shughuli maalum tu, tena haikuwekwa wazi. Sasa jamani eti hapo Wapemba wanajibagua au wanabaguliwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali hiyo hiyo ya Mheshimiwa Amani Abeid Karume, ina Makatibu Wakuu na hali ni hiyo hiyo, ina Manaibu Waziri, hali ni hiyo hiyo, ina Wakuu wa Mikoa watano, hakuna Mpemba hata mmoja, hata wa CCM hakuna! Ina Makamishna, ina ma-*RPC* wa Mikoa mitano, hakuna Mpemba hata mmoja, hata anayetoka CCM hakuna! Sasa katika hali kama hiyo Waheshimiwa mtalaumu vipi Wapemba? Je, mtasema Wapemba wanajibagua au Wapemba wanabaguliwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais, kaonyesha nia nzuri sana ya kulitafutia ufumbuzi suala hili. Nasema si kazi rahisi kulitafutia ufumbuzi suala hili. Lakini Mheshimiwa Rais kwa kuwa nia yako ni njema katika hili, sina shaka Mungu atakusaidia na sisi tuko tayari kukusaidia katika hali yoyote itakayokuwa, lakini nakutanabaisha kwamba, utakutana na vikwazo vingi vya kulitafutia ufumbuzi suala hili na ninakuhakikishia kuna baadhi ya viongozi wa SMZ wanataka tufikie mahali tukubaliane, twende kama wenzetu katika nchi nyingine. Lakini pia kuna baadhi, suala hili kwao ni biashara na hawako tayari kuona kwamba tunafika mahali Wazanzibari, Wapemba na Waunguja tunakuwa kitu kimoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo likiwepo Zanzibar, bado ni aibu kwa Tanzania. Kwa hiyo, ndiyo maana hata mauaji yaliyotokea mwaka 2001 yaliitia dosari Tanzania nzima, si Zanzibar tu kabisa. Kwa hiyo, tukipata ufumbuzi wa kudumu basi kwa kweli tutakuwa tumeiokoa Tanzania kwa ujumla. Lakini tukikaa na kuonyesha tu jazba kisiasa hazitatufikisha popote. Naomba tuache jazba za kisiasa, tukae pamoja kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa suala la Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wapemba ni sawa sawa na binadamu wengine, wana haki zote kama walivyo watu wengine. Basi katika jambo hili, ninamshauri Mheshimiwa Rais aunde Tume. Tumeunda Tume za vyama na wakakaa muda mrefu, hawakufika mbali. Namshauri Mheshimiwa Rais, katika kutafuta ufumbuzi wa suala hili hasa kwa kuwa si tatizo la CCM na *CUF,* ni tatizo la Pemba na Unguja kama alivyolisema mwenyewe, naomba atumie Waheshimiwa Wabunge kutafuta ufumbuzi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naamini kwamba tutapata kitu cha kutumia na tutasahau yote yaliyopita nyuma. Namwomba Mwenyezi Mungu amsaidie Mheshimiwa Rais Kikwete katika kutafuta ufumbuzi wa suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, katika suala hili hili, labda nimalizie kwa kusema kwamba uongozi Waheshimiwa Wabunge ni dhamana na tutaulizwa siku ya siku. Injili au Biblia inasema kwamba kila mtu atabeba mzigo wake mwenyewe. Hali kadhalika *Quran* inasema *Izaa zul zilatun wizira-uhla,* tafsiri ni hiyo hiyo. Kwa hiyo, kila tunapokaa Waheshimiwa viongozi, tukae tukifikiria hivyo kwamba kuna siku tutaulizwa kama viongozi kwa yote ambayo tumeyatenda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, la muhimu ni vitendo si maneno. Tunaweza kukaa tukasema maneno mengi sana hapa, lakini vitendo vyetu je, ndivyo? Kwa hiyo, baada ya kumaliza hiyo nataka nisimalize muda kwa sababu nina mambo mengine nichangie.

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo nataka nichangie ni suala njaa. Kwanza, nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwa hatua ambazo inachukua kukabiliana na tatizo hili. Njaa ni tatizo. Njaa anaijua mtu mmoja, mmoja. Yule anayeathirika ndiye anayejua njaa hasa kuliko mwingine. Serikali inajaribu kufanya mikakati mbalimbali katika kukabiliana na hali hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri mambo mawili. La kwanza, pamoja na chakula cha akiba ambacho tunacho na wafanyabiashara ambao Serikali inawaruhusu kuagiza ili kuokoa hii hali, ni vizuri na hicho chakula ambacho tunacho tukitumie katika utaratibu mzuri. Kuna hali ya kusikitisha hasa katika Serikali chini huko kwenye vijiji na vitongoji kutumia chakula kwa ajili ya starehe, nakusudia pombe. Wanatumia mahindi, mtama na vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, akiba ile tuliyonayo ni ndogo, kama tutaitumia kwa shughuli za starehe kwa kweli haitatusaidia badala yake itatuongezea mzigo kwa sababu pombe si chakula kwa vyovyote utakuwa unakunywa pombe baada ya kushiba. Kwa hiyo, tuweke

huduma ya chakula kwanza, halafu ndiyo tuje na starehe. Basi ni vizuri Serikali ikawa macho na ikawa makini kuhakikisha kwamba hizi taratibu za upikaji wa pombe za kienyeji kwa kutumia vyakula zinakoma hasa katika kipindi hiki ambacho nchi yetu inaelekea katika hali ngumu ya chakula. *(Makofi)*

La tatu, napenda nizungumzie suala la rushwa. Rushwa kwa kweli ni tatizo, ni tatizo kubwa kabisa katika nchi yetu na si nchi yetu tu, lakini katika dunia kwa ujumla. Taasisi imeundwa katika suala la kuzuia rushwa, lakini bado inaonekana ni tatizo kabisa kabisa. Nakumbuka nilisimama mara mbili kama si tatu humu Bungeni kuchangia suala hili, lakini kuna viongozi wakuu hasa katika mambo ya mashirika haya ambayo kwa kweli hawa ndiyo ambao wanaturudisha nyuma katika suala hili.

Kwa hiyo, Serikali kuwa wakali kwa wale wafanyakazi wa chini tu haisaidii kupunguza rushwa, ni vema ikaandaa mkakati maalum kushughulikia na rushwa nene, nene. Hawa kwa kweli ndiyo wanaorudisha maendeleo ya kiuchumi na maendeleo ya kidemokrasia nyuma katika nchi kutokana hasa na hizi rushwa za hali ya juu. Nashukuru kwamba Serikali ya Awamu ya Nne inakusudia kupitia upya mikataba ya mashirika na hasa ya madini ambapo hapa ndiyo kwenye kiini cha suala la rushwa. Naitakia Serikali kazi njema katika kufuatilia suala hili angalau kupunguza kasi hii ya rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la nne ni suala la UKIMWI. Suala la UKIMWI liamezungumzwa sana hapa. Tulishafanya makongamano mengi na warsha nyingi, lakini bado kasi ya UKIMWI inaongezeka siku hadi siku. Kwa kweli tuna watu wengi ambao wameathirika. Sasa nadhani nguvu kubwa za hii misaada ya UKIMWI basi tuifikishe kwa waathirika moja kwa moja badala ya kupeleka kwenye makongamano na warsha ambazo kwa kweli tija yake katika kuzuia UKIMWI ni ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la tano ni kuhusu ujambazi. Nashukuru kwamba Serikali inalichukulia suala hili kwa nguvu zote katika kuikabili hii hali. Tuwape moyo wenzetu wanaoshughulika na usalama wa raia katika kuhakikisha kwamba wananchi wetu wa Tanzania na mali zao zinakuwa katika hali ya usalama. Lakini pia si sahihi kulaumu tu askari kama wengi ambao wametokea kuwalaumu, lakini tutazame na hali yao iko vipi katika utendaji, hali ya maisha yao na huduma zao, kwa kweli ni ya kusikitisha. Askari Polisi kwa kweli…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Naibu Spika na Spika kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi. Hii inadhihirisha kwamba Wabunge wanayo imani kubwa na wanategemea uongozi thabiti kutoka kwenu na hii inaonyesha kwamba tuko tayari kufanya na nyie kazi hii tuliyokabidhiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza vile vile Mawaziri, Manaibu Waziri na Wakuu wa Mikoa kwa uteuzi walioupata. Waheshimiwa Wabunge wote nawapa hongera, kazi ya kutafuta kura ilikuwa ngumu sana. Kwa hiyo, nawapa hongera kwa kuchaguliwa kwenye sehemu zenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niwashukuru wanawake wote wa Mkoa wa Kagera walionipa kura. Vile vile, nawashukuru wananchi wote ambao walikichagua Chama cha Mapinduzi, wakakipa ushindi mkubwa, asilimia ikatosha na mimi nikaweza kuingia Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri ambayo imejikita katika nyanja mbalimbali zinazomgusa kila Mtanzania. Kwenye hotuba hiyo ametaja wazi kwamba kwa muda mrefu kilimo kitaendelea kuwa uti wa mgongo wa uchumi wa Mtanzania kwa maana ya kutupatia chakula, mazao ya kuuza na malighafi za viwanda. Ndiyo maana sasa hivi tunahaha kwa sababu chakula hakipo kwa sababu hatujaitumia hiyo fursa kwa kuwa kilimo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wanategemea kilimo na hawa ndiyo wanaishi vijijini na hawa ndiyo maskini sana. Kwenye Ilani ya Uchaguzi tunapozungumzia maisha bora kwa kila Mtanzania, nina uhakika tunazungumzia kila Mtanzania wakiwemo na hawa wakulima ambao wengi wao ni maskini. Kama tunataka kuboresha maisha yawe bora kwa kila Mtanzania, sasa wakati umefika tuelekeze nguvu zote na tupange mipango mikubwa kwa ajili ya kuboresha hicho kilimo. Wasi wasi wangu ni kwamba wakulima wengi hadi sasa wanaendelea kutumia jembe la mkono ambalo hata babu mzaa babu yangu alikuwa anatumia jembe hilo hilo kwa Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Spika, katika dunia ya utandawazi tunadanganyana. Haiwezekani tukamsaidia huyu mkulima akaweza kupata maisha bora kama ataendelea kulima kwa jembe la mkono, utakuta anatumia mwezi mmoja au miwili kulima eka moja. Sasa hicho chakula atakachokipata kutoka kwenye eka moja kweli kinamtosha kuweza kujipatia chakula na akaweza kuendesha maisha yake? Sidhani kama inawezekana.

Namshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu sasa hivi ameahidi kutoa fedha nyingi kwa ajili ya kupanua kilimo cha umwagiliaji. Sasa nilikuwa najiuliza, hayo mashamba yatakayomwagiliwa ni yale ambayo yatakuwa yanalimwa kwa jembe la mkono au ni vipi?

Mheshimiwa Spika, naomba nipendekeze kwa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na bahati nzuri Waziri wake namfahamu, kwa maana nimefanya naye kazi. Mnazungumza mambo ya *Standards and Speed,* kwa *speed* ndiyo mwenyewe, Mheshimiwa Mungai, tunaomba sasa upangwe mpango mkubwa wa kupeleka matrekta huko vijijini kwa sababu Serikali ilipoamua kwamba sasa hivi *main roads* zote lazima zijengwe kwa kiwango cha lami iliwezekana na tunajua kwamba huu mradi ulikuwa ni mkubwa sana. *Statistics* tulikuwa tunasikia Mheshimiwa John Magufuli, anazitoa hapa,

iliwezekana, fedha zilipatikana na huo mradi ulifanyika. Sasa wakati umefika wa kupeleka matrekta huko vijijini.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwamba tulime kitaalam, tupalilie kitaalam na tuvune kitaalam. Hii idara ya hali ya hewa badala ya kila siku kuwa wanatwambia mvua za rasharasha zitanyesha kesho katika mkoa wa Kagera na mikoa yote iliyozunguka Ziwa Victoria, basi wawashauri wakulima maana sasa hivi wamechanganyikiwa. Wakati wanapotegemea kulima ndiyo mvua hakuna, wakati wanapotegemea kuvuna ndiyo mvua zinanyesha. Sasa tunaomba idara hii iwashauri wakulima kwamba, kufuatana na utaalamu tunaona mvua katika mkoa wa Kagera, katika mkoa wa Ruvuma zitaanza kunyesha mwezi fulani kusudi hawa wajiandae kulima. Wote tukubaliane kwamba hali ya hewa imebadilika sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha hiyo sekta nashauri vile vile kwamba ruzuku ipelekwe kwa wakulima na utafiti uendelee kufanywa, tusiendelee kulima kwa kutegemea mvua. Sasa hivi kuna kitu kinazungumzwa juu ya *artificial rain formation.* Tunaomba huu utafiti ufanywe haraka kusudi tuweze kuona kama tuna uwezo wa kutengeneza mvua kusudi kuweza kuboresha kilimo. Kama tutaboresha kilimo, hao wakulima wakapata mazao, lakini wakikosa mahali pa kuyauza itakuwa ni kazi bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwa upande wa mkoa wa Kagera. Zao ambalo linafahamika unaweza ukaliuza wapi ni hizi *cash crops* kama kahawa. Tukubaliane kwamba kahawa bei yake imeteremka sana na labda ndiyo maana umaskini umeongezeka sana katika mkoa wa Kagera. Lakini kuna mazao mengine kama mahindi na maharage.

Kwanza hayo yanavunwa mara mbili kwa mwaka, kahawa inavunwa mara moja na sasa hivi bei ya maharage na ya mahindi hata kabla ya njaa ni kubwa kuliko ya kahawa. *Why don't we promote* mahindi na kahawa na tukahakikisha kwamba kuna *buying centers* ambazo zimekuwa *introduced* na Serikali ili huyu mkulima akaweza kuuza mazao yake?

Sasa hivi akishapanda na akavuna tunamwachia walanguzi wanamlangua, anauza kilo kwa shilingi mia moja au mia moja hamsini anaendelea kuwa maskini. Huyu *middleman* anayenunua kutoka kwa mkulima ndiye anapata faida kwa sababu anaenda kuuza mahali pengine. Kwa hiyo, nafikiria kwamba tutengeneze *buying centers* kwa ajili ya haya mazao mbadala. Hayo mazao yanaweza yakakaushwa yakawekwa kwenye hifadhi ya Taifa na huyo mkulima sasa atakuwa amepata maisha bora, kwani atakuwa ameuza kwa bei nzuri na inayoeleweka.

Waheshimiwa Wabunge, nafikiri wakati umefika wa kutafsiri hotuba ya Rais kwa vitendo. Tungependa kujua Wizara ina mipango gani katika hii ari mpya na nguvu mpya ya kununua matrekta kupeleka vijijini na kutafuta masoko kwa mazao mbadala.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe pongezi zangu kwa Serikali ya Awamu ya Tatu kwa kuanzisha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi ambao umeboresha elimu ya msingi, ukatoa fursa kwa wanafunzi ambao wangekosa kwenda shule, sasa hivi wanakwenda shule. Kweli ukiangalia sasa hivi mashule yetu ya msingi yanapendeza, yamejengwa mengi, yamekarabatiwa, walimu wameongezeka na ruzuku ya kuendesha shule hizo inatolewa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mimi kabla sijawa Mbunge nilikuwa mkuu wa shule kwa kipindi kirefu tu. Nataka niwahakikishie kwamba elimu inayotolewa kwenye shule zetu ni bora, si kweli kwamba watoto wanaosoma kwenye shule zetu hawapati elimu bora na hata watoto wetu wakitoka hapa wakaenda kusoma kwenye shule za nchi jirani au kwenye Mataifa mengine unakuta wanafanya vizuri au vizuri zaidi kuliko hata wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari ndiyo umeanza, nafikiri uko kwenye mwaka wake wa pili. Kuna matatizo makubwa sana kwa nia nzuri tu, ni kwa sababu ya maendeleo ambayo yamejitokeza katika elimu ya msingi. Elimu ya msingi ilipanuliwa haraka sana kuliko elimu ya sekondari, ndiyo maana sasa hivi tunashuhudia shule hazitoshi, madarasa yamejaa sana, walimu hawatoshi. Napendekeza kwa Serikali kwamba sasa hivi wapeleke ruzuku za uendeshaji mashuleni kwa wakati unaotakiwa kwa sababu nafikiri mpaka sasa hivi hawajaanza kupeleka kwa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, hii ruzuku ya maendeleo ya kujenga shule ina *element* ya kuchangia. Wanapopeleka shilingi milioni 7 kwa ajili ya kujenga darasa hazitoshi, kwa hiyo, mwananchi anatakiwa kuchangia kwa sababu darasa ni pamoja na *furniture,* siyo kuta tu. Lakini tatizo linakuja unakuta kwamba wananchi hawachangii, hakuna *community contribution.* Kwa hiyo, unakuta zile shilingi milioni 7 zinakuwa hazitoshi. Naomba iwe changamoto kwa Wabunge tukishirikiana na Madiwani na Halmashauri zetu, Kata zetu na vijiji vyetu tuone namna gani ya kuweza kuhamasisha wananchi ili waweze kuchangia hiyo *community contribution* kusudi majengo hayo yaweze kujengeka na tuboreshe elimu yetu ya sekondari.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Wizara ya Elimu kwa mpango mzuri wa ku-*train* walimu kwa sababu tunaelezwa kwamba kila mwaka sasa hivi watakuwa wana-*train* walimu wengi maelfu kwa maelfu. Walimu wengi wanaopelekwa kule shuleni hawakai au hawaendi *especially graduate teachers,* kwa sababu ya maslahi ambayo ni finyu.

Naomba nitoe mfano kwamba mwalimu *graduate* anapomaliza Chuo Kikuu akapelekwa kuwa mwalimu, mshahara wake anaanza na shilingi laki moja na nusu. Ni hela ndogo sana! Hawa walimu wanatoroka wanaenda kutafuta mahali ambapo kuna *green pastures. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapendekeza kwamba maslahi ya walimu walio mashuleni na walio maofisini yaboreshwe na ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu

amesema kwenye hotuba yake kwamba ataboresha maslahi ya wafanyakazi, basi ikifika huo wakati maslahi ya walimu yaangaliwe.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wanawake, wote mmeona akinamama walivyotusaidia kwenye kampeni na hiyo ikaonyesha kwamba mama akiamua atatekeleza kweli na atafikia malengo. Lakini wanawake hao hao ndiyo maskini kuliko kila mtu kwenye familia. Wanafanya kazi sana na ni maskini wa mwisho. Ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwani kwenye hotuba yake ameahidi kwamba atawawezesha wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo ninaloliona ni kwamba haya yanaweza yakabakia yakawa maneno mazuri tu kwenye sera na kwenye hotuba. Inabidi uwe ni mpango mkubwa kwa sababu wanawake ni zaidi ya asilimia 51 ya wananchi wanaoishi katika Tanzania hii na wengi wao ni maskini. Sasa mnaposema itakuja hii mifuko, hii mifuko inaweza kuishia Dar es Salaam au katika makao makuu na wajanja wachache wakaipata tukashindwa kuwafikia wale akinamama walio kwenye *grassroots.* Napendekeza kwamba hiyo mifuko ya kukopesha vikundi mbalimbali na akinamama mmoja mmoja ipelekwe kwenye ngazi ya Wilaya. Kila ngazi ya Kata basi, akinamama wafungue *SACCOS* wachangie, lakini na Serikali iwe tayari ku-*inject in funds.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inapofika hii Bajeti ambayo sasa hivi iko kwenye *stages* mbalimbali za kuandaliwa, hii ndiyo Bajeti mwananchi anaingoja kwa hamu kwa sababu ndiyo Bajeti ya ari mpya na nguvu mpya. Tungetegemea basi kwamba kwa kila *section* tutaona ni namna gani watakavyoweza kuboresha hali ya mwanamke. Kwa hiyo, tunategemea kwamba kutakuwa na *portion* kubwa ya Bajeti ambayo itakuwa inaenda kuinua hali ya mama ambaye ana kipato kidogo.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kagera naomba utazamwe kwa ajili ya usalama wa raia. Kwa miaka minne/mitano iliyopita tulikuwa tunapata *police escort* kutoka Wilaya moja kwenda nyingine, sasa hivi ni zote. Ukitaka kutoka Bukoba, kwenda Karagwe *police escort,* Karagwe kwenda Ngara, *police escort,* Ngara kwenda Biharamulo, *police escort*. Sasa hivi hakuna *police escort* kati ya Bukoba na Muleba, lakini watekaji wameanza. Hii ni kwa sababu Mkoa wa Kagera umezungukwa na Burundi, Rwanda na Uganda ambako kote kulitokea vita, wakimbizi wakaja wakaingia kwenye hiyo misitu.Napendekeza kwamba sasa hili tena siyo suala la polisi, lipelekwe Jeshi, likavamie lile pori na siyo kwa mara moja na kurudi, wakae kule kule mpaka wahakikishe kwamba wamewaondoa majangili wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja ya hotuba ya Rais. *(Makofi)*

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hii hotuba ya Mheshimiwa Rais. Lakini kwanza, kwa sababu jina la Sigonda huwa linawatatanisha sana watu, naomba nijitambulishe rasmi. Mimi jina langu ni Guido Gorogolio Sigonda. *(Kicheko)*

Tatizo la jina kwa kweli limeanza mbali sana. Gologorio maana yake ni Gregory. Sasa Gregory, baba yangu alibatizwa wakati alipokuwa mdogo. Alipokuja kujua kwamba jina ni Gregory akashindwa hata kutamka Gregory. Kwa hiyo, yeye akaanza kulitamka wa kilugha, Gorogolio. Mimi nimeshika hilo hilo, kwamba mimi ni Guido Gorogolio Sigonda, Mbunge wa Jimbo la Songwe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, si vibaya nikaeleza jinsi nilivyopata huu Ubunge, kwa ufupi kabisa. Baada ya kura za maoni na kupita katika kura hizo, chama changu kilinipendekeza ili kusudi nigombee Jimbo hilo pamoja na wenzangu wa upande wa upinzani. Lakini wenzangu, ndugu zangu wa upande wa upinzani walifika mahali wakaona kwamba kuna haja gani ya kumweka mtu kwenda kumpinga huyu ndugu yetu! Kwa hiyo, waliamua nao kukubaliana na uamuzi wa CCM kwamba sisi wapinzani hatuna mtu wa kumpinga huyu Sigonda. Tunakubaliana na hilo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilipita bila kupingwa. Kati ya wale watu wanne waliotangazwa mapema kabisa mimi nilikuwa ni mmojawapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana Mheshimiwa Naibu Spika, alitoa rai kidogo kwamba Waheshimiwa Wabunge wageni wanaelekea kwamba wanazungumza sana, ni kweli. Mimi najua kwamba alikuwa ana maana ya kutwambia kwamba tupunguze kuzungumza sana. Lakini naomba nieleze kwamba mimi nafikiri nitavunja rekodi kwa kuzungumzia kidogo sana kwa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia naomba nitoe pongezi kwa viongozi wote ambao walichaguliwa, kuteuliwa katika Bunge letu hili. Nawapongezeni sana ndugu zangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, kama nilivyoahidi kwamba nitazungumza kwa uchache sana, naomba niende moja kwa moja katika hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii inagusa maeneo 27 ikianzia na pongezi, shukrani na hatimaye hitimisho. Kwa sababu hii hotuba kwa hali ya kawaida ilikuwa ni kwenda kutekeleza, ni *working paper* ambayo inatuagiza kwenda kutekeleza.

Kwa hiyo, naomba niende katika lile eneo la mwisho kabisa la hitimisho na ninaomba ninukuu katika ukurasa wa 62. Baada ya kuzungumzia katika maeneo mengine yote, Mheshimiwa Rais amesema kwamba: "Lengo letu kuu ni kusukuma ukuaji wa uchumi kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya ili kuwa na maisha bora kwa kila Mtanzania." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba, kutakuwa na watu ambao ni watekelezaji na bahati nzuri tarehe 30 Desemba, 2005 hiyo hiyo Mheshimiwa Rais alituahidi kwamba ataunda Serikali ambayo itakuwa imara. *(Makofi)*

Naomba vile vile kwa kauli yake ninukuu sehemu aliyoizungumzia, ni ukurasa huo huo wa 62, anasema: "Nitaunda Serikali itakayodumisha umoja, amani na utulivu.

Aidha, nitajitahidi kutoa uongozi wenye ufanisi na uadilifu mkubwa, Serikali itakayowaongoza na kuwawezesha Watanzania."

Naomba nikiri kabisa kwamba Rais, alikuwa makini kabisa katika kuwateua Mawaziri. Nina imani kabisa kwamba Mawaziri, ambao wameteuliwa watatekeleza ipasavyo hili agizo na tayari tumekwishaanza kuona matunda yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa tatizo ambalo mimi naliona hapa ni kwamba kwa uzoefu ambao tumekuwa nao utekelezaji mkubwa kabisa huwa unatekelezwa kwenye Mikoa, kwenye Wilaya, lakini Vijijini matatizo ndiko ambako yako. Mimi naelewa kabisa kwamba lengo la hii hotuba ilikuwa ni kuboresha maisha ya wananchi walioko Vijijini. Sasa watekelezaji kule pamoja na kwamba Mawaziri ndiyo viongozi wetu wakuu, Wabunge ndiyo kiungo kikubwa kati ya Mawaziri na wananchi wanaoishi Vijijini.

Sasa hali ilivyo hivi sasa huko vijijini ni ngumu sana. Hasa zaidi kwa wale watekelezaji ambao wako chini ya Serikali. Bahati nzuri Serikali imeweka watumishi kule vijijini kwenye Kata, kwenye Vijiji pamoja ni watendaji, Madiwani, Madiwani ndiyo watu ambao wanatusaidia sana. Lakini hali za Madiwani zinasikitisha sana. Diwani ambaye tunamtegemea kwamba ndiyo kiungo kati ya Mbunge ambaye ndiyo kiungo kati ya Serikali na wananchi anakuja kupewa shilingi 30,000 kwa mwezi inasikitisha sana. *(Makofi)*

Mimi nilikuwa naona kwamba pengine umefika wakati Serikali ifikirie hilo jambo. Hawa ndiyo watendaji wakuu kule, ndio wasimamizi wakuu huko. Halafu vile vile katika ngazi mbalimbali za Serikali naomba ifikirie vile vile wale Watumishi ambao ndiyo wanaotusaidia sisi kusimamia maendeleo ya nchi kule Vijijini. Kuna *extension officers,* kuna Maafisa Uvuvi, kuna Maafisa Misitu, lakini utakuja kuona kwamba Afisa Misitu au Uvuvi anawekwa mahali kana kwamba ametelekezwa kule Vijijini.

Mheshimiwa Spika, hakuna kumbukumbu yoyote ukimuuliza umekuja lini anasema nina miaka 20 hapa. Lakini huyo Afisa ukianza kumuuliza sasa kazi gani ambayo unafanya, hajawahi hata siku moja katika mwezi mzima kutembelea Vijiji vya karibu kwa sababu ya matatizo aliyokuwa nayo ya usafiri hata vile vile ya mafungu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri kwamba wakati umefika kwa sababu tunataka kwenda na ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya, basi Wizara zinazohusika na ambazo zina maafisa kule naomba kabisa zifikirie kuwaboresha hawa maafisa. Motisha ni kitu ambacho ni kidogo sana lakini kina nguvu sana katika utendaji. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hawa wafikiriwe, kuna wengine wamekaa kule miaka zaidi ya 20 bila hata ya kupandishwa cheo, bila kupata nyongeza ya mishahara.

Sasa watu kama hawa usitegemee kama kweli wanaweza wakasaidia kusimamia maendeleo. Nilikuwa nafikiri kwamba pengine wakati ni mzuri sasa Wizara zinazohusika ambazo zina watu vijijini wafikirie kuwapa motisha itakayowasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliahidi kuzungumza kwa ufupi na nitajitahidi nizungumze chini ya dakika kumi. Upande wa siasa tumezungumza sana, ndugu zangu Wabunge wamezungumza kuhusu hali halisi ilivyo upande wa wenzetu Zanzibar. Lakini mimi ninachosema ni kwamba sisi tuna utamaduni hasa ndani ya chama. Tuna utamaduni kwamba baada ya uchaguzi, basi tunakaa kama kulikuwa na tatizo lolote basi tunakaa pamoja tunazungumza ili kusudi kulitatua tatizo hilo, ndiyo utamaduni ambao tunao. Kwa hiyo, nilikuwa nawaomba wenzangu ndugu zetu wa Zanzibar kama walivyoahidi wao wenyewe kwamba tukae chini tuzungumze, lazima tutapata muafaka hakuna lisilowezekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna hili tatizo ambalo sasa ndiyo linazungumzwa kwa nguvu zaidi la ujambazi, bahati nzuri mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama sitalizungumzia hili kwa sababu tuna mikakati jinsi gani tunaweza tukalishughulikia. Kwa hiyo, nawahakikishieni kabisa kwamba hali ya ujambazi itafikia mahali iwe ni historia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika eneo la utalii, Wilaya ya Chunya ina maeneo ya vivutio vingi sana, naomba Mheshimiwa Waziri, anayehusika ajaribu kuangalia Wilaya ya Chunya. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SAMEER I. LOTTO:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na ndugu Wabunge wenzangu, kwanza nashukuru kuendelea kupewa nafasi mara kwa mara na naomba msinichoke. Wenzangu wengi wamechukua nafasi hii kupongeza na kushukuru waliowapa kura, kupongeza viongozi wa juu. Mimi nitaongelea kwamba na mimi vile vile nimeshapongeza. Lakini napongeza tena wale wote wanaostahili kupongezwa. Lakini sitawashukuru kamwe wana vijiji wana kata, wana jimbo langu hapa, sioni kama ni sahihi kuwashukuru kwa kupitia vyombo vya habari. Nimeshakwenda na bado kwingine ambako sijafika nitaendelea kwenda kuwashukuru ana kwa ana pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaongelea mambo kadhaa katika hotuba ya Rais, kwa ufupi, nitaanzia na kilimo. Nitazungumzia kwangu zaidi kwa sababu sijui kwingineko. Lakini viongozi wa Kiserikali na kichama na baadhi ya Mashirika yamekuwa na tabia ya kuhodhi maeneo kwa kutaka kuendeleza mashamba lakini hawafanyi hivyo wanayachukua maeneo yale, wanayachukulia mikopo Benki na wanayatekelekeza. Sehemu nyingi sana tunayo matatizo hayo. Wananchi wanashindwa kwenda kulima kwa sababu maeneo yale yamepatiwa mpaka *title* kwamba watu wanayamiliki. Sasa Serikali nafikiri imefika wakati tuangalie maeneo ambayo hayaendelezwi tuweke labda muda miaka miwili, mitatu, mitano hawayaendelezi yarudishwe kwa wananchi. *(Makofi)*

Pia kuhusu matrekta mwenzangu hapa nyuma aliongelea hili ni agizo kwamba matrekta ya Dar es Salaam yarudi sasa mashambani, yako mengi yanazoa takataka, yanaleta misururu ya magari pale kwa sababu yanakwenda kwa mwendo wa pole, wanakuwa hawalipii kodi kwa sababu yanatakiwa yatumike kwa ajili ya kilimo, lakini yapo Dar es Salaam yanazoa takataka. Yarudi sasa yaingie katika maeneo ambayo yanatakiwa matrekta hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la ufugaji. Bahati mbaya Waziri Mkuu hapa hayupo, ufugaji hili ni tatizo sugu, ni tatizo ambalo wengi tunaogopa kuli-*address,* mimi huwa sipendi kuongea kiingereza, suala la ufugaji kwa kweli ni nyeti, tuna wafugaji, ni wapiga kura wetu, tuna wakulima, migongano kwangu pia iko mingi. Mimi sitapenda kutaja jina lakini atoke kiongozi wa Kitaifa anayeongea lugha yao aende huko aongee nao waelewe kwamba Serikali ina maamuzi gani juu ya kupunguza mifugo na kwa nini tunapunguza mifugo hiyo. Mimi naamini kabisa kwamba sisi wengine tukienda kuongea nao hatutaelewana Kiswahili chetu. Kwa hiyo, ningeomba kiongozi wa Kitaifa wa ngazi ya juu sitataka kutaja jina. Kwa sababu wao kufuga mifugo mingi ni kitu cha *status,* kiasi kwamba ukimwambia apunguze anaona kwamba kama unataka kumharibia heshima yake katika jamii. Ni vigumu sana hili kuwafahamisha jamani, tunakwenda kule unamsalimia mtu unamsalimia na ng'ombe pia ndiyo wanakuelewa. Yapo hayo, kwangu yapo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mazingira, tunajenga shule, tumeshajenga na tunaendelea kujenga shule za msingi, sekondari, vyuo zinataka samani kama, meza, viti, milango, makabati, hivi vyote vinahitaji mbao. Mbao tunazotumia ni *hard wood* hatutaki *soft wood. Hard wood* hivi sasa hivi zimeanza kuadimika. Mimi ningependekeza kwamba tutafute njia mbadala.

Mheshimiwa Spika, hivi viwanda vya *plastic* vitumie *plastic* ambazo zinazagaa, tuzipe masharti kwamba zikusanye hizi takataka zilizotumika, kutengeneza madawati ya *plastic*. Naamini inawezekana, tutakuwa tumepunguza kwanza takataka nyingi za *plastic* zilizozagaa lakini pia tutakuwa tumehifadhi mazingira na kutunza miti yetu katika suala hili. *(Makofi)*

Katika masuala ya mazingira hivyo hivyo alikuwa ni Waziri wa Maji alikuwa ameongelea kwamba maji mengi sana ambayo yanatiririka kutoka milimani yanaishia baharini au katika Maziwa Makuu. Mimi ningependa katika hili vile vile tujaribu kuangalia. Kwangu kuna mito mingi ambayo kwa kweli yote inatiririka ikienda baharini. Tuweke vikwazo au vizingiti au tujenge *embarkment* fulani za kuweza kuzuia maji yasiwe yanatiririka moja kwa moja kwenda kwenye mito hiyo. Katika sehemu fulani tuweke kizuizi kidogo ili maji yakifika pale yawe yanazuiliwa, kiasi fulani hatimaye kila mwaka tuzidishe vile vizuizi vipande juu tuwe tunapata mabwawa madogo madogo katika mito yetu kuliko maji yetu kutiririkia baharini. Maji yale tunaweza kuyatumia katika kilimo cha umwagiliaji na matumizi ya binadamu pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilizungumza Dar es Salaam kwamba tunatumia fedha nyingi katika *Songas, IPTL,* makaa ya mawe, lakini nikasema kwamba tukitumia fedha hizi tulizonazo kidogo fulani zikapelekwa kama ruzuku kwa wanavijiji ambao maji yanayotoka ili wapande miti, miti ile tukawa tunachangiana sisi basi tutakuwa tunapeleka fedha ndogo sana, tutatumia gharama ndogo wananchi watafaidika tutakuwa tumehifadhi mazingira na tutakuwa tumepunguza hili tatizo la upungufu wa maji katika kuendesha mitambo yetu ya umeme.

Lakini pia ningependekeza kwamba kuna kitu nasikia sasa kinaitwa *windmill* kina-*produce* umeme kwa kutumia upepo hebu tufanye utafiti huko pia. Naamini ile ni *safe* kabisa kwa mazingira kuliko hii ya *Songas,* ya *IPTL* au makaa ya mawe.

Katika masuala ya elimu nahoji michepuo kila mara kubadilika. Michepuo inabadilika kila Waziri anapokuja analeta ya kwake. Sasa hii inasononesha kidogo na inakatisha tamaa wakati wa maandalizi ya shule zetu. Shule tulipendekeza na bado mimi napendekeza kwamba ziwe na michupuo kwa sababu michepuo inamwandaa mwanafunzi anapomaliza angalau hata kidatu cha nne, aweze kuendeleza maisha yake kutokana na michepuo ile ambao iliyomwelekeza katika shule husika. Vijijini michupuo ya kilimo ingepewa kipaumbele. Mjini wataongea wenyewe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, katika elimu vile vile nimesikia hili sina hakika nalo kwamba walipa kodi wanaweza wakapunguza asilimia fulani ya kodi zao wakachangia katika elimu na halafu wakaonyesha risiti kwamba wamelipia michango elimu basi huwa wanapunguziwa katika kodi *indirectly* inakuwa kodi lakini imekuwa imechangia moja kwa moja katika elimu. Sasa hili sina hakika kama lipo mpaka sasa hivi, pale awali mimi nimeshawahi kulisikia lakini kama lipo basi hili liendelezwe.

Mheshimiwa Spika, kama lipo hawa walipa kodi wakubwa hasa wa Dar es Salaam mimi nawawahi huko jamani nakuja mimi huko kwa ajili ya hilo. Nitaongea nao kwa Kihindi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumzia uhusiano wa walimu na wanakijiji husika katika maeneo ya Vijijini. Serikali nafikiri ilisisitiza kwamba walimu wasiwe wanapewa nafasi ya kuwashirikisha wanafunzi katika kuchangia mambo fulani fulani katika shule au katika nyumba za walimu, mimi naona kwamba tujenge uhusiano mwema, wazazi wa vijijini wawakubali walimu, kama wale walimu ndiyo wanaoweza kuwasaidia watoto wao na walimu wawakubali.

Mheshimiwa Spika, tujenge ushirikiano tu-*harmonize* vitu hivi. Akienda kulima akamletea mwalimu mhogo kilo mbili, mzazi akimwachia mwalimu pale wamekwenda kuchota maji wakamwachia ndoo moja ya maji vile vinamfanya ahisi kwamba hawa wananitaka na yeye ajenge moyo wa kushirikiana nao. Hicho kitu pia naomba kiangaliwe.

Mheshimiwa Spika, katika masuala ya afya nilisikia pia hapo awali wakati wanajenga *Panama Canal* kule Marekani watu walikufa kwa sababu ya *malaria.* Wakaenda katika awamu ya pili wakatafuta mbinu, wakadhibiti kabisa *malaria* katika eneo lile walimwagia dawa fulani nafikiri ilikuwa *DDT* au nini lakini malaria iliisha eneo lile na mpaka sasa hakuna malaria pale. Mara moja ilifanyika na ikaisha. Sasa sisi hapa kwa nini tusitafute mbinu kama hiyo ya kuweza kumaliza malaria moja?

Kila siku tunaendelea kutafuta mbinu ndogo ndogo za kusema kwamba tunafanya hiki na kile lakini malaria yenyewe hatujaitafutia ufumbuzi wa kudumu. Leo tunatafuta

vyandarua, leo tunatafuta dawa hii, kesho tunatafuta dawa ile, lakini kwa kweli tukikusudia basi tunaweza kuimaliza malaria. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, katika suala la mikataba, tunaambiwa kwamba kuna mikataba ambayo ina masharti ya kuridhiwa na Bunge lakini kuna mikataba haina haja ya kuridhiwa na Wabunge. Kuna tofauti gani kati ya mikataba hii?

Kama walivyoongea wenzangu kwamba kongamano, semina, warsha zimeshafanyika nyingi haziwafikii walengwa zinaishia Mijini. Kwa hiyo, sasa hivi mambo yaelekezwe vijijini kwa walengwa wenyewe husika kabisa.

Mheshimiwa Spika, Wizara husika zifanye *reshuffling* Katani na Vijijini kama alivyofanya Rais, ili watu wasiwe wanang'ang'ania na kuzoea maeneo wanamokaaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu kuhusu suala la UKIMWI, naomba nizungumzie kwamba ile hadithi ya kwamba tuna milango saba hapa, fungua sita ule mmoja usifungue, anayeambiwa ule usifungue ndiyo mtu anakwenda kuufungua. Watoto wa shule za msingi waambiwa kwamba haya yote unaweza kufanya hili epukana nalo. Wanakwenda kule kule. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia naomba kwamba Tanzania tumefanya tafiti nyingi, tuna makabrasha mengi hapa kwenye maktaba zetu, kwenye vyuo vyetu tumeshafanya tafiti za kutosha katika kila fani. Sasa hivi ni wakati wa kuzitafuta zile tafiti na kuanza kuzifanyia kazi. Sasa hivi siyo wakati wa kwenda kuendelea kufanya tafiti. Kama haijafanyiwa basi ni suala lingine. Lakini nyingi zimeshafanyiwa tafiti katika fani mbalimbali tumeshapitia na tumeshafanya tafiti nyingi. Kabrasha zipo, vipeperushi vipo, maelezo yapo, mengine kwenye kompyuta naomba tutumie yale ambayo tayari yapo katika kuendeleza kwenda mbele.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache nashukuru sana kupewa nafasi na naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MWANAWETU SAID ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii kwa mara ya kwanza kuzungumza katika Bunge lako Tukufu. Pia napenda kuwapongeza viongozi wote ambao wamechaguliwa kwa awamu hii ili kuliongoza Taifa letu hili la Tanzania. Zaidi ya hapo ningependa pia kutoa hongera na kuipongeza hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kweli yeye ametuweka mahali pazuri katika Tanzania kwamba yeye ni mpenda maendeleo na ni mpenda haki. Kitu ninachotaka kuzungumzia wale waliosema kwamba huyu kweli ni *progressive president* nina hakika kabisa kwa sababu hakuna Rais yeyote ambaye ameweza kupambanua hali halisi ya Tanzania kwa kuelezea sekta zote zilizotajwa hapa. Isipokuwa mimi nataka kusema kwamba pamoja na maelezo hayo na hotuba yake sisi ndiyo tutakaofanya hizo shughuli kwa hiyo, tumuunge mkono tumsaidie kwa njia zote ili aweze kufanikisha yale ambayo ameyakusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ninalotaka kuzungumzia nitazungumzia kuhusu wanawake, mimi ni mwanamke na nitaanza na hilo. Yapo mengi lakini kwa sababu wengi wameshazungumza mimi nitazungumza machache. Ninachozungumzia kuhusu wanawake kwamba sisi wanawake ndio tunaoongoza hii jamii. Kama tunaongoza hii jamii tunakumbana na vikwazo vingi katika maisha.

Kwanza, tukiangalia watoto sisi ndiyo tunaoangalia na jamii nzima. Kwa hiyo, tunapambana na maradhi tusiyoyakusudia mfano UKIMWI, kwa sababu mwanamke hawezi kumwona mtoto wake pale anakufa kwa njaa wakati wewe unajua kabisa kuna mtu pale amekupa *appointment* atakupatia chochote. Kwa hiyo, watu wengine hawafanyi hivi vitu kwa kukusudia. Sasa basi huo ni mfano mdogo, mifano mingi imeshaelezwa hapa na wanawake wenzangu na hata akina baba wametusaidia. *(Makofi)*

Mimi ninachoomba kwamba mifuko mingi ya misaada kwa wanawake inayotolewa mara nyingi inaishia Miji Mikuu ya wajanja kama Dar es Saalam, Arusha inarudi Dar es Salaam, Iringa inarudi Dar es Salaam. Mimi ninachoomba hii mifuko hasa ile ya miradi ya Serikali ipelekwe pia katika Wilaya zetu na Mikoa yetu. Kitu cha kwanza ambacho nitatolea mfano Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote *(EOTF),* ambao wengi tumesikia kwenye redio (bomba) huu mfuko kwa kweli tulifikiria kwamba ni wa Tanzania nzima, lakini badala yake huu mfuko umekuwa wa sehemu chache au wa watu wachache kwa mfano huo tu ndio maana nasisitiza kwamba hii mikopo iwafikie wengine isiishie tu sehemu za watu wajanja watupu. Ifike hadi kwenye maeneo yetu vijijini na hata Wilayani hata kama hakuna Benki za kutosha kama ilivyo Dar es Salaam tuna *NMB* tu katika Wilaya nyingi.

Mheshimiwa Spika, halafu pia naomba kuuliza swali, kwamba je, Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote mara ya kwanza ulikuwa chini ya mke wa Mheshimiwa Rais Mstaafu, je, hivi sasa huu mfuko utakwenda mikononi mwa mke wa Mheshimiwa Rais wa sasa Bi. Salma Kikwete? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili nataka kuzungumzia mazingira. Mazingira ndiyo chanzo cha vitu vingi kama tukiharibu. Kwanza mvua tunaikosa kwa sababu ya kuharibu mazingira, huu umeme tunaolalamika tunaukosa kwa sababu ya kuharibu mazingira. Halafu vile vile ukame ambao unaleta njaa pia unaletwa kwa kuharibu mazingira. Sasa basi mimi nataka kuzungumzia kwamba hata katika eneo langu mazingira yanaharibiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuharibiwa kwake mazingira ni kwamba kuna hawa wanaochimba mawe *Gypsum* wako pale katika Wilaya yangu ya Kilwa sehemu inayoitwa Mandawa, pale wamechimba na wanatoka na mawe wakiwa wamepakia tani nyingi katika barabara yetu ya Kusini ambayo tumekuwa tukililia miaka mingi kwamba tutengenezewa barabara. Lakini kwa ukosefu wa mizani wao wanapitisha yale mawe kuyaleta Dar es Salaam na huenda wakasababisha uharibifu wa barabara.

Sasa nauliza swali moja, je, hayo mawe hayawezi kubaki yakachimbwa pale Kilwa ili wananchi wa Kilwa wapate ajira na kiwanda kijengwe pale Kilwa kwa ajili ya kutengenezea *cement* au vyovyote itakavyokuwa? Tungeomba kwamba yale mawe yabaki pale Kilwa na Kiwanda cha kutengenezea *cement* kiwepo pale Kilwa ili wananchi wetu na vijana wetu wa Kilwa pamoja na Kusini Lindi na Mtwara wapate ajira pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu lingine pia ninalotaka kuzungumzia ni kuhusu michezo, utamaduni, burudani. Kwa kweli Mheshimiwa Rais, amelizungumza kwa undani hili suala, kwa kweli ni ngumu sana michezo hapa Tanzania kuendelea. Kwanza, kwa sababu wale wanaoshughulikia michezo hawana fedha za kutosha za kutumia kwa ajili ya kuendeleza michezo. Idara zinazopewa ruzuku katika Halmashauri au Mikoa ni chache tu na zinaitwa Idara nyeti. Lakini Idara ya michezo, Utamaduni pamoja na hizi burudani, hizi zote zinaonekana siyo Idara nyeti.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, katika Halmashauri hakuna hata siku moja kwamba Idara hii inapewa ruzuku. Hali kadhalika katika kurugenzi zetu za michezo sijui labda ni mwaka jana pengine kurugenzi ya michezo imefikiriwa kwamba pale Mkugurenzi anahitaji kupata ruzuku kiasi gani. lakini kwa kawaida hakuna. Hizi Idara zimekuwa ombaomba kwenye maeneo mengi ni michango tu ili kuweza kuendeleza michezo. Hizi Idara ni muhimu kwa sababu hawa vijana tunaozungumzia wanapatikana katika maeneo haya. Wale wanapotoka kuzunguka mitaani ni kwa sababu maeneo haya, hakuna burudani ya kutosha, hakuna michezo, hakuna mambo ya utamaduni vijana hawa wanapotoka mitaani na kuzunguka ovyo na baadaye kuingia kwenye majanga ya kuvuta unga na kadhalika. Kwa hiyo, basi mimi naiomba Serikali ifikirie Idara zile za Halmashauri kuhusu michezo, utamaduni na burudani kuwapelekea ruzuku kama Idara zingine zinavyopelekewa na ionekane ni Idara nyeti kama zilivyo Idara nyingine pamoja na Wizarani kule kwa Mkurugenzi wa Michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ninalotaka kuzungumzia ni kuhusu amani na utulivu. Hili suala Mheshimiwa Rais amelizungumzia kwa uchungu sana, amezungumza kwamba si kwa sasa hivi ameliona, hili ameanza kuliona tangu akiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje, amekuwa akikumbana nalo suala la Zanzibar na Visiwa vya Pemba. Mara atokako swali ni hili hili. Na sisi Watanzania tumezoea kuwa na amani, tukitoka nje ya nchi mtu anapokuuliza wewe ni nani ukisema ni Mtanzania kwa kweli unapata sifa kubwa kwamba wewe nchi yako ina amani na kila mtu anaku-*admire*. *(Makofi)*

Sasa hivi suala hili linakuwa tofauti, tunaulizwa wewe ni Mtanzania tunataka kugeuka kama nchi fulani fulani ambazo siwezi kuzitaja ambazo kama mwanafunzi ukienda kusoma nje ukiingia *airport* unaulizwa maswali wewe ni wa chama gani, kabila gani. Sisi Watanzania tuna kawaida ya kukupokea kama Mtanzania, bila kuuliza ni kabila gani, ni chama gani. Lakini sasa kwa hali hii inaelekea sisi tutabadilika tuanze kuuliza ehee Mtanzania akaanza kuingia kama mwanafunzi Mtanzania, ameingia ehee, unatoka chama gani, wewe ni kabila gani, hii ndiyo hali halisi ambayo inataka kuwa hapa Tanzania. Kwa kweli hii hali n ngumu tunaomba iondoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amelizungumzia kwa uchungu hili suala kama tunavyolizungumzia sisi suala la UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba sana tuangalie kama tunavyopimwa ugonjwa wa UKIMWI mimi ni Mtanzania, kama ninaliona hili suala linalotokea Zanzibar ni la kawaida, basi naomba na mimi pia nikapimwe kama linaonekana ni la kawaida kwa sababu si kitu cha kawaida, mpakasuko kama huu mtu auseme kwamba tumeuzoea. Naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu hili tuliangalie kwa undani tuache ushabiki wa kivyama, vyama ni muhimu kwa kila mmoja, lakini maendeleo na haki ya binadamu ni muhimu kwa Tanzania nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kuzungumzia hali za wafanyakazi, kwa kweli hali za wafanyakazi katika Halmashauri zetu tuziangalie kwa undani. Sisi kama Waheshimiwa Wabunge ili tuweze kusaidiana na wale hatupaswi kuingia pale na kofia kwamba mimi ni Mheshimiwa Mbunge, kwa hiyo, unauliza maswali kwa ukali au kwa kulazimisha. Wale ni wataalam wetu katika Halmashauri kwa hiyo tuna haki zote za kuwaendea kwa kauli nzuri kama umeona jambo limeenda kinyume na kuwaulizia, nafikiri watufahamisha vizuri kuliko ukienda kwa hii kofia ambayo tumeibebe kwamba sisi ni Wabunge unaenda unaamrisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la wafanyakazi, naiomba Serikali kwa wale ambao wanadai *areas* zao hususan watu wa afya, naomba wao wafikiriwe kwa sababu wao wanafanyakazi ngumu, mfano milipuko ya kipindupindu imekuwa ikitokea mara kwa mara na matokeo yake watu hufanyakazi usiku na mchana na bila malipo yoyote wakiahidiwa watalipwa.

Mheshimiwa Spika, lakini hupita miaka na miaka mtu anadai lakini asipate hayo marupurupu, tuzingatie kwamba wao wanafanya katika mazingira magumu na hatimaye mara nyingine kupoteza maisha yao na kwa hiyo, wao pia wanahitaji *future* kwa familia zao. Ahsante naomba hilo lipewe kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo namaliza kwa kusema kwamba naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa asilimia mia moja na tutakuwa pamoja nae katika kumsaidia yale ambayo atahitaji kusaidiwa. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niwe mmojawapo ya wachangiaji katika hotuba ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuwapongeza na kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mbarali kwa kunipigia kura kwa asilimilia kubwa, asilimia isiyopungua sabini. Lakini vile vile niwapongeze kwa kumpigia kwa kura nyingi Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa asilimia 85, nawashukuru na kuwapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukupongeza wewe mwenyewe Spika kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana na Waheshimiwa Wabunge ndani ya Bunge hili wakiwa na imani na wewe na kwamba utafanya yale yote ambayo wanategemea uyafanye, nakupongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nafasi ya pekee niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wenzetu walioteuliwa kwa nafasi mbalimbali za Uwaziri, Unaibu Waziri na Ukuu wa Mkoa, ninaamini kabisa wanatuwakilisha sisi Wabunge katika kumsaidia Rais kuweza kutekeleza Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuwateuwa akina mama, ninaamini kwa *speed* hii tunayokwenda kipindi kijacho swali la kusema wanawake wangapi wamechaguliwa halitakuwepo, litakuwa linasema tu ni nani ambaye ameteuliwa bila kujali jinsia kwa maana tutakuwa sawa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naomba nianze kwa kuunga mkono kwa asilimia mia moja hotuba ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba hii ni nzuri sana imeonyesha mwelekeo kama vile mtu unaota unasema kwamba hiki kilichoandikwa ndani ya hotuba hii leo uamke kwamba kimetekelezwa, nafikiri ndoto za Watanzania zimekuwa mbali sana. Nampongeza sana kwa kiwango kikubwa ambacho ameweza kusema ndani ya hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii nzuri nafikiri mwelekeo mkubwa na matumaini makubwa ya yeye kufanikisha aliyoyasema kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwamba anategemea jitihada kubwa zianzie na sisi wananchi, tumsaidie sisi viongozi, tusaidie kila mtu kwa nafasi yake kuhakikisha yote yaliyoainishwa humu yanatekelezwa. Kwa hiyo, naomba tu nianze kusema kwa yale ambayo yamezungumzwa kwa sasa ambayo labda hayamo kabisa kwenye hotuba hasa kwa upande wa njaa.

Mheshimiwa Spika, tatizo la njaa linaonekana ni kubwa na hata pale ambapo Waziri Mkuu alitoa ile tathmini Waheshimiwa Wabunge wengi sana walionyesha masikitiko kwamba mbona mimi kwangu hakujaonyeshwa kama kuna njaa.

Mheshimiwa Spika, hali halisi inayojionyesha ni kwamba Tanzania nzima kuna njaa isipokuwa tunazidiana kwa kiwango. Kwa hiyo, jitihada kubwa ziongezwe kuhakikisha kwamba watu wanafikiwa na wanapata chakula na hawafi na njaa kama Rais alivyoahidi. Kwa sababu ilishajitokeza kipindi kilichopita mwaka uliopita kulikuwa na njaa baadhi ya maeneo na ugawaji wa chakula haukuwa mzuri sana, vyakula vilipelekwa vikafikishwa Halmashauri. Halmashauri hazikuwa na uwezo wa kufikisha kwa walengwa kwa sababu pesa zilikuwa zinafikishwa pale. Sasa naomba Mawaziri wenye dhamana hiyo ya kugawa chakula kuhakikisha kwamba ili kauli ya Mheshimiwa Rais isionekana kwamba ilikuwa ni ya kusema inatekelezwa na kweli watu hawafi na njaa, tathmini ifanywe kwa makini na ikizingatiwa kuwa taarifa zote ambazo zitatolewa na Wabunge na hata madiwani na hatimaye wazingatie ni jinsi gani chakula hiki kwa gharama yoyote ile

kinafikishwa kwa walengwa na watu hawawezi kufa na njaa tena, kwa hiyo hilo nilikuwa nasisitiza sana.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kuhusu elimu, taarifa ya elimu imetusikitisha sana, watoto wengi wamefaulu lakini hawakuweza kwenda sekondari na hasa mkoa wangu wa Mbeya ninaotoka kwa sababu na sisi tulisikitishwa Wabunge wa Mbeya kuona kwamba kwa kweli watoto 45,000 wamefaulu na 5,000 tu ndio wamekwenda sekondari hatujarudi majimboni, hatujarudi mkoani kukaa na vikao vya ushauri wa mkoa tukajua ni kwa nini kimetokea hiki. Lakini yawezekana tathmini ni kweli na tumeipokea kwa masikitiko makubwa na tuna mkakati mkubwa kabisa wa kuhakikisha kwamba yale majengo yote ambayo ni sekondari, wengi tumeanza kila kata kuwa na sekondari isipokuwa hayajakamilika, tukafanye kila nia ili kuweza kuyakamilisha.

Mheshimiwa Spika, lakini ninachokiomba kwa Waziri ambaye mwenye dhamana na elimu, ule mpango wa *MMES* zile pesa kama zipo kwa sababu wananchi sasa hawawezi kuchanga tena kukamilisha yale majengo, angekubali kupokea hiyo tathmini ili pesa zipelekwe mapema yakakamilishwe yale madarasa kusudi watoto waweze kuanza mapema. Hilo nilitaka nisisitize na niombe tena kwa sababu mpango wa kutoa pesa ni mgumu sana kwenda kukamilisha mlengo, mpaka ukamilishe kiwango fulani ndipo pesa zipelekwe. Sasa ili tuweze kutoa hii kero ambayo ipo kwa wanafunzi kubaki bila kusoma basi jitihada zionyeshwe kwamba hizi pesa pale pale ambako majengo yameanzishwa zipelekwe yakakamilishwe washirikianea na michango ya wananchi na Halmashauri zichangie kusudi watoto wengi waweze kwenda Sekondari.

Mheshimiwa Spika, mimi nimeguswa sana katika hotuba ya Rais kwa upande kilimo, kilimo kinachangia kwa asilimia zaidi ya 80 katika Pato la Taifa, lakini pili ni ajira kubwa sana kama alivyosema Mheshimiwa Rais kwa wananchi, kwa mtu mmoja mmoja na yeye amekusudia awamu hii kwamba atahakikisha kipato cha kila mtanzania sasa kinaongezeka, tunaposema pato la Taifa maana yake ni kwa ujumla wake lakini tumekuwa hatuangalii pesa inayoingia mfukoni kwa mwananchi, maisha ya mwananchi mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kuhakikisha kwamba kipato cha mwananchi mmoja mmoja kinaboreka ni lazima tuhakikishe kwamba tunaboresha ile sekta ambayo inaingizia watu wengi zaidi kipato ambacho ndio kilimo. Sasa amesema kwamba ataboresha kilimo cha umwagiliaji, atahakikisha kwamba kilimo cha umwagiliaji kinaboreshwa. Lakini mara nyingine huwa napata taabu, tumekuwa tukilisema suala la kilimo Bajeti zilizopita kwa wale ambao tulikuwepo ilizungumzwa kwamba sasa Serikali itatoa ruzuku kwa mbolea, ilianza kwa mikoa minne hiyo mbolea ilivyotolewa jinsi ilivyofika na kugawanya tumeishia kununua mbolea kwa mfuko shilingi 30,000/= na hizi labda ni mbinu za wafanyabiashara.

Aidha, wanahodhi ile mbolea ambayo imepelekwa kwa ruzuku au inatolewa kwa watu ambao hawahusiki wanakaa mpaka pale ambapo mahitaji yanapanda ili kusudi mtu anunue kwa kiwango cha bei ya juu. Sasa naomba Waziri anayehusika mwenye dhamana kwa sasa kama hili jambo litaendelea au ruzuku itaendelea kutumika basi mkakati

uwekwe wa kuhakikisha kwamba inamfikia mlengwa na hakuna mtu anayekatisha hapa katikati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pili tulisema kwamba kila Wilaya ichague zao moja la biashara na zao moja la chakula ili liweze kufanyiwa mkakati wa kuliboresha kwenye kila wilaya. Lakini mambo hayo yaliishia nusu na hatujui yaliishia wapi, wananchi walikaa wanasubiri sijui kama kuna wilaya ambayo ilifanikiwa kufanya hilo zoezi na likafanikiwa. Lakini ulikuwa ni mkakati wa kuongeza kipato kwamba wale ambao wana zao moja la biashara lisimamiwe mpaka lihakikishe kwamba linapata soko na wananchi wanaongezwa kipato. Kama ni zao la chakula basi liboreshewe huduma zote kusudi watu waweze kupata chakula cha uhakika, lakini yaliishia kwenye vitabu.

Lakini vile vile kulikuwa na mpango wa kusema kwamba mbegu bora zizalishwe kusudi zipelekwe Wilayani na za muda mfupi kwenye Wilaya mbalimbali yote hayo yaliandikwa, siku ambayo Rais anatoa hotuba niliguswa nikasema yale yote ambayo tuliyaweka kule nyuma na kwa kweli tunataka kumsaidia Rais kwamba tuboreshe kilimo je, ya kule nyuma tutayafanya nini? Na hasa kwenye kilimo cha umwagiliaji. Kwa mfano tu kwangu nina *scheme* za umwagiliaji zisizopungua 14 kubwa kabisa ni kama sita moja ambayo imegharimu zaidi ya bilioni 24 imetengenezwa na imeweza kuzalisha mazao kwa muda mwingi na wananchi wameweza kupata kipato lakini ule usimamizi wa kila mwaka wanasema ku-*maintain* hii miradi, samahani kwa kutumia hii lugha. Kuihakikisha kwamba inadumua na inaendelezwa tumekuwa tukisahau ukishakamilishwa mradi unaachwa unaachiwa wananchi utaalamu haufikia kule na zile *scheme* ambazo zimeanza tu kufanya kazi kufuatilia mpaka mwisho tuone matunda yake ni nini imekuwa ni tatizo. Lakini hapa leo Rais anatuambia kwamba atahakikisha kwa nguvu zote kuhakikisha kwamba kilimo cha umwagiliaji kinaboreshwa, sasa ningependekeza au ningeshauri kwamba zile *scheme* ambazo ziko sasa iwe ni wakati muafaka wa kuhakikisha kwamba zinafufuliwa na zinafanya kazi.

Pia tuchague tu maeneo ambayo ni muhimu kwamba hawa wanazalisha labda kama Mbarali wanazalisha mpunga na wana *scheme* nyingi za umwagiliaji basi nguvu zipelekwe huko ili tuweze kuhakikisha kuona kwamba kweli hii miradi na inaleta manufaa kwa wananchi wote wa Tanzania kwa sababu tukizalisha huko tutagawana chakula kwa Tanzania nzima na uvunaji wa maji tulizungumzia hapa kwa ajili ya umwagiliaji hasa kwenye mito ya muda mfupi. Kazungumza Mheshimiwa mmoja kuchimba mabwawa makubwa ambayo yatakinga maji wakati wa mvua na yatakaa wakati wote ambapo mvu imepungua tutayatumia kumwagilia na kilimo cha umwagiliaji kwa kweli kitaboreshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ningeomba hili kwa kweli liangaliwe kwa Waziri mwenye dhamana hii ya Kilimo na Chakula kuhakikisha kwamba haya yaliyozungumzwa na Mheshimiwa Rais na sisi tutakuwa nyuma yake kumsaidia na kuwashawishi na kuwahamasisha wananchi kuungana naye kwamba yanafikiwa muafaka na kuona kwamba kweli kilimo sasa kinachangia kwa asilimia 80 na mwananchi anaboresha kipato chake cha mtu mmoja, mmoja *and individual income* iwe kubwa kuliko ile ya kusema pato la Taifa lakini mtu ukimkuta maisha anayoishi kila siku ni ya

kusikitisha na hasa sisi tunaotoka vijijini kunasikitisha na Mbunge huwezi ukakaa kweli unaletewa malalamiko unaona haya malalamiko kwa kweli ni sahihi.

Mheshimimiwa Spika, hili nilipenda kusisitiza sana, lakini lingine ni kwa upande wa utunzaji wa mazingira. Mazingira hasa kwenye sehemu ya vyanzo vya maji tunapata matatizo ya umeme sasa mimi wilaya yangu ina sehemu ambayo ni chanzo cha Mto Ruaha ukisikia Bonde la Usangu sehemu za Ihefu na ni sehemu ambayo ilikuwa ni nzuri sana hata kwa utalii yenye chepechepe nzuri, ilikuwa na maji ya muda mrefu yanatoka kila mwaka. Lakini unaposema Ruaha imepungua mimi kama mwakilishi wa wananchi wa Mbarali naguswa sana na hilo lakini yale mazingira yameharibiwa sana ufugaji. Wafugaji wamehama mikoa yote ya Shinyanga, Mwanza, Dodoma wamehamia kule Mbarali. Lakini walipohamia kule kwa lengo moja, wasukuma wanasema kuna mmoja alihamia kule alisema ukilisha kule mifugo maana ng'ombe wanazaliana sana. Kwa hiyo, wakapeana taarifa watu wakaja kule, sasa wakileta ng'ombe haleti watano wala 10 analeta ng'ombe 600, ng'ombe 1,000, ng'ombe 2,000. Lakini kwa mila zao sijui kama zipo hataki kuona mnyama haonekana ng'ombe wake anataka mita 100 awaone wanakuja na ili awaone lazima akate miti. *(Makofi)*

Kwa hiyo, popote msukuma anapofuga ng'ombe maana yake miti unakuta imekatwa na kuna tambarare hakuna mti hata mmoja. Kwa hiyo, sasa kutokana na ukame wa bonde la Usangu maana yake sehemu yenye maji pekee ni ile ya Ihefu wakati wa kiangazi wanahamia kule kwenda kupeleka mifugo, sasa ule uchepechepe wote umekwisha imekuwa ni ukame, ni vumbi na wanang'ang'ania kwenda kule. Lakini nimekuwa nikilisemea hili Serikali ikawa inasema kwamba halmashauri, wananchi na wafugaji mshirikiane kutenga maeneo kitu ambacho hakiwezekani, ng'ombe lakini sita, laki saba katika wilaya moja halmashauri haiwezi kupata pesa za kutenga maeneo.

Kwa hiyo, nilikuwa nagusa kwamba kama kweli tunamkakati mzuri, basi tungeangalia maeneo ambayo yana wafugaji kama pale Mbarali kwamba tushirikiane wote tuone ni jinsi gani tutawasaidia hawa wafugaji, ni jinsi gani tutahakikisha kwamba tunatenga maeneo kwa ajili ya wakulima tu na wafugaji na kile chanzo cha maji kiweze kutunzwa ili kusudi tuweze kupata maji kwa ajili ya kuzalisha umeme. Kwa kweli hali ya mazingira kule imeharibika na kila siku nilikuwa naomba kwamba ile ingefanywa hata kama sehemu ya utalii kwa sababu ni *game reserve* vile vile, kwamba ingekuwa ni ya utalii, ni hifadhi ya wanyama pori ingesaidia vile vile kutunza chanzo cha maji. Lakini kama alivyosema mwenzangu kwamba ukimwambia msukuma punguza ng'ombe lakini vile vile ni mpiga kura wangu atakuambia unatumbia sisi tuhame twende wapi? Lakini mimi naiomba Serikali na ni kilio ambacho nakitoa kwamba hili kwa kweli tuboreshe na kuhakikisha kwamba chanzo cha maji kinalindwa na Serikali Kuu na halmashauri na sisi tutakuwa tayari tusaidiane kuona kwamba tunawasaidiaje wafugaji, tunaboreshaje kile chanzo cha maji kusudi tusiweze kupata tena matatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo ninaomba nilizungumze kwa msisitizo na wale wenye dhamana hiyo wanisaidie kuhakikisha kwamba lile tatizo linaondoka. Lakini lingine ni kwa upande wa maslahi ya watumishi, Mheshimiwa Rais amezungumzia sana hili kwa kweli ni la muhimu miaka ya huko nyuma tulikuwa tunasema kwamba kuna

watumishi walikuwa wanasema kuna *rare professional* kuna *professional* za kati wale ambao ni wa muhimu sana kama ukichukua madaktari ukiwachukua wahasibu, ukachukua wahandisi mbalimbali walikuwa wanapangiwa viwango vyao vya mishahara. Ili kuwa-*maintain* wabaki ndani ya Serikali, lakini sasa tunapozungumzia hata wahasibu wanamaliza Chuo hawaendi Serikalini , wahasibu ni wachache kwa sababu tunapokagua hesabu huku unakuta wahasibu unaambiwa ni mtu wa *NAD,* mtu wa *NADOCE* lakini waliomaliza *CPA* wako wengi, akifika anapata mshahara ambao akienda kwenye kampuni binafsi atalipwa mara tano lakini hapa tunasema tunataka kudhibiti mapato na matumizi ya Serikali na hawa wasomi wetu hatuwezi kuwa-*maintain* ndani ya Serikali kwa sababu vipato havitoshelezi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nasema hilo alilozungumza Rais tulifanyie kazi kuanzia ngazi za juu mpaka chini na nikisema chini ni mpaka kwa maafisa watendaji wa vijiji ambayo imekuwa ni kero kubwa sana kwa Wabunge wengi, tangu mwaka jana tulisema tumeweka bajeti kwa ajili ya mishahara ya maafisa watendaji lakini waliolipwa ni asilimia 50. Sasa hivi hawajapata mishahara kwa mwaka mmoja sasa na wako kule na walishahamishwa kwenye sehemu zao za makazi wakaenda kwenye sehemu za kufanyia kazi tofauti familia zimebaki nyuma. Lakini kama tuko tunamuunga mkono Rais kwa kweli tuangalie maafisa watendaji wa vijiji ambao mpaka leo wameajiriwa na hawajapata mishahara na imekuwa kero kubwa sana kwa Halmashauri na hata sisi Wabunge haya maswali tunashindwa kuyajibu kwamba kama mlisema Bajeti tangu mwezi Julai, 2005 tungeanza kupata mishahara lakini mpaka leo hatujaanza kupata mishahara ni lini sasa wataanza kupata mishahara?

Mheshimiwa Spika, kwa hilo ningeomba kwamba kwa kweli uboreshaji wa maslahi ni muhimu na ninamuunga mkono kabisa Mheshimiwa Rais kwa hili kwamba wale wafanyakazi kuanzia ngazi ya juu mpaka ya chini sasa tuhakikishe kwamba tunawatunza wanabaki ndani Serikali ili tusiwape ile kwamba mtu anaweza akapokea rushwa, anaweza akaiba, anaweza akafanya chochote kwa sababu atakuwa na uhakika na kipato chake cha kuisha kwa siku nzima na hata kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kwa upande wa michezo nimefurahia sana upande wa michezo Mheshimiwa Rais amesisitiza lakini kwa sababu Waziri mwenye dhamana ya michezo wapo, wasisitize ujenzi wa viwanja vya michezo. Naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. SAMUEL M. CHITALILO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua nafasi hii kukushukuru sana wewe kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia yangu machache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakupongeza sana kwa kuchaguliwa kwako wewe na Naibu Spika na tumwombe Mungu awape maisha marefu zaidi hapa duniani. Vile vile nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa na ninampongeza sana Waziri Mkuu kwa kuteuliwa na ninawapongeza Mawaziri wote na Manaibu kwa kuteuliwa kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mengi yameshazungumzwa lakini nami nitarejea kwa machache niliyonayo, jambo la kwanza ni janga la njaa kwa wastani nchi nzima imegubikwa na janga la njaa. Lakini naishukuru sana Serikali kwa hatua mbalimbali ilizoanza kuchukua kwa ajili ya kudhibiti hali hii, lakini kitu kingine cha kusikitisha ni kwamba kule Sengerema kuna maafisa wetu wa Wilaya wanakwenda wanagawa hizi mbegu za mtama kwamba watu wapande sasa, kweli mtu ana njaa unaenda kumpa mbegu atapanda na huku hana nguvu? Hili ndilo jambo linalonisikitisha, kwamba mtu ambaye ana njaa unampelekea mbegu leo hii akapande atalima vipi na huku ana njaa? hili ndio jambo ambalo najaribu kusema ni la kusikitisha.

Mheshimiwa Spika, pia nimeangalia katika taarifa ya chakula, Wilaya yangu ya Sengerema haimo kabisa, sasa sijui taarifa hizi zimekuja kwa usahihi, nitapenda baadaye wakati ana-*windup* Waziri mhusika anifafanulie labda kuna njia nyingine ambayo wametumia kwa ajili ya kupeleka kule chakula au namna gani, maana hata Buchosa na Sengerema nzima ina njaa kubwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nitazungumzia hapa ni elimu, kwenye hotuba ya Rais amezungumza kwamba sasa hivi ni vema kukawepo na shule ambazo ni za Serikali, za *High School* hata huko majimboni na sehemu mbalimbali kwa ajili ya wa watoto wetu, wadogo zetu waweze kufaidika na elimu. Lakini tatizo kubwa ni kwamba pamoja na kuongeza shule hizi tatizo kubwa hadi sasa hivi ni tatizo la walimu, upungufu wa walimu ni mkubwa sana hapa nchini si Buchosa peke yake na wala si Mwanza peke yake ni nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, ningependa Waziri mhusika ajaribu kufanya utafiti wa kutosha na kuuchukua kama dharula kwa ajili ya kupatikana walimu wa kutosha katika shule zote za msingi na shule za sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la tatu ni umeme vijijini, mimi nipo kule Buchosa umeme unakomea Sengerema Mjini na watu wengi wanatoka vijijini wanakwenda kukimbilia Dar es Salaam au Mwanza Mjini kwa sababu ya kufuata mwanga, maana yake uko gizani sasa wanaona kuna giza nene wanashindwa kuvumilia kukaa huko. Kwa hiyo, njia nzuri ya kudhibiti watu ili waendelee kukaa kwenye sehemu zao na kufanya shughuli zao za kuzalisha ni kuwapelekea umeme huko waliko vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili likifanyika hutaona watu wengi wanajisomba kwenda Dar es Salaam wala kwenda Mwanza Mjini kwa sababu kila kitu kiko kule kama Buchosa tuna Ziwa la kutosha, tuna ardhi nzuri. Kwa hiyo, watu wangeweza kubaki kule, tuna msitu mkubwa sana unaitwa Buhindi, watu wangeweza kubaki kule wanafanya shughuli zao. Hili ninaomba kwa sababu hata Waziri wa Nishati kilichopita wakati ule Mheshimiwa Daniel Yona, aliwahi kunijibu hapa Bungeni kwamba umeme Buchosa utapelekwa, utapelekwa kule Nyakalilo, Nyeunge hadi Kaunda akasema kwamba tatizo ni pesa zipatikane za Serikali na mimi najua kwa sababu mapato ni mazuri

tunayoyakusanya mimi ningeomba sasa jambo hili litekelezwe umeme ufikishwe katika sehemu hizo za Buchosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni barabara vijijini, kwanza napenda kuishukuru sana iliyokuwa Wizara ya Ujenzi wakati ule kwa sasa hivi Miundombinu na ninazidi kumshukuru sana aliyekuwa Waziri wakati ule Mheshimiwa John Pombe Magufuli, pamoja na Naibu wake, pamoja na timu yake ya wakati ule kwa kuhakikisha kwamba Buchosa inapitika na ni kweli inapitika.

Mheshimiwa Spika, na hivi ninavyozungumza hapa ni kwamba kuanzia mwezi huu wa pili bado barabara za Buchosa zitaendelea kutengenezwa na mkandarasi atakuwa barabarani wakati wowote kuanzia mwezi huu wa pili ili kuendelea kuziimarisha kwa kiwango cha changarawe, kwa hiyo, ninamshukuru sana kwa kipindi hicho. Vile vile naomba Wizara ya Miundombinu iendelee kusaidia kuhakikisha barabara za vijijini zinapitika kwa urahisi, tunavyo vijiji ambavyo hata wewe Mbunge unapoenda kufanya *campaign* au unaenda kutembelea wananchi wako unaona hata aibu kwa sababu gari utaliacha zaidi ya kilometa tatu utatembea kwa miguu ili kufika sehemu ya wananchi walipo na watakueleza tatizo la barabara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kabisa mpango kabambe ambao tumeshaambiwa hapa Bungeni wa kupeleka barabara vijijini uharakishwe haraka sana iwezekanavyo na huu mpago wa miundombinu uendane sambamba na vivuko, leo hapa asubuhi wakati Waziri anamjibu Mbunge mwenzangu wa Sengerema Mjini, Mheshimiwa William Ngeleja alipokuwa anamjibu kuhusu kivuko, nashukuru sana kwa kusema kwamba kivuko kipya umetamka kitaanza kazi haraka sana iwezekanavyo mwezi Septemba mwaka huu. Lakini tusisahau kwamba tunacho kivuko kingine, kivuko cha Nyakalilo kwenda Kone, kivuko hiki mimi nasema hata kura zangu kwenye kisiwa kile zilipungua kwa sababu ya kivuko hiki kibovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kimeshasababisha maafa ya watu sio chini ya watu karibu 100, kwa hiyo, ninaomba hii ichukuliwe dharula kama mwenyewe ulivyokuwa unaomba hapa kura ukasema kwamba ni *Speed and Standard* na dharula vile vile ulizungumza. Kwa hiyo, naomba jambo hili lichukuliwe kwa dharula iwezekanavyo kwa sababu kivuko hiki kinapokwenda katikati mara kinazimika tu hata katikati ya ziwa majira na watu wanashinda ziwani aidha wanakaa siku mbili, siku tatu, siku nne. Kwa hiyo, Mbunge ukienda kila siku ni kutukanwa kwa ajili ya kivuko hiki, ninaomba hili lichukuliwe *serious* kabisa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nitakalozungumzia hapa ni kuhusu ujambazi, ujambazi umekithiri moja kwa moja na ninashangaa ujambazi unapotokea Dar es Salaam kila mtu ndio anaanza kuzungumzia ujambazi upo. Mimi nilishazungumzia hapa Bungeni katika Bunge lililopita kwamba ujambazi Buchosa ni kwamba inapofika saa 12 jioni Bendera ya Serikali inapoteremshwa wale watu wanajichukulia madaraka mpaka asubuhi, watu hawalali kule wananyanyaswa, wanauawa Ziwani wananyang'anywa vifaa vyao vya kuvulia samaki. Sasa naomba kwa nini iwe tu kama sisi Wabunge kila siku unazungumza kitu halafu hakitekelezeki ninaomba sasa hii awamu ni hari mpya, kasi mpya na nguvu mpya vitu hivi vifanyiwe kazi haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa nikiwa Bungeni juzi tu katika visiwa vya Zilagula, Mchangani na Maisome walivamiwa siku nne tu zilizopita au siku tano. Wamevamiwa na kunyang'anywa zaidi ya *engine* 20 hizi za kuvuliwa na kila *engine* moja ina thamani ya shilingi milioni moja na laki saba, milioni 2, wavuvi hao na hao wavuvi ndio wanachangia sana pato la Mkoa wa Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe mwenyewe ulivalie njuga kabisa kuwaeleza Waheshimiwa wanaohusika. Jambo lingine na la mwisho nitakalozungumza mimi ni *brief* sitaki kuwa na maneno mengi. Jambo lingine ni la Muungano, Muungano wetu una amani takriban zaidi ya miaka 40 lakini leo tunataka kuwaona watu wanavuruga muungano na sisi bado tunaacha mwanya huu uendelee kutumika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuomba kura kwa Bunge lile la Afrika hapa niliona Mbunge mmoja wa *CUF* yeye alisimama wazi hapa na akaulizwa swali, unaitambua Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar akasema siitambui, leo hii tunaendelea kumlipa posho ya Serikali ya Muungano, tunatafuta nini? Sasa sisi Serikali hii tunapingana na Serikali ya Mapinduzi ambayo tunaitambua sisi kwamba ndio Serikali yetu? Kwa sababu kama tunaendelea kuwalipa hawa watu na wanasema hawaitambui Serikali ya Mapinduzi tunachofanya kina maana gani katika jamii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba jambo hili lisichukuliwe kama masihara, mtu anakuja kutamka hapa haitambui Serikali na bado analipwa mshahara na bado anachukua posho na bado anafanya vitu vyote. Naomba mambo kama haya yasiwepo na nitapenda kupata majibu yanayolingana na jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitakuwa na maneno mengi bali ninawashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Buchosa kwa kunirudisha mara ya pili katika Bunge lako Tukufu.

Kwanza nawashukuru sana wananchi wangu kwa sababu kwanza mnajua magazeti yaliyoandika Samuel Chitalilo chupuchupu, kweli chupuchupu wameninusuru nimerudi hapa Bungeni, nawashukuru sana. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mimi niungane na Wabunge wenzangu kumshukuru na kumpa pongezi Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi za kuliongoza Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Waziri Mkuu, ndugu yetu Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kuteuliwa kushika wadhifa wa Waziri Mkuu katika Serikali hii ya Awamu ya Nne, hongera sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakupongeza wewe kwa kuchaguliwa na Wabunge kuwa Spika wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tena kwa kura za imani. Nimpongeze Naibu Spika, kwa kuteuliwa kwake pamoja na Mawaziri wote. Niwapongeze Wabunge wenzangu kwa kuchaguliwa katika nafasi zao za uwakilishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipeleke shukrani zangu za dhati kabisa kwa wapiga kura wa Jimbo la Kisesa, kwa kunichagua mimi kwa kura nyingi kabisa za ushindi na hatimaye nikawa katika Bunge lako hili Tukufu. Ninawapongeza wananchi wa Jimbo la Kisesa kwa sababu wananchi hawa walikuwa hawajawahi kuchagua CCM tangu Jimbo lile lianze, lakini safari hii wameamua kuchagua CCM, ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sishangai yale anayofanya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa sababu nilijua kabisa tangu anaomba kuchaguliwa atafanya haya anayoyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda nianze na suala la chakula. Ni kweli kabisa kwamba Taifa letu limekabiliwa na tatizo kubwa la upungufu wa chakula, majira yamebadilika. Lakini labda basi nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa jitihada zake alizozichukua kuamua kwenda kuyatembelea maeneo na kujionea yeye mwenyewe ukubwa wa tatizo hili la upungufu wa chakula lilivyo.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru mpaka sasa hivi kwenye Wilaya yangu hususan kwenye Jimbo langu la Kisesa tayari nimeshaona kwenye *schedule* nimepangiwa chakula japokuwa siwezi kusema hapa nimepangiwa kiasi gani kwa sababu ukianza kutaja taja zinaanza kupunguzwa, lakini nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho sasa hivi ninaomba ni kwamba kama tulivyotangaziwa na Waziri wa Kilimo kwamba chakula hiki kitapelekwa kwa walengwa kijijini moja kwa moja na wala kisishushwe tena kwenye kata. Sasa hivi wananchi tunajua wamedhoofika kutokana na upungufu wa chakula sasa kusafiri kilomita 20 kufuata chakula bado tunawaongezea mzigo. Kwa hiyo chakula hiki sasa kama ilivyosemwa bajeti imetoka ya kukipeleka chakula hiki moja kwa moja kwa wananchi wetu vijijini kule waliko basi na iwe hivyo.

Mheshimiwa Spika, chakula hiki kinaposhushwa kwenye Kata tunasababisha hata huu wizi wa chakula unatokea lakini wakifikishiwa kule kule hata haya masuala ya kusema Mtendaji wa Kijiji kaiba chakula, sijui wa kijiji fulani wamefanyaje, hayatakuwepo.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichangie tena upande wa kilimo cha pamba. Kama kweli Watanzania tumeamua kuleta mapinduzi ya uchumi na maendeleo tena kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya basi ni lazima tufikirie wakulima hawa wa zao la pamba. Zao hili la pamba linashuka bei siku hadi siku na wakulima wetu wengi wameanza kukata tamaa hata kulilima zao la pamba. Gharama za kilimo unatumia shilingi 70,000 kwa ekari moja unavuma unauza unapata shilingi 80,000 miezi sita

umezalisha shilingi 10,000. Naomba sasa Serikali ifanye kila linalowezekana kuhakikisha kwamba zao hili la pamba linapatiwa ufumbuzi na kisha basi tupate soko la uhakika la zao hili la pamba.

Mheshimiwa Spika, siku ile Waziri anajibu swali la Mheshimiwa Richard Ndassa, alikubaliana na makato na ushuru mwingi ambao tunawarundikia wakulima hawa. Kuna ushuru wa aina tano, *Cotton Development Fund* mkulima anakatwa shilingi 20 kwa kilo kuendeleza zao la pamba lakini hatuoni zao hili linapanda bei, hatuoni zao hili linaongeza ubora halafu wao wanasema wana *develop* wana-*develop* nini katika zao hili la pamba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu kuna *Tanzania Cotton Lint and Seed Board* shilingi 5 inakatwa zinakuwa shilingi 25. Kuna *Council Cotton Levy* shilingi 15 ambayo ni 5% ya bei ya pamba. Kuna *contribution for Education Board* sjilingi 5 *per k*g. Kuna, pembejeo shilingi 15 kwa kilo. Sina matatizo na hii 5% inayokatwa kwenye Halmashauri zetu hizi kwa sababu ni changa hazina mapato baada ya kodi zingine kuondolewa ina maana ndio zimebakiza tu huu ushuru wa zao la pamba lakini hizi zinazokwenda kwenye Bodi ya Pamba ndizo nina matatizo nazo jumla ya shilingi 45.

Mheshimiwa Spika, mtu anakwambia kwamba ana mfuko wa kuendeleza zao la pamba la shilingi 25 lakini bado tena anakuja kukata pembejeo shilingi 15 na ile inayokatwa kwenye pembejeo, wakulima wetu hawaletewi pembejeo na anakatwa pembejeo kwa ajili ya msimu unaokuja yaani wewe unauza leo unakatwa pembejeo ya mwaka unaofuata. Pembejeo ya zao la pamba ni tofauti na pembejeo ya mahindi unaweza ku-*switch on* mwaka unaokuja usilime pamba lakini *already* wewe umeshakatwa pembejeo ya pamba. Kwa nini wakulima hawa wasiuze pamba yao na kulipwa pesa yao yote halafu wao wakajinunulia pembejeo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha zinazokatwa na Bodi ya Pamba, zirudishwe kwenye bei ya mkulima. Hili tulichukulie *serious* kwa sababu Sh.45 kwa wakulima ni fedha nyingi zitawasaidia wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siku ile Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, alikiri kabisa yeye mwenyewe kwamba ubora wa zao la pamba uko chini lakini wakati huo huo wana fedha hizo zote kuendeleza zao la pamba. Mimi kwenye Wilaya yangu tunazalisha tani 25,000 kwa mwaka. Ukifanya hesabu makato na ushuru ni jumla ya shilingi 1.125 bilioni Bodi ina kazi gani?

**MBUNGE FULANI:** Haina kazi.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, bodi iwajibike kuangalia ubora wa pamba kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, kwanza utakuta watu wa Bodi ya Pamba wame-*dominate* lile zao la pamba wanasimamia wao ubora wa pamba na wanasimamia ngazi ya kiwanda *(ginnery level)* lakini wakati pamba inalimwa, inavunwa, inauzwa kwenye chama cha

msingi hawaangalii wanaenda kuangalia ubora wa pamba kwenye *ginnery level.* Hata kule kwenye ngazi ya kiwanda hawaangalii ubora wa pamba isipokuwa wanataka kujiridhisha kwamba kiwanda kimepokea kilo kiasi gani ili wasije kupunjika kwenye yale malipo. Naomba Maafisa Kilimo wetu walioko kule kijijini wasimamie ubora wa zao la pamba na sio tena watu wa Bodi ya Pamba, hawa wanaweza kutuletea ubora wa zao hili la pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye mifugo, naomba Maafisa Mifugo wetu wasiwe maafisa wa ofisini wawe wanawatembelea wafugaji wetu wanawafundisha habari za ufugaji na kuwashauri inapobidi.

Mheshimiwa Spika, vile vile basi ziwepo rejista za mifugo kwenye vijiji vyetu. Wakati wa kodi tulikuwa na hizi rejista nzuri kabisa sasa hivi hazipo. Naomba hizi rejista za mifugo sasa hivi ziwepo kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za mifugo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa majosho na mabwawa, Serikali yetu imeshatamka na nguvu hizi zipelekwe basi Jimbo la Kisesa ambalo lina mifugo mingi sana lakini hakuna josho wala bwawa mpaka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la malisho, wakulima wetu wapewe semina tu za namna ya kutunza malisho, kuna mapua, nyasi huwa zinachomwa moto lakini zile nyasi wanaweza kuwa wanazikata, wanazihifadhi kwa ajili ya kulisha mifugo kwenye muda wa dharula au kipindi ambacho malisho ni machache. Wanaweza kununua mashudu na pumba zikawasaidia wakati wa dharura.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori, ningeomba sheria hii ipitiwe upya ili iruhusu wafugaji wetu kuchungia kwenye hifadhi ya wanyamapori pale dharula zinapojitokeza. Nimeona Wabunge wenzangu wengine walikuwa wanalalamika kwamba mifugo inayovamia maeneo yao inamaliza maji. Lakini mimi sioni tatizo kama mifugo ni ya Watanzania na wafugaji wale ni Watanzania sioni tatizo isipokuwa basi labda tufikirie tu ni namna gani tunategeneza chanzo cha maji kwa ajili ya mifugo hii. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na mjadala wa Waziri wa Hifadhi ya Wanyamapori na huyu wa Mifugo kwamba wakubaliane ili waruhusu mifugo yetu kwenda kuchunga kwenye hifadhi ya wanyamapori katika muda huu wa dharula. Nafurahia mjadala ule lakini sasa mjadala wenyewe unachelewa, ningeomba uwahishwe zaidi ili wananchi wetu waweze kwenda kuchungia kwenye hifadhi ya wanyamapori katika kipindi hiki cha dharura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, afya, katika Jimbo langu ninacho kituo kimoja tu cha afya na kituo kile hakiwezi kuongeza damu, mganga ni mmoja *(Clinical Officer)*. Kutoka kwenye Hospitali ya Wilaya mpaka kwenye kituo changu cha afya ni zaidi ya kilometa 60, akina mama wengi wanakufa, watoto wengi wanakufa kwa kuishiwa damu na kwa kukosa huduma za afya. Ninaomba Wizara ya Afya basi nikiondoka hapa Bungeni nipate kibali cha kwenda kuajiri Madaktari ili matatizo haya yaweza kutatuliwa.

Mheshimiwa Spika, hata hizi *ambulance* zinatakiwa ziwepo kwenye vituo vyetu vya afya kwa sababu ni sera ambayo imekuwepo muda mrefu lakini sasa naomba ianze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, daraja la Mto Simiwi, ningeomba kabisa lichukuliwe hatua kwa nguvu zote tukalijenge. Mheshimiwa Rais wakati anaomba kura aliwaambia wana Kisesa kwamba mkimpa kura Mpina nitawajengea daraja la mto Simiwi, Mpina yuko ndani ya Bunge naomba niende sasa na mpango mzima wa kujenga daraja la mto Simiwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu sina tatizo na majengo, lakini ninachokisema majengo sisi tutajenga na tutasaidia na Serikali kujenga lakini matatizo ya vitabu, vifaa vya maabara, Walimu ambayo yanawezekana kabisa kwenye Serikali yetu yatatuliwe basi. Mimi sioni sababu ya kwa nini vijana wetu wanakosa vitabu, sioni sababu ya kwa nini vijana wetu wanakosa vifaa vya maabara. Watoto wetu wanamaliza mpaka *form four* hawajui hata *Bunsen burner* hawajui, lakini ndio wataalam tunaowategemea waje wawe waganga na walimu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniteua kuwa mmoja wa Wabunge kuja kuliwakilisha Bunge la Tanzania hapa.

Pili, naomba nikishukuru Chama cha Mapinduzi, UWT, wananchi wa Kibaha Mjini, kwa kweli ingekosa wao kunipendekeza sasa hivi nisikuwepo hapa. Ninawakushukuru sana wananchi wa Kibaha kwa sababu wameonyesha rushwa kwao sio kitu cha kuwafanya wachague kiongozi. Nilipambana na watu waliokuwa wanagawa unga, maharagwe, *butter* na pesa. Walikula na wengine wakawaambia sainini kuwa wanaugua UKIMWI wakasaini lakini walinichagua mimi, naomba niwashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kukubalika kwake. Niliweza kutumia nafasi hiyo na nikakubaliwa na wananchi, namshukuru sana. *(Makofi)*

Natoa ahadi kwa wananchi wa Kibaha, kwa Serikali yangu na Chama changu na UWT kuwa nitafanya kazi karibu nao sana na sitawaangusha. Nawaomba watendaji, mimi na wao tufanye kazi kama ndugu kwa maendeleo ya Mtanzania, Madiwani wangu tufanye kazi kama ndugu, viongozi wote, nikisema viongozi wote ni pamoja na wa Vyama vya Upinzani waliokuwepo Kibaha nitafanya nao kazi kama wenzangu. Ninaziomba *NGOs* wengine ninaowafahamu nitawafuata, nisiowafahamu naomba waje wanisaidie kwa maendeleo ya wananchi wa Kibaha Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Zanzibar, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Spika na Naibu Spika, Wabunge, Mawaziri na Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu na Wakuu wa Mikoa. Naomba tufanye kazi, Mtanzania hana haja ya upinzani haja yake ni maendeleo, kwa hiyo, tusaidiane nao ili tuendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nirudi kuchangia hotuba, Mheshimiwa Rais, alipokuwa anazunguka kuomba kura alipokuja Kibaha Mjini aliahidi ili Kibaha isiwe maficho ya Mkoa wa Pwani aliahidi kuwa ataleta viwanda. Kwa hiyo, naomba Wizara ya Viwanda iweke mpango madhubuti kwenye hili ili ahadi hii itekelezeke Rais asionekane mwongo.

Mheshimiwa Spika, moja ya kero Kibaha Mjini ni maji, naomba *DAWASA* na *DAWASCO* kwa sababu maji yanayopelekwa Dar es Salaam bomba lake linapitia Kibaha yaani Ruvu Juu na Ruvu Chini pia ingawa inapitia Bagamoyo lakini ina ukaribu na Kibaha, naomba pia watandaze mabomba ambayo yatawasaidia wananchi wa Kibaha Mjini yote sio kwa eneo fulani. Kwa hiyo, naomba hilo lishughulikiwe na hiyo ni kero ya kwanza ya wananchi wangu.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Kibaha sasa imekuwa mji lakini bado iko katika mazingira ya kijiji. Hivi sasa bahati nzuri ya Kibaha haijavamiwa kwa majenzi holela holela. Naomba Wizara ikae na mimi na wataalam tufanye Kibaha uwe ndio mfano wa mji ulioanza sio katika *shunt town*. Ninaomba Wizara inisaidie kwa hilo na bahati nzuri mji ule ndio makao makuu ya Mkoa wa Pwani na kaka yangu Kikwete ndio utakuwa mji wake huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye ajira. Wananchi wengi hasa vijana, wakulima, hili suala la ajira limempa sifa kubwa Kikwete. Naomba Wizara husika isikae chini kusudi imani hii isije baadaye tukataniwa. Ninaomba kwa wale watakaoajiriwa ushauri wangu wa kwanza elimu. Elimu ya msingi, sekondari na ya mafunzo yaani taaluma iwe na *continuity* mtu asimalize elimu ya msingi anakwenda sekondari Mwalimu anafundisha anashangaa lugha, ana akili kwa sababu haelewani na Mwalimu anajikuta haelewi kwa hiyo akifika chuo kikuu ndio kabisa.

Kwa hiyo, naomba iende kwa mtiririko. Ninaomba tupate wataalam ambao tutawashindanisha ndani ya nchi na nje ya nchi. Tuchukue mfano wa wenzetu Afika Magharibi wenzetu wengi wanaajiriwa nje na ndani ya nchi. Ninaomba tusiwe na ukiritimba tuwe kwa mfano Madaktari watatu, mafundi wanne, aah, tuwafundishe wengi.

Mheshimiwa Spika, natoa mfano wa Udaktari kwa sababu mimi ni Daktari kwamba tufundishe *Medical Officers* wengi ili hata kwenye *dispensary* za vijijini wawepo, tusifikirie tu *Clinical Officers, Paramedics* aah, tufundishe hao hao *Medical Officers* wengi ili itakapofikia wakati wengine wanataka wapate pesa nyingi za mshahara na sababu wanashawishiwa na *Senior Doctor*s basi matokeo wajikute wanaweza kukosa kazi tukiwa na wataalam wengi na ukiritimba utaondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tulivalie njuga suala la ajira, kuna ajira tayari, walimu wa Kiswahili wanatakiwa, Tanzania mmeshajiandaa kiasi gani? Wanatakiwa wengi Afrika kwa mfano kule Libya wanataka walimu wa Kiswahili wengi tu. Naomba hili tulivalie njuga tusisinzie twende kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya katika kipindi cha miezi sita tuwe tumeshapeleka walimu kule, hiyo ni ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kujiajiri hapa ndio ajira kubwa ilipo. Kwanza ajira ya kilimo. Bado hatuko *serious* kwenye kilimo. Tuna Maafisa Ugani wanakaa mjini hawaendi vijijini. Mtu kapewa pikipiki anakaa makao makuu ya Jimbo unafika mahali kwa mfano Kibaha unautizama mkorosho una matawi mpaka chini, unauliza Afisa Ugani yuko wapi.

Sasa mimi naomba Afisa Ugani muwapangie taratibu za kazi na mfano tutaupata kwa kilimo bora kwa wananchi na wananchi watalima kilimo bora wakifundishwa.Watu walikuwa wanakataa kupeleka watoto wa kike shuleni lakini sasa ukiacha kupeleka mtoto wa kike unatiwa ndani watu sasa hivi wameona elimu muhimu na hii tuwalazimishe maafisa Ugani wakawafundishe ili mtu akishika jembe kulima alime kilimo cha kisasa.

Naomba ikiwezekana kuna Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, wao wana mradi mzuri unaweza kusababisha ajira na kisoma. Inakuwaje? Unachukua vikundi kwa mfano sasa hivi kuna *camps* za vijana kwa mfano mafundi seremala, waimbaji na wasanii wa kila aina, wana utalaam wa aina mbalimbali wawachukue hawa na wawaweke kwenye makundi kisha waambie elimu ya watu wazima pamoja na kumwendeleza katika elimu ya ufundi wa ujuzi wake. Wasanii kwa mfano pale Kibaha unawachukua Afisa Elimu Watu Wazima anawafundisha tunakwenda Chuo cha Sanaa Kaole tunawaomba wanakuja wanawafundisha usanii ili usanii pia uwe kazi. Upande wa michezo mfano *footballer* asicheze tu kwa ajili ya afya pia iwe kazi, anaweza kuajiriwa na Simba na Yanga kutokea kijijini. Mpika maandazi tumuombe Bakharesa awafundishe kupika maandazi mazuri ili auze maandazi sio maandazi unavuta mpaka jino linaondoka unamtoa hapa alipo unampeleka pale huyu anayejiajiri. Hilo naomba tusaidiane.

Mheshimiwa Spika, lingine wenzetu wa Thailand wametuambia sasa tushirikiane nao. Wao wenzetu wanatengeneza mvua, naomba Wizara ya Kilimo, hili tusilichukulie utani. Walikuja Wabunge wa Thailand na wakaahidi tushirikiane na nafikiri Katibu wa Bunge atawapa *briefing* wanasema wako tayari kuwafundisha kutengeneza *artificial rain. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba yale mazao yanayostahimili ukame ndio tuyasisitize. Mimi nashangaa tunazungumzia mahindi, mvua hakuna mahindi yamekwisha, muhogo upo. Yale maeneo ambayo muhogo unazaa tuyahimize na tutengeneze zile mashine ambazo unachukua muhogo kutoka shamba unausafisha unauingiza katika mashine unatoa kama *chips* unaanika *in a day* bado muhogo mweupe unatoa unga.

Mheshimiwa Spika, nisipozungumzia utawala bora nitakuwa nimejisaliti. Katika utawala bora nitazungumzia machache. Tunaomba elimu kwa viongozi wote kuanzia

ngazi ya kitongoji, kijiji, mitaa, Madiwani wetu na ngazi ya Wilaya ianze sasa hivi. Kwa hiyo, TAMISEMI waanze sasa hivi sio wangojee bado miaka miwili ndio wanawafundisha inakuwa mnapoteza hela baada ya miaka miwili uchaguzi unakuja wale wanaondoka. Kwa hiyo, naomba sasa elimu ianze.

Mheshimiwa Spika, lingine ni sheria, naomba hizi sheria zifike kwa wananchi na viongozi wetu kwa lugha ya Kiswahili, Kiingereza hawajui jamani kwa sababu lugha yetu ni Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, *PCB,* naomba nao tuwape uwezo, taarifa zao zije kwenye Bunge kama sio kwenye Bunge zima iingie katika Kamati maalum tuwe tunajua nani wenzetu hawa wanaotunyanyasa. Lingine basi wawe na uhuru sio kila wanachotaka kabla hawajapeleka Mahakamani *DPP, DPP* naye ni binadamu. Suala la mikataba, naomba mikataba mikubwa ipitie Bungeni, mikataba kupitia Halmashauri wapewe Madiwani waione. Huo ni ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye utawala bora suala ambalo tunalitania lakini litatufikisha mahali pabaya ni suala la rushwa Mahakamani. Mimi nilikuwa nawaambia historia ya watu kuanza kupiga wezi ilianzia Dar es Salaam baada ya kuchoshwa wakiripoti wezi, wezi wanapelekwa wanarudishwa halafu wanawaumiza watu, watu wakachukua sheria mkononi. Zamani ilikuwa mtu kupigwa mpaka kufa au kuona damu mtu anasisimkwa lakini sasa hivi ni kitu cha kawaida. Tunawafundisha watoto wetu roho ya imani inaondoka wanajua kuua ni kawaida na hii tutawafundisha watoto wetu waondokwe na amani ile tu kusisimkwa kuona damu ndio inasaidia amani pia leo unaua hovyo.

Mheshimiwa Spika, naomba tuwe na utaratibu, Serikali inasimamiwa na wananchi na Wabunge ikifanya vibaya wananchi wanaiondoa Wabunge wanaisimamia, Bunge linasimamiwa na wananchi wake ukifanya vibaya Mbunge au chama kinaondolewa na ndani ya Bunge pia kuna Kamati lakini kwenye Mahakama kuna Kamati inayohusika na Mahakama tu wanaweza kulindana. Basi kuwe na utaratibu ikiwezekana ile Kamati ya Haki za Binadamu iwe na fursa pale mtu kweli ameonewa, hukumu inaonyesha imemuonea lakini hana uwezo wa kwenda mbele najua kuna uwezo wa *referral* lakini waki-*twist* tu hapa mambo ya sheria mtu unaweza kukosa. Kwa hiyo, angalau ile Kamati ya Haki za Binadamu iruhusiwe mtu kweli kaonewa na Mahakama na hukumu inaonyesha kabisa hapa ameonewa basi na wao wawe na uwezo sasa hivi hawana uwezo wa kuingilia Mahakama. Ndio maana Mahakama tukiifanyia utani itaipeleka Tanzania mahali pabaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, mimi ni daktari nimefundishwa *punctuality,* nasema namshukuru na naipongeza hotuba ya Mheshimiwa Rais na naiunga mkono. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Pia muda wa kusitisha shughuli zetu kwa asubuhi hii nao umewadia. Ninayo matangazo. Kwanza saa 11.00 jioni ile kipindi cha jioni wachangiaji

atakayetangulia ni Mheshimiwa Stella Manyanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdulkarim Shah.

Tangazo la pili, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, anatangaza kwamba huduma za *passport* kwa Waheshimiwa Wabunge bado zinaendelea wahusika toka Uhamiaji wako chumba Na.3 kwenye jengo lile la huduma za Posta na Benki. Lingine ni kwamba Kamati ya Uongozi, tutakwenda kukagua jengo la ukumbi mpya wa Bunge mara baada ya kusitisha shughuli hivi sasa, tukutane sasa hivi saa saba hii kwanza hapa kwenye *Lounge* ya *Speaker*.

La mwisho nataka kukumbushia tu, kumekuwa na ukiukwaji mkubwa sana wa Kanuni 53 na inashangaza hasa kwa upande wa Waheshimiwa Mawaziri. Hairuhusiwi wakati kuna mchangiaji, Mheshimiwa Mbunge yeyote apite katikati yaani ukimtazama Mheshimiwa Mbunge anayechangia na Spika usikatize katikati yake. Ndio hivyo tunaanza basi twende kidogo lakini mara nyingine itakuwa kidogo fedheha mtu ukikumbushwa hilo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 07.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Tulikuwa tumependekeza saa za asubuhi tulikuwa tumependekeza kuwa ili kuwapa nafasi waliojiorodhesha wote 93 waweze kuchangia hoja hii muhimu ningemuomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kutumia kifungu kile kanuni ya 124 atuingize katika kanuni ile ya 49(A)(a) ili iweze kutenguliwa kuturuhusu kutumia muda mfupi zaidi yaani badala ya dakika 15 tutumie dakika 10.

Mheshimiwa Waziri.

## HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Kufuatana na kama ulivyoeleza kanuni ya 124 (1) inayosema kwa idhini ya Spika yoyote kati ya kanuni hizi yaweza kutenguliwa kwa madhumuni mahsusi baada ya Waziri kutoa hoja kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa hoja kwamba Kanuni ya 49(A) (a) ambayo inasema kila Mbunge anayejadili hoja ataruhusiwa tena kwa muda usiozidi dakika 15 sasa naomba kutoa kwamba kanuni hiyo itenguliwe na Bunge hili na badala yake Waheshimiwa Wabunge waruhusiwe kusema kwa dakika 10 ili kuwapa nafasi Waheshimiwa Wabunge wengi zaidi kushiriki katika mjadala huu muhimu kwa taifa letu ili isitokee Mbunge wa kubaki bila kutoa na yeye hoja zake.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Kutengua Kanuni 49 (a) (i) iliridhiwa na Bunge)*

**MHE. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa akina Mama wa Mkoa wa Ruvuma kwa kauli yao moja ya kunichagua kuwa mwakilishi wao, hata hivyo napenda pia niwashukuru akina Baba wa Mkoa wa Ruvuma pamoja na Vijana kwa kuwa kila penye Mama kuna Baba na hivi kwa namna moja ama nyingine waliweza kuchangia ushindi wangu.

Napenda pia nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete pamoja na Mheshimiwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mheshimiwa Amani Abeid Karume na vilevile napenda kukupongeza wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika pamoja na Mawaziri wetu walioteuliwa katika awamu hii ya nne kwa kuweza kupata nafasi hizo na wote tunaahidi tutawaunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Rais nikirejea ukurasa wa 33 kuna kifungu kinachozungumzia jinsi ya kusambaza utajiri uliopo pamoja na ku-*share* umaskini uliopo. Mkoa wa Ruvuma mimi naufananisha ni sawa na Mama ambaye ameweza kulea watoto wake kwa muda mrefu, wakasoma halafu baadaye wale watoto waseme kwamba hatuwezi kumtunza mama kwa sababu hazalishi tena wakaamua ku-*concentrate*, kuendelea na vijana kwa sababu wao wanazalisha.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu gani. Hata juzi tulivyoambiwa katika tatizo la njaa Mkoa wa Ruvuma haumo katika wale wanaohitaji kupelekewa chakula lakini kwa kweli Mkoa wa Ruvuma pamoja na Wilaya zake mfano Wilaya ya Mbinga ni Wilaya ambazo zimeanza zamani toka mwaka 1965 lakini ni hali ya kusikitisha sana hali ya mkoa wa Ruvuma bado iko nyuma sana katika masuala ya maendeleo kwa mfano viwanda, hatuna kiwanda hata kimoja na hivyo kutufanya kwamba hata tunapohitaji kusindika mazao yetu kwa mfano maembe tunashindwa matokeo yake tunaona uchungu yanavyooza na wakati juhudi kubwa zinakuwa zimefanyika.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna sababu ambazo zinazungumzwa za umeme, tumekuwa tukiahidiwa kila siku pamoja na ahadi ya mwisho ambayo Mheshimiwa Rais ametupa

lakini kwa kweli mimi sioni kuna sababu gani zinazofanya Mkoa wa Ruvuma hususan Mbinga kukosa umeme wakati Bunge hili linapozungumzia masuala ya gharama zinazohusika katika kuchangia umeme ambao unazalishwa kwa mfano na IPPL au Songas, ni watu wote wa Tanzania wanahusika katika kuchangia ruzuku hiyo lakini wanafaidi wachache. Tumepewa ahadi nzuri sana safari hii, tunaamini Wizara inayohusika pamoja na watendaji ambao wako *TANESCO* hawatatupa tena kiswahili ambacho hakina sababu za Msingi kwa sababu ni agizo tunaomba watekeleze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikiwa kama Mama nitakuwa si mwingi wa fadhira kama sitaweza kutoa shukrani za dhati kwa Mama Salma Kikwete ambaye aliweza kutumia muda wake kwa uvumilivu mkubwa kuutembelea mkoa wa Ruvuma. Aliweza kufika hata kwenye sehemu ambazo hazifikiki kirahisi na alikuwa amefunga, maeneo ya Lusewa na Liuli. Hata mkuu wa msafara alihofu kwa nini nimefanya safari ndefu hivi lakini Mama Salma kwa ushujaa kabisa alisema huko ndiko wanakokaa wapiga kura ni lazima tuwafikie. Tunamshukuru sana.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini si hivyo tu kwa heshima hizohizo na kwa ahadi ambazo Mheshimiwa Rais amezitoa tumeona kwamba dawa ya kumpata kwa mfano kama chui amekaa mahali unataka kumuwinda humpati basi chukua mtoto wake utampata, sasa sisi tumeona tukiwa na Mama yetu, Mama Salma kwa vyovyote vile basi tutafanikisha mambo yetu kwa sababu tumesahaulika muda mrefu. Kwa hiyo tunaomba mtufikishie salamu tunamuomba awe mlezi wetu wa Mkoa wa Ruvuma ili tuweze kupiga hatua za maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia kwa nafasi hii uliyonipa niweze kutoa taarifa ambayo mara nyingi nimekuwa nikiisoma kwenye magazeti. Kuna maneno yanazungumzwa kwamba "ndiyo maana wasomi wengi sasa wanahamia Bungeni". Mimi nikiwa kama Mtanzania kwa kweli ninaposoma habari hizo zinanisikitisha sana kwa sababu Bunge hili siyo la watu wajinga kwani linajadili mambo ya busara na ya msingi linataka kuwe na wasomi inavyowezekana na ndiyo maana hata wale walioingia wakiwa na vyeti vya kawaida sasa hivi kwenye Bunge hili wanajiendeleza. Kwa hiyo tunapenda kutoa rai kwa watu wote wasomi wote wanaozungumza sentensi hiyo ni kwamba inaashiria hawajui faida za kusoma. Tunaomba wabadilike na wote wawe kwenye msimamo wa kuhakikisha kwamba maana ya elimu ni kutumika katika sekta zote na maeneo yote ili kuweza kuharakisha na kuchochea maendeleo.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nirudi kwenye upande wa taarifa mbalimbali ambazo tumezipata kutokana na sera zetu nzuri zilizotengenezwa. Nawaomba sana Waheshimiwa Waandishi wa Habari, kwanza nawapongeza kwa juhudi mlizofanya kuelimisha kuhusiana na maslahi wanayopata Wabunge ni jambo zuri wananchi wetu wakafahamu lakini vilevile tungeshauri ikiwezekana muendelee na utaratibu huu hata katika sehemu nyingine.

Lakini si hilo tu hasa, ninaomba sasa katika zile sera ambazo zimekuwa zikizungumzwa mara kwa mara mzipigie makelele kwenye magazeti yetu nafahamu wananchi wengi au vijana wetu wengi wanaomaliza wanashindwa kujiendeleza au

kuweza kujitafutia ajira kutokana na kukosa taarifa mbalimbali. Mimi ninavyoelewa ukweli ni kwamba maendeleo yanatokana na juhudi zake mtu mwenyewe, hakuna wa kuweza kukutafutia maendeleo, watu wanakuwa wamesoma lakini faida ya kusoma ni pamoja na kujua hii elimu niliyoipata inanisaidia vipi na katika mazingira yapi ili kuweza kuwa wajasiriamali. Wengi wanafikiria ujasiriamali ni kile tu kitendo cha kumuona mtu anafanya biashara la hasha! ujasiriamali ni jinsi gani wewe unaweza kubuni au kufanya kazi zako vizuri kiasi kwamba ukamfurahisha mteja wako au wewe mwenyewe ukajiingizia kipato cha ziada (faida).

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nakushukuru sana naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana.(*Makofi*)

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Rais wetu katika hotuba yake aliyoitoa Bungeni katika Bunge lililopita wakati wa ufunguzi.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze yeye kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuteuliwa kwake na kuthibitishwa na Wabunge wote, pia nakupongeza wewe kwa kupata kura za kishindo pamoja na Mheshimiwa Naibu wako wa Spika pamoja na Mawaziri wote na Manaibu na Wabunge wote mliokuwemo humu ndani, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, naomba katika kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Rais nilikuwa ni kukazia tu katika ukurasa wa 28 wa hotuba yake katika kitabu katika eneo la uchumi endelevu wa kisasa unaokua.

Mheshimiwa Spika, "anasema kwa mujibu wa ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kazi ya Msingi ya Serikali ya awamu ya nne ni kukuza uchumi kwa lengo la kuongeza kipato cha Watanzania ili waishi maisha bora zaidi".

Mheshimiwa Spika, haya yote katika kuboresha haya mambo lazima sehemu husika jambo la kwanza kabisa ni kuhakikisha kwamba miundombinu ya hilo eneo inakuwa mizuri.

Mheshimiwa Spika, leo ni miaka 44 toka tupate uhuru, wamepita Wabunge wengi leo mimi ni kipindi changu cha pili silaumu wala siseme lakini nafahamu kutokana na hali ya nchi ilivyokuwa lakini naomba sana safari hii ahadi hizi zimesemwa sana, Viongozi wetu waliopita wametoa ahadi hizi na walisema kwamba zitatekelezwa lakini matokeo yake hawakujaliwa kwa sababu tunafahamu kila jambo lina wakati wake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba sana kwa kupitia Serikali ya awamu hii ya nne na hasa leo Mheshimiwa Rais wetu alipokuwa akiwahutubia wananchi wa Dodoma alisisitiza sana juu ya mpango wa mikakati wa ilani ya uchaguzi kuwaeleza kwamba Waheshimiwa Mawaziri waliochaguliwa safari hii watakuwa imara na watafuatilia kwa karibu kabisa chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu Edward Lowassa.

Mheshimiwa Spika, sasa ninachoomba sana Mafia adha yetu kubwa ni gati, gati ndiyo kilio chetu tunakililia ili wananchi wa Mafia waweze kuwa na uchumi mzuri, uchumi endelevu. Wilaya ambayo iko ina vivutio vingi vya utalii inaweza ikaleta pato kubwa kabisa katika kuchangia pato la nchi yetu lazima gati liwepo na uwanja wa ndege uwepo mzuri bila ya hivyo hali itakuwa mbaya. Kwa kauli aliyosema Mheshimiwa Rais kwamba tuhakikishe kwamba na sisi Wabunge ahadi tulizotoa. Mimi kama Mbunge wa Jimbo la Mafia niliwahakikishia najua sitoi pesa hizo mfukoni kwangu lakini tulisema kwamba gati litajengwa, uwanja wa ndege utajengwa na bahati nzuri alipokuja Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni nae pia aliahidi.

Kwa hiyo kama alivyotoa ahadi katika daraja la Simbiru naomba sana Mheshimiwa Waziri kupitia Wizara zako, Waziri wa miundombinu ajitahidi sana safari hii uwanja wa ndege wa Mafia ujengwe, jitihada zako Mheshimiwa Waziri wa Mazingira Mheshimiwa Professor Mwandosya tumeziona tunakushukuru na imani hiyo naamini itaendelezwa sana na Mheshimiwa Waziri wetu wa miundombinu Bwana Basil Pesambili Mramba kwamba na yeye anafahamu fika tatizo la Mafia ndiyo maana aliamua kutoa zile shilingi bilioni 2 lakini safari hii naomba sana Serikali iweze kutuangalia.

Hali ya uwanja ni mbaya wakati wowote mnaweza mkasikia ajali inatokea mafia, hali ni mbaya sana. Naomba sana Serikali hii isitufedheheshe kwa sababu Mheshimiwa Rais ameshatoa ahadi ametamka mbele ya umma wa watu wa Mafia naomba sana ahadi hizi zitekelezwe.

Mheshimiwa Spika, Mafia kazi yetu kubwa ni uvuvi na mifugo kidogo lakini uvuvi ndiyo suala kubwa tunaomba sana kupitia kwako Waziri wa Maliasili na Utalii ahakikishe huu mradi wa *MACEMP* unaanza haraka unakuja na kuweza kuwapatia wavuvi wetu wa Mafia, wenyeji wa Mafia zana bora za kisasa zinazokubalika kimazingira ili na wao waweze kupata kipato kizuri, waweze kutunza mazingira ya eneo letu la bahari na pia kulipatia Taifa letu hasa Halmashauri yetu pato kwa ukusanyaji wa ushuru wa yale mazao watakayokuwa wanayatoa baharini.

Mheshimiwa Spika, kilimo Mafia nako tunalima, adha hii ya njaa sisi Mafia laiti kama tungekuwa na japo matrekta miwili niliongelea katika Bunge lililopita tunaomba matrekta angalau miwili tufanye kazi, lakini kwa bahati mbaya matrekta hayo hayakupatikana. Lakini ninaamini naomba sana Wizara ya Kilimo tukishirikiana na Halmshauri yetu na sisi tupo tuweze kufanikisha kupatikana kwa haya matrekta na tutalima na tutaweza kupunguza adha ya njaa katika maeneo ya Wilaya yetu. Hali ya Mafia si mbaya sana kama Wilaya nyingine lakini nashukuru Mwenyezi Mungu jana imenyesha mvua nyingi kabisa hata ndege ilishindwa kurudi, naomba mvua hii iendelee kwa nchi nzima kwa nguvu za Allah!

Mheshimiwa Spika, sina mengi ya kusema natumia fursa hii ya mwisho kabisa kukuombeni nikiwa kama Mbunge wa awamu ya pili nia yangu ni kuendeleza na kutoa fikra zangu kwa nchi hii na Bunge hili naomba tu niwaambie Wabunge wenzangu kwamba nimechukua fomu ya kugombea Ukamishna natumia fursa hii kuwaomba ili

mnichague niweze kutetea maslahi ya Bunge, Wabunge na watumishi wake na kuliweka Bunge katika " Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya". Ahsante Sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa atafuatiwa na Mhesahimiwa Dr. Raphael Chegeni.

Nieleze tu kwamba kengele ya kwanza ni baada ya dakika saba halafu unakuwa na dakika tatu za kumalizia.

Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. KHALIFA S. KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru mimi naanza kwa kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Gando kwa kunipigia kura nyingi na kunirudisha tena kama Mbunge wao tena hapa. Naamini wamenichagua kwa kuniamini na mimi nitajitahidi nisiwasaliti kwa kuwafanyia yale ambayo yamo ndani ya uwezo wangu yote.

Mheshimiwa Spika, pili napenda nianze kwa kusema kuwa naiunga mkono mia kwa mia na mimi hii hotuba ya Mheshimiwa Rais na ninataka kuzungumza mambo matatu tu katika mambo mengi mazuri yaliyomo lakini nataka nijielekeze katika mambo matatu.

Mheshimiwa Spika, la kwanza ni suala la kilimo. Kwa kweli inaonekana tuna tatizo na tatizo hili kama hatujabadilika basi siku zote itakuwa ni malalamiko hayahaya njaa na kadhalika, *mind set* yetu badi haijabadilika hivi kuna sababu gani watu wanaoishi kandokando ya maziwa au mito walalamike wana njaa ilhali wanaweza kuchukua maji hata kwa keni tu wakamwagilia ekari moja au mbili za mahindi wakapata kula na watoto, mambo haya ni kwa sababu hawajataka kujielekeza wanaamini Mungu yupo na sisi tuamini hivyohivyo lakini Mungu anasema tujitahidi. Sasa ni vizuri basi Serikali ikawachukua wataalam ikawapeleka kwenye sehemu za vijiji, sehemu wanakoishi wananchi wakawaamsha juu ya hili.

Mheshimiwa Spika, Pili ni suala la ujambazi. Suala la ujambazi kwa kweli linaonekana ni tatizo na kila utakalosema basi lina mwelekeo wa kukubalika, ukisema polisi labda wanahusika unaweza ukaamini hivyo kwa sababu inakuwaje mtu anavamiwa mita 100 kutoka walipo polisi halafu hapati msaada? Unapiga simu haijibiwi, vitu kama hivi vinatisha lakini pia mimi naamini hata suala la woga linaweza likachangia kwa sababu hata mimi kama tunagombana na wewe ukaniona nina fimbo wewe uko mikono mitupu unaweza kufikiri mara mbili ili uweze kuja kupigana.

Sasa vijana hawa wanaofanya ujambazi inaonekana kwanza wana mafunzo pili wana silaha kali, siku iliyovamiwa pale Mkunguni kijana yule kashika silaha kwa mkono mmoja anamimina risasa kama chicha, mkono mmoja tu. sasa ni kweli haiwezekani jambazi ana AK 47 ukamchukua mtu ana silaha ndogo yake akampelekea na Serikali

mimi naamini inaweza ikitaka kufanya mambo haya, ni mashahidi sote hapa kabla ya uchaguzi tumenunua magari ya maji machafu kwa pesa nyingi, tumenunua manuwari, tumepeleka vijana wetu mahali mbalimbali ili kulinda uchaguzi wetu tumeshindwa nini kuwanunulia askari hawa silaha za kuweza kukabiliana na majambazi? Tunaweza tukafikiri labda ni *syndicate* ya kuleta ubaya lakini pengine ni woga hili mimi nafikiri tulifikirie kwa kina (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatu, kwa masikitiko makubwa mimi nataka nizungumze suala hili alilolizungumza Mheshimiwa Rais la Mpasuko. Kwanza mimi napenda tutanabahi kuwa Rais hakutuuliza kuwa upo mpasuko au hapana, yeye alisema upo, sasa tunapokaa humu ndani tukasema hapana mimi naona ni *insubordination* kwa Rais mimi natafsiri hivyo. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili mimi nawaomba sana ninyi watu wa Chama cha Mapinduzi na Wabunge wenzangu wengine tumsaidie Rais kwa hili. Tatizo lipo na mimi nakuangushieni ninyi tatizo kwa sababu sisi kama mtakumbuka kina Dr. Mwakyembe hawa na wenzake walikuwa kwenye Tume ya Muafaka tulifikiri mambo mengi tu mfano mdogo tu katika Muafaka walipendekeza hata Serikali ya pamoja katika Zanzibar ili ku-*stabilize situation*. Sisi kwenye Chama chetu hili jambo tulilikubali taarifa nilizonazo ninyi Chama cha Mapinduzi mlikataa sasa ni ninyi Chama cha Mapinduzi wa ku-*push forward* hili jambo ikiwa kweli tunataka maslahi ya nchi yetu lah! kama tunakuja hapa tunanunu kofi kwa kusema maneno ya ajabu ajabu na ninyi mnazipiga kwa sababu tunanunua inatisha sana.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tatizo tunalo mimi nawaambieni tatizo lililojitokeza Pemba baada ya uchaguzi mtu yoyote hapa kama analijua basi angeweza kusikitika badala ya kuchukulia kijuu juu akaona ni mambo ya masihara. Hivi ni nani katika sisi hapa angekubali aje achukuliwe mtoto wake ndani atolewe nje, apigwe asema mimi sasa jamani nimeshachoka kupigwa na nimeshachoka kubeba mawe anaambiwa nenda zako anapigwa risasi anakufa. Hivi nani katika sisi angekubali?

**MBUNGE FULANI:** Unao ushahidi?

**MHE. KHALIFA S. KHALIFA:** Ninao ushahidi, ninao ushahidi.

*(Hapa vielelezo vilionyeshwa Bungeni)*

**MHE. KHALIFA S. KHALIFA:**Mheshimiwa Spika, mimi katika kadhia ile iliyotokea Piki, mimi Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano pamoja na kuwa Bunge lilikuwa limeshavunjwa lakini kwa mujibu wa Katiba mimi namaliza shughuli zangu pale anapotangazwa Mbunge mwingine katika Jimbo.

Mheshimiwa Spika, mimi nimetekwa na nimepigwa na vijana wale wamejazwa fikra za ajabu ajabu anakwambia sisi tumekuja hapa kutia adabu Wapemba. Ushahidi huu hapa hatusemi kwa kunong'ona ninayo *CD,* ninazo picha hizi hapa. Vitu kama hivi vinasikitisha na ni vitu vipo, vitu vipo.

Kwetu katika historia ya Zanzibar moja katika tukio baya na lililokuwa ni *highly provocative* kwa Serikali ni mwaka 1972 kama tukikumbuka ameuliwa Rais wa nchi lakini hapakufanywa *capital punishment* hata siku moja, ameuliwa Rais walioshukiwa kuhusika walikamatwa, wakahojiwa, wakahukumiwa hawakuhukumiwa watu wote leo Piki palitokea tatizo ambalo mimi nalilaani, mimi nalilaani kama Mbunge na kama mtu wa Chama cha *CUF* nalilaani. Lakini hivyo kweli? Suluhisho la tukio lile ni kuwavamia watu wote wa Piki ukawaibia, ukawapiga, ukawanajisi watoto wao, ukawabaka watoto wao kweli? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, halafu tunakuja hapa tunasema watu wanajaribu kubeza mambo haya, tunabeza matatizo madogo baadaye yanaweza yakazaa matatizo makubwa. Watu wanafikiri madhali anamiliki bunduki mikononi mwake *he has everything that is not the case to be.*

Mheshimiwa Spika, kwangu mimi *I feel very much ridiculous a sensible person with sound brain you are adopting the posture of an ostrich in a sand storm,* kwa sababu jambo hulitaki unaficha uso unasema halipo, lipo hata kama wewe hutaki kuliona. Huo ndiyo ukweli ulivyo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda niliase sana katika Bunge letu, sisi ni Wabunge tunapewa hizi *Diplomatic Passport* kwa maana ya kuwa sisi tuna hadhi ya Kibalozi kwa vile maneno yetu humu ndani yanatakiwa yawe hivyo hivyo, nchi yetu ina uhusiano mzuri na nchi nyingi, Rais wetu anajulikana dunia nzima kwa sababu ya tabia yake na uhusiano wake tunapokaa humu ndani si vibaya kama tutawataja watu mmoja mmoja lakini ni makosa makubwa kuitaja nchi kwa sababu ukiitaja nchi katika chombo kama hiki hii ni *allegation* kubwa *and you have to prove it*.

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa tutofautishe sana maneno ya vijiweni na maneno ya ndani ya Bunge, lakini mimi sishangai kwa sababu inaonekana labda tunataka kutumia Bunge hili katika ku-*insight* na humu ndani ya Bunge watu wachukiane, humu hatutachukiana hata siku moja tutajadili hoja, tutazi- *analyse* na hoja ambayo itakuwa ni ya msingi itabakia kuwa ya msingi hata kama watu wataibeza namna gani.

Mheshimiwa Spika, namalizia maneno yangu kwa kusema tumsaidie Mheshimiwa Rais kwa hili sisi kama Chama, sisi kama Wabunge tunakuhakikishia tutatoa ushirikiano tunaouweza. Nakuombeni sana na ninyi mfanye hivyo ili Rais aondokane na hili tutazame mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi uliyonipa na ninaunga mkono haja iliyo mbele yetu.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Khalifa Khalifa sasa namuita Mheshimia Dr. Raphael Chegeni atafuatiwa na Mheshimiwa Lucas Selelii.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais.

Kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais, nikupongeze mwenyewe Spika, nipongeze Waheshimiwa Mawaziri na niwapongeze Wabunge wenzangu kwa kuchaguliwa na kurudi katika Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kazi ya uwakilishi ni kazi ngumu sana na kazi ya uwakilishi inatakiwa jamii inayowakillishwa ndiyo ieleweshwe vizuri pasiwepo na tafsiri tofauti katika dhana ya uwakilishi.

Mheshimiwa aliyetangulia kusema amesema kwamba kumekuwa na dhana potofu ambayo imejengeka miongoni mwa Watanzania kuona kwamba Wabunge wanaostahili kuja hapa ni watu ambao hawana sifa stahimilivu za kuingia ndani ya Bunge, hii ni dhana ambayo ni potofu kwa sababu Wabunge ni watu ambao wanasaidia Serikali kufikia maamuzi na kuisimamia Serikali ifanye maamuzi sahihi kwa maslahi ya wananchi.

Sasa tukiiachia hii iendelee namna hii matokeo yake tutafika pabaya, Mheshimiwa Rais katika *theme* yake yote ni maisha bora kwa Watanzania, maisha bora kwa Watanzania na hata leo amesisitiza kwamba angependa kuwa na Serikali yenye kuwajibika kwa wananchi lakini inapofikia suala hili sijui Bunge ni sehemu ya Serikali, sijui ni kitengo cha Serikali au na yenyewe ni muhimili mojawapo kati ya mitatu katika nchi hii sasa hiyo heshima isipoangaliwa tutafikia pabaya.

Mheshimiwa Spika, mimi napenda niseme kwamba ni vema vyombo vinavyohusika na wananchi wanaohusika waelimishwe umuhimu wa kuwepo na chombo hiki katika nchi, waelimishwe umuhimu kwamba Wabunge ni watu ambao wanakaa na kujadili maslahi ya Watanzania. Pamoja na hayo sasa napenda nirudi kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais. Tumekuwa mara nyingi tukirukia mambo mbalimbali, ikitokea njaa sasa hivi tunafanya kazi ya zimamoto lakini njaa haijaanza kutokea leo kila miaka inatokea ikitoea tunatafuta chakula, tunapata wananchi wanahudumiwa tunaendelea. Mimi ningependa sasa tuwe na mkakati endelevu ili njaa hii isije kurudia mara kwa mara.

Waheshimiwa mnajua kwamba tuna mabonde mazuri, tuna mito, tuna maji kutoka ziwa Victoria ambayo yangeweza kutumika kuanzisha kilimo cha kumwagilia na kuweza kupata mazao kwa ajili ya chakula. Lakini sisi ni wazuri sana wa kusema na ni wachovu sana wa kutekeleza mambo kitu ambacho nadhani ingekuwa vema sasa kwa *spirit* mpya ya Serikali mpya tuwe na upeo wa kuweza kuwa endelevu tufanya mambo endelevu tusifanya mambo kwa ajili ya kurukia na baadaye ikishaisha tatizo tunakaa kimya.

Mheshimiwa Spika, umahiri wa Waziri Mkuu unafahamika, mimi nilikuwa Cairo. Cairo wanasema kwamba wanaikumbuka Tanzania kwa mambo manne. Jambo la kwanza ni Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, ukimtaja Misri anafahamika kama fedha ya Misri. Jambo la pili, wanafahamu Simba *Sport Club* na jambo la tatu wanafahamu Jiji la Dar es Salaam. Lakini juzi wanasema tunamfahamu mtu anayeitwa Edward Lowassa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wanasema kwa sababu ni kuhusu suala la kuanzisha mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria na kuweza kuyapeleka katika Mikoa ya Mwanza na Shinyanga. Kitendo hicho ni cha kihistoria, kimekuwepo miaka mingi lakini hakikufanyika, kimefanyika katika kipindi hiki, kwa hiyo kwa sifa hiyo ninaamini Mheshimiwa Lowassa ana uwezo mkubwa sasa wa kuiongoza Serikali pamoja na Baraza la Mawaziri katika kutekeleza majukumu ambayo Watanzania wanayategemea. Sasa hivi Mheshimiwa Rais amejenga matumaini makubwa sana kwa Watanzania na sisi tuna wajibu mkubwa sana kumsaidia katika ngazi mbalimbali ili matumaini haya yaweze kutekelezwa. Lakini kuna matatizo, tumezungumza suala la rushwa na suala la Mikataba. Naomba tukifika hapo tufungane kengele. Hili suala la Mikataba mibovu waliohusika basi ni vema wakawekwa wazi, ni vema wakachukuliwa hatua, ni vema tukapata fundisho na Watanzania wakaridhika. Kwa sababu tusiishie kuzungumza tu, tuna Mikataba mibovu ambayo imefanyika, wahusika wanafahamika wengine na nashukuru kuna vyombo vya habari vimeanza kusema kwamba wanaandaa orodha ya baadhi ya watu ambao wamehusika katika mambo mbalimbali yanayohusika na rushwa. Ni vema Watanzania sasa wakaeleweshwa na watu wakawekwa hadharani.

Mheshimiwa Spika, uwiano wa maendeleo katika nchi yetu bado unatakiwa vile vile uangaliwe. Kuna Mikoa ambayo kama ingesaidiwa kwa kuweka fedha ya Serikali vema na ikatumika vema basi maendeleo makubwa sana yangesisimuliwa na Mikoa hii. Nazungumzia kwa mfano, leo asubuhi kulikuwa na swali kuhusu reli ya kati. Mwananchi anayeishi Mikoa ya Magharibi na Kanda ya Ziwa anapata bidhaa kutoka Dar es Salaam kwa bei kubwa sana kwa sababu hakuna huduma ya treni ya kubeba mizigo kutoka Dar es Salaam kupeleka Mwanza au Kigoma. Siku hizi mizigo inakuja kwa magari mpaka hapa Dodoma, halafu wanapakia kwenye treni kwenda Mikoa inayohusika. Yote ni gharama kubwa sana na hawa wote ni Watanzania na ndio maana suala hili tujaribu kuliangalia sana, kama kuna haja ya kuchukua hatua za makusudi basi zichukuliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine, tukija katika suala hili la ujambazi mimi nafikiri tulitafutie dawa. Polisi wale ambao wameonyesha kwamba hawana nidhamu ya Jeshi la Polisi basi ni vema wakafukuzwa. Kuna vijana wengi wazuri wapewe nafasi na naamini kabisa watafanya kazi vizuri. Lakini pili, Jeshi hili la Polisi lina zana ya kupambana na zana za majambazi? Kila mwaka hapa tunahangaika, bajeti ya Polisi ni ndogo, kwa sababu uwezo wa Serikali ni mdogo. Saa nyingine tuwasaidie kuwapatia zana ambazo zitawasaidia kukabiliana na majambazi. Siku zote sisi tu wema wa kusema sana, lakini kutenda kidogo tunapata kigugumizi. Nashauri kwamba suala zima la mchakato huu wa maendeleo sisi kama Waheshimiwa Wabunge tushiriki kikamilifu Serikali yetu itusaidie na Watanzania kwa ujumla tushikamane bega kwa bega. Huu sio muda wa kunyoosheana vidole nani kafanya nini, ni muda wa kufanya kazi ili sote tuweze kusukuma maendeleo ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote haya napenda nimalizie kwa kusema kwamba changamoto tuliyokuwa nayo Watanzania ni kuhakikisha kwamba Ilani ya Uchaguzi tunaitekeleza kwa sababu Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi imezungumzia

mambo mengi sana, yote haya tunapaswa kuyatekeleza na tutafanya hivyo iwapo tutafanya kazi kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Nitoe maelezo hapa baada ya Mheshimiwa Lucas Selelii ilikuwa aje Mheshimiwa Dr. James Alex Msekela, lakini kamwachia nafasi yake Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia. Kwa hiyo sasa namwita Mheshimiwa Selelii, atafuatiwa na Mheshimiwa Amina.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nami naanza kuunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mia kwa mia katika hotuba ya Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Awamu ya Nne kwa kuanza kazi kwa stahili ya aina yake. Kwa kweli imetia moyo wananchi na wananchi wanatoa pongezi kubwa sana kwa kazi hii na changamoto kubwa sana iliyopo mbele yetu ni kuhakikisha kwamba staili hii ambayo imeanzishwa iendelee hadi pale ambapo tutakuwa tumefikisha mzigo mwaka 2010 kwa kazi ambayo itakuwa imeonekana ambayo staili ya Awamu ya Nne imeanza. Mimi nakumbuka wakati ule tumeingia mwaka 1995, Awamu ya Tatu tulianza kwa staili ya *mini budget* lakini mwaka huu tumeingia vizuri, Serikali ina mapato ya kutosha. Nakumbuka wakati ule tulikuwa tunakusanya jumla ya shilingi bilioni ishirini na tano mpaka ishirini na saba kwa mwezi lakini sasa uchumi upo vizuri, unakua kwa asilimia 6.7 na makusanyo ni mazuri ya kila mwezi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Spika, changamoto iliyopo mbele yetu kwa Serikali ya Awamu ya Nne ni kuhakikisha kwamba mapato hayashuki lakini kazi ambayo inategemewa kufanywa na wananchi kwa ajili ya kuwaletea maendeleo inafanyika bila matatizo yoyote. Nami ningependa kutoa wito kwamba changamoto iliyopo katika Serikali ya Awamu ya Nne ni kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2015 basi uchumi wetu wa Tanzania na bajeti yetu ya Tanzania iwe ni bajeti ambayo inajitegemea kuliko kungoja misaada kutoka nje, misaada ije kuja kufanya maendeleo tu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na haya ya utangulizi mimi nilikuwa na haya yafuatayo:-

Ningependa kushauri Serikali ya Awamu ya Nne kuzingatia uchumi wa kijiografia. Nchi yetu Tanzania ni kubwa na ina maeneo makubwa mengi, ina kanda mbalimbali za Magharibi, Kaskazini na Kusini, lakini mimi ningependa kuzungumzia Kanda ambayo natoka, Kanda ya Magharibi na Kanda ya Ziwa. Ipo tabia ya muda mrefu ambayo imejitokeza kutoipa nafasi nzuri Kanda hii ya Magharibi na Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Mikoa ya maeneo hayo kama vile Mkoa wa Tabora, Kigoma, Rukwa, Singida na Mwanza imeachwa kama watoto yatima kwa muda mrefu uliopita. Hii ni hatari sana na inaweza kutuweka mahali ambapo sio vema tukaendelea namna hii. Kwa hiyo kwa staili ambayo Awamu ya Nne imeanza chonde

chonde Serikali hii ya Awamu ya Nne ambayo Kanda ya Ziwa ina rasilimali za kutosha na ikiwekezwa inaweza kuibua uchumi huu ukakua kwa haraka sana kuliko tunavyotarajia na tunavyodhani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo napenda kutoa mapendekezo kwamba, ili twende sambamba na maeneo mengine, naomba Serikali ya Awamu ya Nne iweze kutazama Kanda ya Magharibi na Ziwa kwa jicho la kuleta maendeleo. Mikoa hii ya Magharibi ina rasilimali nyingi za kutosha, ina watu wa kutosha wengi tu karibu watu wote wa kule ni wachapakazi, tena wanafanya kazi kwa kujituma. Kwa hiyo kama Wizara ambayo inataka kuwekeza kujaribu kuwawezesha watu iende ikawekeze katika Kanda hii ya Magharibi na Ziwa, ni watu wanaojituma na wana uwezo na ni waaminifu. Rasilimali hii ya watu inatosha kabisa kwa sababu ni wengi na wana nguvu. Pili, ina mifugo yote kama ng'ombe, mbuzi na kadhalika inatoka katika Kanda ya Ziwa. Tatu, ina mazao; pamba, tumbaku, mchele, samaki, dagaa wa Kigoma wapo wa kutosha na kule Ukerewe samaki wanatosha kabisa kuendeleza nchi yetu. (*Makofi*)

Pia kuna madini, madini yanayotoka katika nchi hii yanatoka katika Kanda ya Magharibi na Ziwa. Lakini hebu angalia utalii, kuna utalii kule Katavi, Gombe lakini Kanda hii imesahaulika haina barabara za kutosha kuunganisha mawasiliano katika Kanda hiyo ya Ziwa, hakuna umeme, *grid* ya Taifa imepita kwa muda mrefu miaka ya themanini lakini hakuna umeme unaopita sambamba na *grid* ya Taifa kuvipatia Vijiji ambavyo vinapitiwa na *grid* ya Taifa umeme wa kutosha kwa ajili ya kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia kuhusu reli. Reli imejengwa na Mjerumani, bado haiwezi kutosha kufanya kazi ya kuleta maendeleo. Kuhusu usafiri wa anga, hatuna viwanja vya ndege, kuna uwanja wa ndege pale Mwanza, unaweza kubeba samaki wa kutosha wengi kabisa kwa ajili ya kupeleka nje, masoko ya Jumuiya ya Ulaya na pengine, lakini bado haujatosheleza hasa *terminal* hakuna na uwanja wa ndege wa Kigoma na Tabora hakuna. Kwa hiyo mimi nilikuwa napendekeza kwamba Serikali ya Awamu ya Nne iweze kuangalia yafuatayo:-

Kwanza, barabara ya kutoka Mwanza-Shinyanga-Tabora mpaka Mbeya ijengwe kwa kiwango cha lami. Barabara ya kutoka Manyoni-Itigi-Tabora-Kigoma ijengwe kwa kiwango cha lami. Barabara ya kutoka Sikonge-Ipole-Rukwa-na yenyewe ijengwe kwa lami na barabara hizi zikijengwa zinaweza kufanya mambo mawili. Jambo la kwanza, zitaibua uchumi lakini tunaweza vile vile kushika uchumi wa kibiashara na nchi zile zinazotuzunguka. Ipo nchi ya *Congo DRC* kuna mizigo mingi sana ya kufanya kazi pale na pia zipo nchi za Rwanda, Burundi, Zambia. Sasa hivi wananchi wa Bukoba wakitaka kusafiri anapita Uganda, Kenya, Arusha ndio anakuja Dar es Salaam, ni aibu kwa Serikali ya Awamu ya Nne kuendelea hivi, naomba tubadilishe tujenge barabara hizi kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, naomba tuwekeze vya kutosha kuimarisha reli na hasa kuimarisha bandari za Kigoma pamoja na ya Mwanza. Pale Kigoma peke yake kuna biashara nzuri sana kutoka *DRC Congo,* kama tungeweza kuibua ile bandari ya Kigoma tungeweza kubeba mizigo ya kutosha kutoka pale *DRC Congo.* Leo hii kuna mawazo ya

kujenga reli kuanzia Isaka iende mpaka Rwanda, ukishajenga ile reli kwenda mpaka Rwanda (Kigali) maana yake unachukua mizigo ya *Congo* inapitia Kigali, kwa nini tusifanye sisi biashara moja kwa moja kupitia bandari yetu ya Kigoma? Naomba hili tulichukulie kwa umakini kuhakikisha kwamba tunaibua uchumi kwa ajili ya faida ya Watanzania na wananchi wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, la tatu ni kuhusu umeme. Umeme katika maeneo hayo ukiangalia Mkoa wa Rukwa, Kigoma na Tabora ni tatizo. Mkoa wa Tabora una *grid* ya Taifa lakini katika maeneo mengi hakuna umeme. Angalia Mkoa wa Shinyanga, Singida na Mwanza, katika maeneo mengi ambayo *grid* ya Taifa imepita, hakuna umeme hata wa kiwango kidogo ambao unaweza kutumika kwa wananchi wa kawaida lakini *grid* ya Taifa imepita juu. Ziwepo hatua za makusudi kuhakikisha pale ambapo *grid* ya Taifa imepita basi Vijiji vile vyote vinapatiwa umeme na hili ni suala ambalo kwa kweli lifanyike mara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri wa anga, sio vibaya kuwa na viwanja viwili vitatu katika nchi moja vya Kimataifa. Ni nzuri kabisa, pale Uingereza wana viwanja viwili vya Kimataifa, ni vizuri tu, kwa nini sisi tusiwe na kiwanja pale Kigoma cha Kimataifa, tusiwe na kiwanja cha Kimataifa pale Mwanza na Tabora pia kwani ni vizuri kwa ajili ya kufanya biashara ya kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Spika, la nne, nilikuwa nataka kusema juu ya madini ambayo yameanza kuibuliwa katika maeneo yetu ya Kanda ya Magharibi, kwa kweli katika Mikataba ambayo haifai ni hii ya madini. Mimi nimekuwa miongoni mwa watu ambao nimekataa tangu mwanzo, nimebisha, nikajaribu kuleta hata hoja binafsi, nikajaribu kuleta Muswada binafsi na kutumia kila njia ili Mikataba hii iweze kupitiwa. Naomba Serikali ya Awamu ya Nne, tunaipenda, tunawaamini, leteni Mikataba ya namna hii tuweze kuizungumza, kuijadili kwa pamoja na iweze kuleta maendeleo hasa katika maeneo ambayo yanatoka madini mbalimbali. Angalia *impact* ya madini katika maeneo hayo. Eneo lote la Magharibi pale kunatoka madini, angalia Shinyanga ilivyo, Nzega ilivyo na Mwanza ilivyo haifanani na maeneo ya madini. Pale wanazoa mabilioni ya fedha, lakini ukitoka mita mia moja peke yake unakuta watu wanaishi maisha duni, maskini na ya kilala hoi kabisa. Katika suala hili naomba tubadilike, Halmashauri zetu za Wilaya ziweze kupata tozo ambalo litasaidia wananchi wetu kuweza kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nchi yetu haina *National Carrier, Air* Tanzania imekufa na inakwenda kufa, tumeingia Mkataba ambao hautufai kwa ajili ya Shirika la Ndege, naomba Awamu ya Nne ianze upya kuangalia ni kitu gani ili tuweze kuliamsha Shirika la Ndege la Tanzania. Kwa sasa hatuna Shirika la Ndege la Taifa.

Naomba sana Waziri wa Miundombinu ajitahidi katika hili. Waziri Mkuu ni mtu ambaye ana staili za aina yake, aingie akafufue *Air* Tanzania ili tuwe na *National Carrier*, hatuwezi kuwa na nchi ambayo haina *National Carrier*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwashukuru na kuwatakia kila la kheri na niwape pole Wapinzani kwa kukosa viti vingi, fanyeni tu polepole ipo siku baada ya karne moja mnaweza na ninyi kurudi na kuwa Chama Tawala.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi ya kuweza kuzungumza kwa mara ya kwanza katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutujalia uzima pamoja na afya hatimaye tumekutana hapa Bungeni kwa ajili ya kutetea mambo ya maslahi ya wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii pia kumpongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa ushindi mkubwa kabisa alioupata baada ya kuchaguliwa na wananchi katika zoezi ambalo liliendeshwa Desemba 14, 2005. Pia napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Waziri Mkuu na pia kumpongeza Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nachukua pia nafasi hii kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika kwa ushindi mkubwa kabisa ambao uliupata hapa Bungeni baada ya kupigiwa kura nyingi kabisa na Wabunge bila kumsahau Naibu Spika mama yetu Mheshimiwa Anne Makinda.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mawaziri, Manaibu Waziri pamoja na Wabunge wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao wamepewa nafasi kubwa kabisa, heshima kubwa kabisa na wananchi wa Majimbo yao kwa ajili ya kuja kuwawakilisha katika Bunge hili Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais ningependa kuwashukuru kwa dhati kabisa wajumbe wa Baraza Kuu la Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi Taifa kwa kuweza kunipigia kura nyingi ambazo zimeniwezesha mimi kuingia hapa ndani kuja kuwatetea vijana pamoja na Watanzania kwa ujumla. Naanza kwa kusema naiunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa asilimia zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mambo yapo mengi sana katika hotuba hii lakini nitajaribu kuzungumzia mambo machache. Najua Mheshimiwa Rais tayari amekwishatoa mwongozo, kilichobaki sasa hivi ni utekelezaji tu na naamini Askari wake wa Miavuli hawatomwangusha pamoja na sisi Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikianza na suala la afya nasikitika sana na inaniuma sana kuona mpaka leo nchi yetu ya Tanzania inakosa hospitali ama kitengo cha kutibu ugonjwa wa moyo. Nashindwa kuelewa tatizo ni nini, kwamba vifaa hakuna ama wataalam hatuna au ni nini ambacho kinaendelea hapo.

Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi sana kuwapeleka wananchi wanaosumbuliwa na ugonjwa wa moyo India. Sisi kama Watanzania kweli hatuwezi kujenga hospitali hapa nchini kwetu, Serikali ya Tanzania haiwezi kujenga hospitali ambayo inaweza kutibu ugonjwa wa moyo na kama labda hakuna fedha mbona hospitali zipo.

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ni kubwa sana na ina majengo makubwa sana, hivi kweli imeshindikana kutenga kitengo tu kwa ajili ya kutibu ugonjwa wa moyo au tatizo liko wapi?

Naiomba Serikali ya Awamu ya Nne, chonde chonde, kwa sababu wanaoathirika sana ni wananchi wetu na ni wale ambao wana hali ya chini. Wengi wenye uwezo wanaweza kukimbilia nje na kwenda kutibiwa lakini tuliangalie kwa umakini sana hili tatizo kwa sababu linawamaliza sana wananchi, kila siku watoto wenye matatizo hayo wanazidi kuzaliwa, Serikali ya Awamu ya Nne kupitia Wizara husika naomba iweze kujenga kituo maalum cha kutibu ugonjwa wa moyo. Yapo mashirika ya watu binafsi ambao baadhi wamejitolea kuwa na hospitali ya moyo, basi kama Serikali imeshindwa kabisa ningeomba itoe ushirikiano kwa wazawa, wazalendo ambao wameweza kujenga vituo vya kutibu ugonjwa wa moyo lakini wamekuwa hawapati ushirikiano kutoka kwa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la pili ambalo ningependa kulizungumzia ni elimu. Katika hotuba ya Mheshimiwa Rais amesema kwamba atahakikisha anatokomeza umaskini, ujinga, maradhi kwa ari mpya, nguvu mpya, kasi mpya na maisha bora kwa kila Mtanzania yatawezekana. Kama kweli maisha bora kwa kila Mtanzania yatawezekana, basi mimi ningeomba kukumbusha tu katika upande wa walemavu. Walemavu naona kama wamesahaulika kidogo hata kama juhudi zipo lakini si kubwa sana, basi ningeomba ziongezwe kwa sababu sawa wana ulemavu lakini wapo ambao pia tunawategemea na wanaweza kufanya kazi zingine ambazo sisi pia binadamu wa kawaida tunaweza kufanya kwa sababu wengine wana ulemavu tu wa macho, mkono au wa mguu lakini viungo vingine vinafanya kazi kama kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia shule za watoto wenye matatizo ya kutosikia. Nchini yetu ya Tanzania ina Mikoa ishirini na sita, lakini shule ambazo zinafundisha watoto wasiosikia hazizidi shule tano. Tatizo liko wapi. Watoto wenye matatizo wanazidi kuzaliwa kila siku, haina maana kwamba walizaliwa mwaka fulani tu hawataendelea kuzaliwa, bado wanaendelea kuzaliwa. Shule zipo chache kiasi kwamba wazazi wakipeleka watoto shule wanaambiwa mwaka huu shule imejaa njoo mwaka ujao na tunafahamu kabisa watoto wasiosikia huwezi kuwachanganya katika darasa moja na watoto wengine ambao wanasikia. Kama kweli ni maisha bora kwa kila Mtanzania basi ningeomba Serikali ya Awamu ya Nne itilie mkazo katika upande huu wa elimu kwa watoto walemavu hasa wasiosikia kwa kuweza kuwajengea shule zaidi na pia sisi wananchi ambao tuna uwezo na mashirika binafsi, natoa ombi tujitolee kujenga shule hizi ili kuweza kuisaidia Serikali yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho ningependa kuzungumzia katika upande huo huo wa elimu ni kufutwa kwa masomo ya biashara kwa kidato cha kwanza mpaka cha nne. Pia kidato cha tano mpaka cha sita nasikia masomo haya kwa sasa hayafundishwi, tatizo liko wapi? Tunafuta masomo wakati kuna walimu ambao walisomea kabisa, hiyo ndiyo fani yao ambao wametoka vyuoni kwa ajili ya kwenda kufundisha masomo ya biashara.

Leo walimu watakaa hawana kazi kwa sababu hawawezi kwenda kufundisha masomo ya sayansi tayari alishachukua masomo ya biashara kuanzia kidato cha tatu pale ambapo ndio tunaanza kuchagua masomo kwamba uende mchepuo upi, amechagua na amesoma biashara mpaka kidato cha nne, kaenda kidato cha tano na cha sita kaendelea kusomea biashara, wengine wamekwenda hadi Vyuo Vikuu wameendelea kusomea biashara, wana utaalam wa biashara zaidi kwa ajili ya kuwafundisha wanafunzi.

Leo unapofuta masomo haya unakuwa umeharibu pia ajira kwa walimu hawa kwa sababu sidhani kama watakwenda kufundisha masomo ya sayansi, watafundisha nini na wakati hawajasoma? Pia hawawezi kufundisha hayo masomo mengine kwa sababu hawajasoma masomo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba Serikali ijaribu kuangalia upya suala hili na tukumbuke kuwa masomo haya ya biashara yanasaidia katika kutoa ajira kwa vijana na Serikali pia ya awamu ya Nne imesema itaangalia kwa undani zaidi suala hili la ajira kwa vijana katika kuhakikisha vijana wanapatiwa ajira. Mojawapo nadhani ni hii ya kusoma masomo ya biashara ambapo unapokuwa umemaliza angalau kidato cha nne kama umeshindwa kuendelea unakuwa umeshapata mwongozo wa biashara, unaweza kujiajiri mwenyewe lakini kwa kukosa elimu hii vijana wengi sana wataathirika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa muundo mpya wa Wizara ya Vijana ambayo ameiweka sambamba kabisa na ajira. Nilikuwa naomba Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana msituangushe vijana tunawategemea sana. Lakini pia vijana tusiiangushe Wizara hii ni watu ambao tumekuwa hatuaminiki, tunaonekana kama ni watu wa kucheza cheza tu saa zote, naomba tuwe makini.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ya Kazi, Ajira na Vijana ijaribu kutenga japo fungu kwa vijana wote kama ni Mijini na Vijijini kwa kuwapa vitendea kazi ambavyo vitawawezesha wao kujiajiri wenyewe bila hata kwenda kwenye makampuni au kutafuta kazi kwa sababu masharti pia yamekuwa magumu sana. Ukienda kuomba kazi unaambiwa mpaka uwe na uzoefu wa miaka mitano, kijana ametoka chuoni, hana uzoefu wowote, hiki kinakuwa ni kikwazo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaomba Wizara ya Kazi, Ajira na Vijana mliangalie hilo na kama mngeweza kama kweli vijana wapo tayari kulima, basi wasaidiwe kupewa mbegu, majembe au kuwapa vifaa ambavyo vitawasaidia wao wenyewe kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, ninayo mengi lakini kwa kuzingatia muda, mwisho kabisa ningependa kuchukua nafasi hii kuipongeza Televisheni ya Taifa (TVT) kwa kuweza kuonyesha mashindano ya mpira wa miguu wa kombe la Afrika.

Naamini hii ni juhudi ama jitihada ya Serikali ya Awamu ya Nne katika kuendeleza michezo kwani ni televisheni pekee ambayo inaonyesha mashindano haya bure na ni televisheni inayomilikiwa na Serikali yaani iko chini ya Serikali, kwa hiyo hii itatoa changamoto kwa vijana wetu kuweza kuangalia na wao kujifunza na kuiandaa nchi yetu kuwa nchi nzuri yenye vijana wazuri ambao watashiriki katika michezo.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya hotuba ya Rais. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mkumbuke kwamba kengele ile inayokuashiria kwamba bado dakika tatu, basi ni vizuri kuanza kumaliza, sipendi sana kuwaingia kati. Mheshimiwa Aggrey Mwanri atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge.

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu kwa hoja iliyoletwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu hotuba ya Rais wetu mpendwa.

Mheshimiwa Spika, tulipokuwa kwenye semina nilitoa pongezi zangu kwa wale wote ambao walipata nyadhifa mbalimbali na kwa vile umetubana kidogo kwa sababu za msingi, nitaomba nijielekeze moja kwa moja kwenye hotuba ya Rais.

Nataka niseme kwamba ukitafuta uzito *strength* ya hotuba ya Rais aliyoitoa, iko katika maeneo makubwa matatu.

La kwanza, ni namna ambavyo hotuba ya Rais inajaribu kujibu matumaini na matarajio ya Watanzania, Rais huyu alipitishwa na mamilioni ya watu, milioni tisa, wamempa dhamana ile na aliposimama mbele yetu hapa *it is my opinion kama Member of Parliament* kwamba niliona waziwazi kwamba Rais wetu akijibu matumaini na matarajio ya Watanzania, hilo la kwanza *strength* yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *strength* ya pili ambayo niliiona mimi ni kwamba Rais alijaribu kuangalia *margin in a historically perspective*, ukiangalia mambo *in a historical perspective you are trying to be scientific*. Huwezi kushindwa, ukishaangalia mambo kwa mpangilio wa kihistoria kwa maana yake historia ndio binadamu, huwezi kutetereka hata kama unafanya makosa *history* itakulinda, itakutunza na ndicho alichofanya.

Aliangalia kipindi cha Baba wa Taifa, akaangalia kipindi cha Ali Hassan Mwinyi, Rais wetu Mstaatu na akaangalia kipindi cha Mheshimiwa Benjamin Mkapa, vipindi hivi vyote vitatu akaviangalia pale na yale mazuri yote na makubwa yaliyofanywa na Awamu hizo Tatu akaya-*articulate*, akayaingiza katika mipango inayoingia katika Awamu ya Nne. Nguvu yake ya pili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nguvu ya tatu au uzito wa hotuba ile ni *order or presentation*. Rais wetu alipokaa pale mbele tulimwona akiwa *at home*, ame-*articulate issues* vizuri anazo *notice* zake, anayo hotuba yake pale, lakini wale tuliokuwa tunamtazama, tulimwona hapati tabu katika kueleza yale anayoyasikia.

Maeneo hayo makubwa matatu ndiyo naamini kwamba yamemfanya Rais awe na uzito. Ungeweza ukageuza ukasema acha hayo. Ungeweza ukasema mimi hata hotuba sikuisikia. Lakini sikiliza hata *reaction* ya Watanzania wa aina mbalimbali. Hata ndugu zetu wanaotoka katika *opposition* kwa sababu ya hiyo nguvu tuliyoieleza hapa. Unamwona Rais anaonekana amefanya kazi kubwa. Hayo ndio maudhui ya hotuba yenyewe. Angalia anavyokwenda mbele. Ukimaliza kazi ile umekwenda kwenye Mapinduzi unataka kufanya kazi ya kuendeleza nchi, kazi ya kwanza unayofanya ni kuweka pumzi mpya ndani ya *system* yako. Ni kutoa majukumu mapya. Alichofanya Rais baada ya pale tulichokiona ni kupanga kada katika safu mbalimbali na akapanga Baraza la Mawaziri na sisi wote tumeliona Baraza hili linavyofanya kazi vizuri.

Nataka niseme *I am impressed* yaani nimesikiliza siku mbili au tatu nikasikiliza jinsi Manaibu Mawaziri na Mawaziri wanavyojibu maswali hapa ndani *I am impressed*. Unaona hata yale makosa madogo madogo ambayo yalisemwa yasahihishwe baada ya siku mbili tu unaona wote wamesahihisha. Pale ukiangalia unaona matumaini kule mbele ya safari unaona kwamba tumeshinda. Clinton anapoingia kwenye madaraka ulipomwona Clinton ameingia pale la kwanza unaloangalia, unaangalia jinsi alivyopanga safu yake vizuri. Unaangalia siku mia moja za Clinton. Safu imepangwa vizuri na mimi kama *Member of Parliament* ninayetoka Siha nataka niliambie Baraza la Mawaziri nitawapa kila aina ya msaada ili mfanye kazi yenu vizuri. *I am proud,* mimi niko proud najisikia kwamba kweli tunao watu ambao tunaweza tukafanya nao kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, kipindi hiki kifupi hatujafikisha siku mia moja tumeona vitu vikubwa vinafanyika katika nchi hii. Rais wetu anakwenda mpaka katika masoko ya Kariakoo, Tandale. Anaondoka anakwenda na huyu ni mtu anayetokana na walalahoi, ni mtu anayetokana na wanyonge kwa hiyo lazima aji-*identify now* na ndicho tulichokiona. Tumemwona Rais amekwenda pale. Rais Samora Machel wa Msumbiji alijaribu kueleza maana ya *revolution*. Akasema Mapinduzi ni kitendo chochote ambacho kinawaletea manufaa watu kwa muda mfupi. Ukisema unaleta Mapinduzi unasema leo nataka tule ubwabwa ukasema ubwabwa huu tutakula baada ya miaka miwili usizungumze *according to* Samora Machel. Kama tutakula ubwabwa tule leo jioni, asubuhi tumekula ubwabwa. Kama tutakunywa maziwa tunywe leo, tunywe kesho asubuhi. Lakini anaweka *conditions* zake Samora Machel anasema ili uweze kuleta Mapinduzi lazima uwe tayari kufanya kazi muda wa ziada.

Ukisema hivi mimi ni Meneja wa Kampuni. Mimi ni Waziri ni *Deputy Minister*, mimi ni Mbunge saa 9.30 *sharp on the dot* imefika hapa. Kazi imekwisha mpaka kesho asubuhi *you never bring revolution* huwezi. Ni mpaka unapofika mahali uko kufanya kazi muda wa ziada ndipo utakapoleta Mapinduzi. Ukisema mimi daktari natibu mpaka

saa 9.30, mimi ni Waziri saa 9.30 imefika nimemaliza, mimi ni Rais saa 9.30 imefika imekwisha *you will never according to* Samora Machel sio mimi, *you will never bring revolution*. Rais wetu yuko tayari kufanya kazi muda wa ziada unamwona anafanya kazi anakwenda anashughulika. Tukifika mahali tukasema leo ni sikukuu ya Pasaka, X-mas, leo ni Maulid kwa hiyo hatuwezi kwenda kazini *we shall never bring revolution in Tanzania*. Tunataka ku-*deal* na majambazi *perpendicularly* kushoto kulia na katikati lazima uwe tayari kufanya kazi muda wa ziada. Ukifanya hivyo uta-*bring revolution* na ndicho ambacho nimekiona Rais wetu anafanya. Utaleta *revolution* vinginevyo hutaleta Mapinduzi utakwenda utazungumza. Sasa unafanya nini? Haya yote tunayozungumza hapa hayana maana kama hayana miguu yake katika uchumi.

Bwana mmoja anaitwa Carl Max napenda sana kumnukuu anasema *"Always the economic base determine the super structure"*. Haya yanayozungumzwa hapa juu kama hayana miguu yake hapa chini haya yanayozungumzwa hapa unapoteza muda. Ni mpaka kuweko a one to one fuction kati ya linalozungumzwa hapa na *economic base* ambayo ume *create* hapa. Utazungumza habari ya kusomesha watoto, habari ya reli, barabara, majengo kama unayo *a strong economic base*. *Outside that* hii yote ni *huller balloon* unazungumza. Ni ya mwanzo ya mwisho? *(Kicheko).* Ya mwanzo.

Mheshimiwa Spika, ahsante nilikuwa nimeogopa kweli nitachukua *item* moja tu. Unasema Watanzania wana njaa unataka kuwalisha Watanzania huwezi ukalisha Watanzania kwa kusema peleka chakula. Unamwezesha Mtanzania mmoja mmoja kulima chakula chake na kujilisha ndiyo Tanzania imejilisha. Lazima uanzie hapo. Ukisema tunataka tuwasaidie Watanzania tuwapelekee chakula utawapata baada ya miezi miwili au mitatu *it will get out of him*. Ni mpaka useme hivi niwawezeshe Watanzania kuzalisha chakula kidogo kidogo. Acha hii *mechanized agriculture* tusiende huko Watanzania 87 *per cent* inaishi kwa kulishwa kwa jembe la mkono. Watu walichukua mbegu wanarusha hivi, watu wanafanya hivi na nini lakini wanaishi kwa hilo. Kama 87 *per cent* ndiyo inayowalisha Watanzania muwawezeshe. Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa Kilimanjaro alizungumza habari ya *Kilimanjaro Investments Centre*. Tuliambiwa hapa pesa zitatoka zitasaidia jambo hili. Ametuambia yeye mwenyewe mpaka tunamaliza hapa bajeti tunaondoka Bunge linavunjwa shilingi bilioni moja zilizokuwa zimetamkwa hapa hazijaenda. Kwa hiyo tutazungumza tutasema tutapeleka vyakula SGR watafanya njaa ikishaingia mahali habari imekwisha. Nataka ku-*urge* nini tulisema kwamba pembejeo, bei ya mbolea tutapeleka kwa ruzuku hatujafanya hivyo. Tunakwenda hapa njaa itakwisha tutamwomba Mungu mvua itakuja itanyesha na kadhalika. Lazima tufike mahali tuwawezeshe Watanzania.

La pili Rais anazungumzia habari hapa ya misitu, habari ya mazingira. Mazingira *by definition* ni maji jumlisha na kuotesha miti kwisha. Nyuki ni matokeo, utalii ni matokeo. Ukisema hapa Mkoa wa Kilimanjaro utapanda miti,

Mkoa wa Ruvuma usipopanda miti *it is useless*. Ukisema Tanzania tutapanda miti Kenya hawapandi miti *it is useless.* Lazima ufike mahali useme kwamba uweke utaratibu ambao sisi wote kwa pamoja tutafanya kazi ya kupanda miti kuhakikisha kwamba tunahifadhi maji. Hiki kitu tunazungumza hapa namwona Mzee wa Mazingira

kule Prof. Mwandosya anapiga Makofi. Mimi nakuomba nisaidie katika Wilaya yangu mpya ya Siha. Serikali inisaidie tupande miti lakini Siha tu ikipanda miti Tanzania nzima isipopanda miti *you are wasting your time.* Haya ni mambo ya *principles* haya ni mambo ambayo unatakiwa uangalie kanuni zinazotawala. Yota yaliyozungumzwa katika hotuba ya Rais ni kwa kiasi gani wananchi sisi Watanzania tunayageuza yawe ni kanuni amri ya siku. Tutapiga hapa tutamaliza baada ya muda mwaka mmoja umemalizika utakuta *business as usual*. Tunarudi pale pale *it is my conviction* kwa aina ya Rais tuliyompata hapa. Sisi Watanzania tukisimame imara tukagawana majukumu tukapeana pumzi mpya kila mtu akafanye kazi yake vizuri. Baada ya miaka mitano tutajiuliza tulikuwa wapi kwa nini hatukufanya mambo yote. Kila mtu ajitafutie kipande chake cha nchi akakitumikie. Tuchukue haya yote yaliyozungumzwa hapa tukafanye lakini tujue kwamba tunatakiwa kufanya kazi ya ziada baada ya hapo tutaleta Mapinduzi katika Tanzania. Kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Siha napenda kuunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Rais wetu Jakaya Kikwete. Nataka niseme kwamba namwunga mkono Mheshimiwa Waziri Mkuu na wote nawaunga mkono.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ningependa kutumia nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wangu, wapiga kura wa Makete ambao ndio wameniwezesha kuwa katika Bunge lako hili Tukufu.

Baada ya hapo naomba niendelee kutoa mchango kwenye hotuba ya Rais kama ifuatavyo. Sehemu ya kwanza ningependa kuchangia katika sehemu hii ya afya. Kwanza niwapongeze wale wote na kuwashukuru ambao wameelekeza juhudi na misaada mingi katika kutatua tatizo la UKIMWI ambalo linaikabili Wilaya yangu au jimbo langu la Makete. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba basi kusema yafuatayo. Toka janga hili limetokea Wilayani kwangu juhudi zote zimeelekezwa katika kutoa misaada, kutoa elimu lakini hakuna tathmini hata moja ambayo imefanywa ama na Serikali au *NGO* yoyote ile. Kwa hiyo nina wasi wasi takwimu zinazotolewa zinaweza kuwa hazielezi hali halisi ya maambukizi au watoto yatima au wajane waliopo katika jimbo langu la Makete. Kwa hiyo naomba kwa Serikali na *NGO's* kwamba wasikimbilie tu kwenda kutusaidia misaada basi tunaomba sasa wajikite katika kufanya utafiti ambao utaainisha ni sehemu zipi na ni watoto yatima wangapi walioathirika ili misaada iweze kuwafikia wale wanaohusika. Nasema hivi kwa sababu upo usemi kwamba "Ni afadhali uwe na jibu ambalo sio sahihi lakini tatizo uwe umelielewa, kuliko ukawa na majibu mia moja mazuri wakati tatizo hulielewi". Huo ni mchango wangu katika sehemu hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili nilikuwa nadhani sasa hivi ni muda wa muafaka kwa Wizara ya Afya kuona namna ya kuweza kuwakilisha Muswada katika Bunge ambao utawezesha watu wote kujua afya zao. Tuangalie wenzetu wa nchi zingine kwamba suala la kujua afya yako ni la lazima na kwa hapa Afrika nadhani uko mfano kama Botswana.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili nataka kuchangia kuhusu barabara. Mtazamo wangu katika hili ni tofauti kidogo na wenzangu. Kwamba ni kweli tunahitaji barabara zijengwe lakini mimi nadhani tujifunze kutoka kwenye historia. Tumepata uhuru mwaka 1961 barabara za Makete zote zinazoingia Makete toka Njombe mpaka Makete, Mufumbi mpaka Makete na kutoka Mbeya kupitia Kikondo mpaka Makete mpaka leo miaka 44 hazipitiki. Serikali inapeleka fedha kila mwaka nadhani kwamba hizo fedha wananchi wangeamua kuzidunduliza kwa miaka yote hii leo wangejenga barabara ya lami. Nadhani tunatakiwa tuangalie utaalamu unaotumika kujenga zile barabara. Kwa sababu haiwezekani kufikia leo hii miaka 44 barabara hiyo iwe imeshindikana kwa fedha zote ambazo Serikali inapeleka huko. Hivi ninapoongea nimeondoka baadhi ya sehemu hazipitiki na hasa wakati wa masika Makete sio rahisi kuifikia na kwa maana hiyo matatizo ya UKIMWI huwezi kuyatatua, huwezi kupeleka huduma hakuna kinachoweza kuwezekana.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa nini haya mashimo yashindwe kutengenezwa kwa utaalamu na utaalamu tunao na fedha zipo. Ama mvua za Makete zimezidi taaluma ya Watanzania ama vipi. Kwa hiyo hapa tunaomba wale wanaofanya maamuzi kwanza wasifanyie maamuzi wakiwa wamekaa Ofisini Mjini Iringa. Maamuzi yakafanyike kwenye *Site* wakiwa na mifano halisi na kwamba hapa panahitaji teknolojia gani ili hii barabara iweze kutengenezwa. Kwa sababu hili linasababisha biashara nzuri ya utalii ya Makete isiweze kufikiwa na hivyo kupunguza pato la Taifa. Ninao mfano tuna hifadhi zetu nzuri za Kitulo zenye maua mazuri, tuna shamba la ng'ombe Kitulo kwa hiyo nani atakwenda kuwekeza Makete kama barabara haiwezi kufikika. Lakini vile vile sasa hivi kinajengwa Kiwanja cha Kimataifa Mbeya ambacho nadhani tungefaidika sana kuongeza pato la Serikali kama tungeimarisha barabara zinazoingia kwenye hifadhi hizi za Kitulo, kwenye milima ya Livingstone ili kuimarisha utalii.

Mheshimiwa Spika, hili la barabara pia Mheshimiwa Rais wakati wa Kampeni zake aliahidi kwamba atalifanyia kazi kuona barabara kutoka Njombe mpaka Mporoto kupitia Makete inakamilishwa kwa uhakika. Sehemu ya tatu ya mchango wangu ni usalama wa raia. Hapa nina mapendekezo mawili. La kwanza wenzangu wote nawaunga mkono kwa yale yote waliyoyapendekeza kwamba tuwawezeshe Polisi. Lakini mimi nadhani tuwawezeshe na wananchi ili wasaidie Polisi kuleta usalama, tuwawezeshe vipi? Naomba basi juhudi za dharura za lile zoezi ambalo Serikali ilikuwa inaandaa la kuandaa vitambulisho lifanyike ili wananchi wawe na vitambulisho vitatusaidia sana kujua kwamba tunaye nani na anamtembelea nani.

Lakini la pili katika hili basi umefika muda, nimepita pita hapa Dodoma nikaangalia *plan* ya mji inapendeza kwa sababu umejengwa kwa *plan* za kisasa. Kwa hiyo ninaamini hapo baadaye itakapokuwa imekamilika itakuwa rahisi sana kuwakamata vibaka na hawa majambazi itakuwa rahisi sana hata huduma za afya kufika kwenye hizo sehemu. Lakini nenda Dar es Salaam angalia Manzese nadhani aina ya *plan* ya mji wetu inaficha sana majambazi. Kwa hiyo nadhani ni vizuri *master plan* zipitiwe upya na yale maeneo yaelezwe kabisa kwamba itabidi yabomolewe baadaye na watu waweze kujenga nyumba ambazo zinaweza zikapitisha hata huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa nne ni kuhusu kujenga utaifa. Hapa mchango wangu nadhani ni mdogo lakini hapa tuelekeze katika juhudi namna gani ya kuwalea vijana wetu. Kwa sababu ukiwalea vijana vizuri ndio unaweza ukaona kwamba baadaye wanakuwa wazalendo na wakalinda nchi yao vizuri. Mfano ni katika mazingira leo hii tunazo *beach* zetu Dar es Salaam ambazo zinatuingizia fedha za kigeni kwa nini tusiwajenge watoto wetu kama wale wa Shule za Sekondari tukaandaa kipindi ambacho wanachukuliwa na mabasi na kwenda kufanya usafi kwenye mazingira yale na hivyo kuweza baadaye kumkemea yoyote anayetupa karatasi ya nailoni kwenye dirisha la gari kwa sababu atakuwa na uchungu wa mazingira. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tano ni ajira hapa mimi naiangalia ajira kama *Global Agenda of Employment.* Naangalia ajira kama sarafu upande mwingine elimu kwa wote upande mwingine kazi kwa wote. Lakini vile vile naangalia hizi ajira milioni moja ambazo tunazitegemea zitakuwepo katika kipindi hiki. Nadhani hapa kinachotakiwa ni kuwaandaa vijana waweze kushindania zile ajira na kuzipata. Hapa nasema kwa sababu wengi tumekuwa na dhana kwamba wanaajiri wageni, nadhani mgeni yoyote anapokuja kuwekeza hapa lengo lake kubwa inawezekana anasema anataka kuwasaidia muondoe umaskini lakini zile *vision* alizonazo kule *South Africa* zinasema unakwenda kutafuta faida upate fedha. Kwa hiyo anapokuja hapa atamwajiri yule ambaye anajua kwamba atamfanyia kazi vizuri. Kwa hiyo mimi naomba hapa tuwaandae vijana wawe na *skills, knowledge* na *competence* ambazo zinaweza kuwafanya wakashindana kwenye hilo soko na baadaye kuhakikisha kwamba wageni wanaona upo umuhimu wa kutuajiri sisi wenyewe tufanye hizo kazi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni suala la elimu. Hapa naomba tu kwa kuwa kuna hiyo *proposal* ya kuwa na *double sessions* katika Sekondari basi ni muafaka vile vile tuwe na *double sessions* katika Vyuo vya Elimu ya Taifa ambavyo vinafundisha walimu. Nadhani hii itasaidia sana kuongeza Walimu ambao ndio kero kubwa ya shule zetu za Sekondari ama za Msingi. Hapa pia nitoe tu nung'uniko langu moja kwamba tuna Chuo cha Elimu ya Taifa Tandala lakini utashangaa kuona kwamba Shule za Makete ndizo zenye Walimu wachache na wakati nadhani kwamba wananchi ambao wangefaidika ni wale ambaowapo karibu na hiyo miradi.

Mheshimiwa Spika, mwisho michezo. Nadhani sasa ni muda muafaka tuichukulie michezo kama somo na kama elimu ambayo inatakiwa kusomewa. Kwa hiyo hapa namwomba Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu ikiwezekana kutumia vyuo vyetu basi kuwe na kitengo ambacho kinaweza kikaanzisha Shahada ya Michezo. Watu wasomee wapate digrii za michezo wapate digrii za miziki ili tuweze kuhimili huu ushindani wa michezo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naomba nikumbushe kwamba wakati wa Kampeni zake Mheshimiwa Rais ambaye alikuwa ni mgombea wa CCM aliahidi vile vile kwamba atahakikisha wananchi wangu wa Tandala wanapata umeme. Tandala mpaka Makete ni kilomita 30. Tandala kuna Chuo cha Elimu ya Taifa, Tandala kuna Hospitali

ya Ikonda ambayo inatibu Watanzania wengi kutoka sehemu mbalimbali. Tandala kuna Sekondari nadhani wanaohusika wakiliandika ili basi liweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, na mimi naomba nichukue nafasi hii kwanza kabisa niwashukuru wananchi wa Jimbo langu la uchaguzi la Mbozi Mashariki ambao ndio kwa kweli walioniwezesha kunifikisha Bungeni hapa leo hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwashukuru wananchi wangu wa Wilaya ya Mbozi naomba pia niwashukuru na wale waliokuwa wagombea wenzangu kupitia Chama cha Mapinduzi ambao kwa kweli baada ya mimi kushinda kwenye mchakato wa kura za maoni wote walikubali hakuna ambaye alilalamika. Napenda kuwashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naomba pia nichukue nafasi hii kama walivyosema wenzangu na mimi niwashukuru, wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge letu Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini pia nimpongeze Naibu Spika kwa kuchaguliwa. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu lakini zaidi ya yote tumpongeze sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kushinda kwa kura nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nijielekeze moja kwa moja kwenye mchango wangu unaotokana na hotuba ya Mheshimiwa Rais. Jimbo langu mimi ni jimbo ningesema la wakulima na kwa maana hiyo mambo mengi nitakayozungumza yatalihusu sana jimbo langu. La kwanza naomba nizungumzie suala la kilimo. Wilaya ya Mbozi kwa ujumla ni moja ya Wilaya ambazo zinazalisha sana katika nchi hii. Tunapozungumza suala la njaa Wilaya ya Mbozi ina matatizo kidogo katika baadhi ya maeneo. Lakini matatizo haya mimi naweza kusema inawezekana kabisa yanasababishwa na Serikali yenyewe. Naomba nitoe mfano.

Mwaka jana Serikali ilikuwa inasambaza mbolea katika Wilaya na Mikoa mbalimbali katika nchi hii. Wilaya ya Mbozi ilihitaji jumla ya tani 38,015 za mbolea lakini inasikitisha na mtu mwingine anaweza kusema huu ni utani Serikali imepeleka tani 6,112 tu, tunategemea wananchi hawa walime kweli!! Tunategemea wananchi hawa wazalishe. Leo tunalia njaa na ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge wengine, waliotangulia kuzungumza wamesema Serikali haiko *serious* na suala zima la kilimo.

Mheshimiwa Rais kwenye hotuba yake amezungumza kabisa amesema tunatambua kwamba kilimo ndio uti wa mgongo wa Taifa na wote ndio tunaelewa hivyo. Zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wanaajiriwa kwenye sekta ya kilimo kwenye Jimbo langu naweza kusema kwamba kati ya asilimia 90 hadi 95 ya wakazi wa Jimbo langu wote wamejiajiri kwenye shughuli za kilimo. Tunahitaji mbolea tani 38,015 tunaletewa tani 6,112 tunategemea miujiza gani kwenye kilimo ndugu zangu? Kwa kweli hatutegemei miujiza.

Kwa hiyo mimi nilikuwa naomba niishauri Serikali kwamba tunaweza tukaepukana na tatizo hili kwa kujenga Kiwanda cha Mbolea a Mkoani Mbeya. Tunajua kabisa ule wote ni ukanda wa kilimo ukitoka Rukwa, Mbeya, Iringa na Ruvuma ni ukanda wa kilimo.

Kwa hiyo, kama tukijenga Kiwanda cha Mbolea Mbeya mimi nadhani inaweza ikasaidia sana sehemu zote za Nyanza za Juu Kusini mpaka Magharibi. Tutaendelea kuagiza mbolea mpaka lini? Mimi nadhani Serikali ilione hili na kama kweli tuko *serious* na suala la kilimo Serikali ifikirie kujenga Kiwanda cha Mbolea pale Mbeya na hii itatusaidia sana kuinua sekta ya kilimo katika sehemu hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine muhimu kwa kilimo ni ardhi. Bahati mbaya sana wananchi wetu sehemu kubwa hawana ardhi ya kutosha. Sasa kule Mbozi kulikuwa na mashamba mengi ambayo yalikuwa yamechukuliwa na Serikali. Serikali imeanza kuyauza maeneo hayo. Tunashukuru kweli kuna wananchi wachache ambao wamepewa ardhi kwa kuuziwa kwa bei kidogo.

Lakini maeneo mengi yanachukuliwa na watu binafsi na wananchi walio wengi wanakosa ardhi. Sasa mimi naomba niseme lile ambalo nilipokuwa nazunguka kwenye kampeni wananchi walinituma niiombe Serikali. Tuna shamba ambalo lilikuwa linalimwa na *NAFCO* la Magamba. Ni shamba Na. 208 lina ekari 12,051. Serikali inataka kuliuza shamba hilo, hata hivyo wananchi wanaozunguka eneo hili wa vijiji vya Magamba, Iwalanje, Msanyila, Ipoloto na Lwati ambao walikubali kuitoa hii ardhi hiyo kwa Serikali ilipokuwa inaanzisha shamba hil, sasa wanaiomba Serikali iwape ardhi hiyo ili wapate eneo la kulima hasa ikizingatiwa kwamba *NAFCO* imeshindwa kuliendesha shamba hilo kabisa. Naiomba Serikali ili ifute hati ya shamba hilo na iwagawie wananchi wa Vijiji vinavyozunguka shamba hilo.

Mheshimiwa Spika, taarifa zilizopo ambazo mimi nimezipata ni kwamba ameachwa Meneja anayeangalia eneo lile na kwamba hulikodisha. Wananchi wanakodishwa ekari moja kulima kwa shilingi 10,000, sasa sisi hatuelewi hizi fedha wanazokodishwa wananchi zinakwenda wapi.

Naomba Waziri wa Kilimo atakapokuwa anajibu atueleze kwamba hizi fedha ambazo wananchi wanatozwa kwenye ardhi ambayo wao walikubali kwa hiari yao kuondoka zinakwenda wapi? Kwa taarifa tunazozipata wananchi wananyanyaswa sana juu ya matumizi ya ardhi ile. Kwa hiyo ninaomba Serikali itakapokuwa inajibu ilitolee ufafanuzi suala hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la maji. Wilaya ya Mbozi ina matatizo ya maji kwenye baadhi ya maeneo. Mimi naomba niseme kwamba leo Mheshimiwa Rais alipokuwa anatuhutubia pale amesema ameziorodhesha ahadi zote alizozitoa. Alipopita Mbozi tarehe 31 Agosti, 2005 alitoa ahadi ya kutatua tatizo sugu la maji kwenye miji ya Mlowo na Tunduma. Tunaomba Waziri wa Maji achukue hiyo ahadi kwa sababu sisi tuliandika na bila shaka Mheshimiwa Rais kama alivyosema watu

wake wamekamilisha kuandika ahadi zote alizotoa na hiyo ya Mlowo na tunduma itakuwepo.

Mji wa Mlowo ni Mji wa kibiashara kwa Wilaya Mbozi na ni mji ambao unakua sana. Leo tunazungumza tatizo la chakula Mlowo ukienda mahindi yamejaa sokoni, yapo mahindi. Kuna huduma mbalimbali zinazotolewa pale lakini hakuna maji. Mji wa Tunduma hali kadhalika najua Mbunge wa eneo hilo ni Naibu Waziri Dr. Siyame hawezi kulisemea lakini naomba nimsemee Tunduma hakuna maji na penyewe.

Lakini kwa sababu tulizunguka na Mheshimiwa Rais wakati wa Kampeni na akatoa ahadi basi tunaomba sehemu hizo mbili zipewe mkazo sana wa maji. Najua kuna matatizo maeneo mengi mengine mimi nitakaporudi nitakwenda nizungumze na wananchi tuone namna gani tunaweza tukaanza kuyatatua matatizo hayo.

Lakini naomba pia nizungumzie maji, sisi watu wa Wilaya ya Mbozi na hasa maeneo ambayo yanalima kahawa, maji ni muhimu sana. Tunatumia maji kwa ajili ya kuoshea kahawa baada ya kahawa kukobolewa huwa inavundikwa. Baada ya hatua hiyo baadaye inakwenda kuoshwa.

Sasa maeneo mengi hayana maji. Wananchi wanaosha kahawa kwenye maji ambayo kwa kweli sio mazuri sana. Matokeo, kahawa ile inakosa ubora kwenye soko la dunia. Tunakuwa na bei ndogo sana kwenye soko la dunia. Wananchi wanalalamika. Tunaomba suala la maji katika Wilaya yetu liangaliwe sana.

Naomba nizungumzie kwa haraka haraka suala la barabara. Naomba ieleweke kwamba Mbozi tuna barabara muhimu sana inayotoka Mlowo kwenda Kamsamba ambayo inaunganisha Mbozi na Jimbo la Kwela. Tuna barabara ambayo inakwenda Iyula, tuna barabara inayotoka Igamba kwenda Msangano, tuna barabara ya *Mbozi Circle.*

Hizi barabara ni muhimu sana kwa uchumi wa Wilaya na uchumi wa nchi hi i kwa ujumla Wilaya hii ni Wilaya ya wakulima kama nilivyosema, tunalima sana kahawa, tunalima sana mahindi na mazao mengine lakini barabara zake ziko kwenye hali mbaya sana.

Tatizo ni kwamba barabara zinajengwa kwa tope. Kwa kweli barabara zinajengwa kwa tope sio kokoto. Tunamwomba Mheshimiwa Mramba kwa sababu ameshawahi kuwa *RC* kule Mbeya na sasa ni Waziri wa Miundombinu alifuatilie. Kule maeneo ya Usangu kuna Kiwanda cha *TAZARA* ambacho wanazalisha kokoto.

Mimi nadhani Serikali ingeweza kuongea na Mamlaka ya Reli ya Uhuru *TAZARA* ili wauziwe kokoto na barabara zijengwe kwa kokoto. na sio matope ambayo wanaweka barabarani na wakati wa mvua barabara hazipitiki. Ninaomba Waziri pia atakapokuwa ana-*wind up* basi atueleze kwamba wenyewe wana mpango gani.

Mheshimiwa Spika, suala la umeme Mbozi kama nilivyosema ni Wilaya ya Uzalishaji. Maeneo mengi muhimu hayana umeme, kuna maeneo ambayo nguzo za umeme zimewekwa miaka mitatu lakini hakuna kinachoendelea. Mfano kuna barabara ya kutoka Ruanda kwenda Iyula, nguzo zimechimbwa zimechimbiwa karibu miaka mitatu hakuna kinachoendelea. Nguzo pia zimechimbiwa kutoka Vwawa kwenda Nyimbili miaka mitatu hakuna kinachoendelea.

Lakini kuna maeneo mengi kwa mfano sehemu za Itaka ambako pia ni maeneo mazuri sana kwa uzalishaji na huduma mbalimbali zipo lakini hatujui ni lini umeme utakwenda huko. Tunaomba tujibiwe hasa yale maeneo ambayo nguzo zimechimbwa Serikali itapeleka umeme huko lini na maana yake nini kuchimbia nguzo miaka mitatu halafu hakuna kinachoendelea.

Wananchi wamepewa matumaini hewa kwamba wanapewa umeme hakuna umeme unaoenda sehemu hizo. Baada ya kuzungumza hayo naomba mimi nimalize na suala la elimu nizungumze kwa ufupi tu hasa elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Spika, tumejenga sekondari tunajitahidi sana Mbozi kujenga sekondari, Wilaya nzima nazungumzia Wilaya sio Jimbo langu tuna jumla ya sekondari za Serikali 19 lakini inasikitisha Wilaya haina *high school* hata moja, hatuna shule ya kidato cha tano na cha sita hata moja. Sasa hata tukisema tunasomesha hawa watoto tutawapeleka wapi? Labda tunataka waishie mpaka kidato cha nne, mzee wangu Kabuye alisema kwamba pengine tunataka watoto hawa waishie kwenye shule za msingi kwa sababu naamini hata wakifika darasa la 12 bado hawawezi kufanya cha maana chochote. Kwa hiyo tunaomba Serikali pia ifikirie kujenga hata shule ya kidato cha tano na cha sita kule Mbozi, ili sekondari hizi tunazozijenga zitakapotoa watoto wanaomaliza darasa la 12 tuwe na hakika walau wachache wanaweza kwenda kwenye moja ya shule ambazo ziko kwenye Wilaya yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini muhimu na mwisho kabisa niseme kwamba Bodi za shule za sekondari hizi zinazojengwa kwenye Kata sio nzuri sana naomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu, waangalie namna nzuri ya kuunda Bodi. Lakini muhimu zaidi ni kwamba bodi hizi nyingi wajumbe wake sio wazuri sana pengine waangalie namna gani wanaweza wakawapata watu ambao wanaweza wakatusaidia zaidi. Pia madarasa mengi yanayojengwa hayana ubora unaostahili, hili pia lifuatiliwe.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kwanza ya yote na mimi nichuke nafasi kupongeza ushindi wa historia kwa Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, wewe mwenyewe Spika pamoja na Naibu wako, Wahaeshimiwa Mawaziri wote mlioteuliwa katika kipindi hiki

cha awamu ya nne, bila kumsahahu Mheshimiwa Waziri Mkuu Edward Lowassa, lakini pia nipende kuwashukuru mama zangu wa Mwaza ambao kwa kweli wameweza kunifikisha hapa na mimi nikasimama katika Bunge hili Tukufu kuongea nikiwa hapa Dodoma.

Lakini pia ni chama changu ambacho kimenipa umarufu mpaka nikafika hapa kupitia Wabunge hasa wa Majimbo Wabunge wa CCM, ndiyo maana na mimi nikapatikana katika wale wawili kutoka kila Mkoa.

Mheshimiwa Spika, mimi nianze tu moja kwa moja kuzungumzia hotuba ya Rais wetu Mheshimiwa Kikwete. Hotuba hii naiunga mkono kabisa na ninatoa pongezi zangu nyini kwa jinsi ilivyokuwa imeandikwa pamoja na kusomwa na yeye mwenyewe ikihusisha mambo karibu yote ambayo yanahitajika katika nchi yetu hii ya Tanzania.

Lakini pia nikazidi kuona kwamba hakuweza kuwasahau akina mama, hasahasa akina mama ambao ndiyo maana nasema wametufikisha hapa. Akizungumzia nyanja mbalimbali za kumgusa huyu mama kisiasa mpaka tumeweza kuongoza Bara la Afrika kwa maana ya kumuenzi Getrude Mongera, tumshangilie Mama huyu. (*Makofi*)

Bado tumepewa nafasi nzuri tu katika Mawaziri kuwa na maamuzi na bado hata katika nyanja za kiuchumi ameahadi kusimama imara na kwamba anamipango kabambe katika suala zima la kumuenzi mwanamke.

Katika hotuba hiyo, yaliyomo ni mazuri kama nilivyozungumza hapo mwanzo. Lakini napenda kusema tu iliyo kweli katika hotuba hii ni nzuri nawote tumeipokea, lakini kama Watanzania wenzangu kama hatutazingatia suala zima la mipango yetu ikaendana na muda kwamba tumewekaje mipango yetu, tutekeleze vipi na kwa muda gani tutakuwa tunaimba.

Nilitaka kusema tu ukweli maana tunaandaa mipango yetu lakini inafika mahala tunaahirisha tu, tunasema tutamaliza. Tutamaliza lini wala hatujui tunamaliza lini. Sasa katika taratibu hizi wala hatutafika watanzania wenzangu, hatutafika kabisa. Tunapaswa kama tunamipango yetu ili hii hotuba kweli iendane katika miaka mitano tujue kabisa kwamba tunaanzaje, tunatekelezaje, na ni kwa muda gani peke yake ndiyo hii hotuba itakuwa ya maana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala zima la kutii maamuzi ya ngazi mbalimbali. Mimi nitatoa mfano:-

Mheshimiwa Spika, katika elimu kwa mfano, tunaongelea sana sana tukidai fedha za MMES, leteni fedha za MMES, lakini kuna Mikoa hapa imeweza kujenga *secondary schools* bila MMES. Mikoa kama Kilimanjaro imejenga bila MMES, Mikoa kama Kagera imejenga bila MMES. Lakini wameweza kujenga *secondary schools* mpaka katika ngazi ya Kata. Kwa hiyo kwa sasa hivi wenyewe MMES sijui itajenga katika *level* gani?

Sasa katika hili mimi nina amini wenyewe walisikia kauli na wakaitii kauli hiyo na wakaendana na muda. Sasa wengine hatukujari hili ndiyo maana tuna sua sua tu katika hili. Kwa hiyo mimi katika hili tukiendana na hotuba hii tujue kabisa kasema nini, na tunapaswa kufanya nini ili kusudi suala zima la utekelezaji tuliwekee kipaumbele tumalize tuweze kufanya mambo yetu yakiwa yanazingatia muda. Niko pale pale.

Kwa mfano, kama suala zima la hifadhi ya mazingira, ndugu yangu mmoja ameshinda ni maji na miti. Ni kweli, tunaambiwa na wataalam kata mti mmoja upande mitano, ndiyo hivyo mimi nimekuta sera ya namna hiyo. Unapokata mmoja unapanda mitano. Tangia kusikia hilo, unapoukata mmoja unapanda mitano na mingine upande miti ya matunda, lakini nani anafuatalia hili, tumepanda mingapi?

Bado tunalia miti hatuna mvua kwa sababu hatuna miti, kwa sababu kazi yetu ni kukata hakuna anayepanda na hakuna anayefuatilia kama tumepanda. Kwa hiyo katika hali hii suala zima la ufuatiliaji katika ngazi mbalimbali kauli imetolewa na ngazi gani basi tunapaswa kuifutilia na kwa njia ya utekelezaji ulio sahihi.

Mheshimiwa Spika, lingine ni upande wa majengo ya Zahanati, kwa mfano ya afya na majengo mbalimbali. Kuna majengo, mengine sio majengo ni misingi, sijui ni ya tangu lini. Yamewekwa mawe ya msingi mpaka leo. Sasa ni lini utekelezaji huu utafanyika.

Mwisho napenda nizungumzie suala la ajira kwa vijana. Suala la ajira kwa vijana mimi ningeliona lirudishwe tu kabisa, na mwanzoni nilisema kwenye semina. Lirudishwe kabisa kwenye Halmashauri lizamie huko, hao ndio wanaoishi nao huko, na ziundwe Kamati ikibidi mojawapo iwe ya Kamati ya kudumu. Kuwajadili hawa vijana, maana ndiyo wanaokaa nao, na hizi Kamati zisiwe za Madiwani tu waingizwe humo na Viongozi wao waweze kusema ndani ya Kamati hizo wanataka nini; na ikibidi hata na viongozi wengine waweze kurijadili suala hili na Waheshimiwa Wabunge wawemo. Ili kusudi lije kimtandao kabisa tuweze kulitatua. Mimi liki kikundi naliogopa sana, tuwasaidiee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika namalizia na mimi kwa kuiunga mkono hotuba ya Rais kabisa moja kwa moja kwamba hii inahitaji tu utekelezaji na maamuzi na kwa muda unaostahili asanteni sana. (*Makofi*)

**MHE. JOYCE N. MACHIMU:** Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kuongea. Nianze kwa kutoa pongezi kwa ushindi mkubwa ilioupata Serikali iliyoko madarakani pamoja na viongoi wake kwa nyadhifa mbalimbali ikiwemo wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, na Naibu wako.

Mheshimiwa Spika mimi binafsi niwapongeze wanawake wa Mkoa wa Shinyanga walioniwezesha kufika hapa. Hotuba ya Mheshimiwa Rais imejitosheleza, na nimpe pongezi za aina yake kwa jinsi alivyo mahiri wa kisiasa na kiutendaji kulingana na jinsi alivyotoa hotuba yake. Imezingatia kila fani na yenye matarajio ya neema.

Mheshimiwa Spika katika hotuba hiyo naomba nigusie mambo yafuatayo:-

Kwa kuwa tuliahidi katika uchaguzi mkuu, Mheshimiwa Rais alivyokuwa kwenye kampeni yake na hutoba yake imegusia suala la wanawake:-

Tumekuwa tukihamasisha wanawake kuhusu kuunda vikundi vya kuviwezesha kiuchumi. Lakini kuna tatizo moja, naiomba Serikali ibuni njia mbadala kwa maksudi mazima ya kuwasaidia wanawake hawa kwamba, mikopo ambayo wamekuwa wakiipata kupitia vyombo mbalimbali vya Serikali na Taasisi zisizo za Serikali. Nakiri kwamba haiwawezeshi wanawake.

Kwa sababu viwango wanavyopata kwa mfano mwanamke anakopeshwa 50,000/- kwa biashara za sasa bado haijamwezesha mwanamke kukidhi mahitaji yake na aweze kurejesha hela hizo kwa mfano anapokuwa amepewa arejeshe labda kila wiki. Atakuwa amefanya biashara gani ya kuweza kukidhi haja. Isitoshe riba yenyewe ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi katika hoja hiyo ya wanawake nilikuwa na pendekezo la kwamba Serikali ione uwezekano wa kukaa na vyombo hivi ili wawe angalau na kiwango cha chini kumkopesha mwanamke mmoja mmoja shilingi 500,000 badala ya 50,000 aweze kuanza nazo.

Mheshimiwa Spika, naomba nigusie suala la elimu. Suala la elimu kwa jinsi hotuba ilivyojieleza ilituikamilishe kuitekeleza barabara. Katika shule za msingi kumekwa na upungufu ufuatao:-

Wananchi tuliwahamasisha wakajitolea nguvu zao wakajitolea kujenga madarasa lakini kumekuwa na huu mfuko umekuwa hautoshelezi, Mfuko wa MMEM. Kuna maboma mengi ambayo mpaka sasa hivi ninavyoongea hayajakamilika. Sasa niiombe Serikali ione uwezekano wa kutoa fungu jingine ili hizi nguvu za wananchi zisipotee bure, na tusiwavunje moyo ili hatimaye tena tukisema wajitokeze kuboresha hali ya watoto wao waweze kufanya kazi barabara. (*Makofi*)

Mheshsimiwa Spika, nitazungumzia pia mazingira ya mishahara ya Walimu; nitoe mfano halisi katika Wilaya ninayotoka ya Bariadi. Kumekuwa na mgogoro mkubwa unapofika wakati wa ulipwaji wa mishahara ya Walimu. Walimu wamekuwa wakikaa wiki nzima au wiki mbili wako Wilayani na kwa hivyo kupoteza vipindi vya wananfunzi kwa sababu ya utaratibu mgumu ambao unakuwepo Benki. Aidha katika Ofisi ya Mkurugenzi. Kwa hivyo nimwombe Waziri mhusika aboreshe mazingira haya ili hawa Walimu wawe wanafika na kuweza kupata hela yao mapema warudi vituoni mwao.

Mheshimiwa Spika, pia kumekuwa na tatizo la Walimu wachache wasiopenda maendeleo ya watoto wetu, kuwatumikisha watoto katika kazi zao binafsi. Wanafunzi wamekuwa wakipoteza muda kwa kufanya kazi kwenye mashamba ya watu binafsi kwa amri za Walimu wachache ambao hawana mtizamo mzuri ili wajinufaishe.

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa naiomba Serikali ilitazame hili jambo ili kutowaharibu watoto wetu.

Mheshimiwa Spika niongelee swala la elimu katika kitengo cha Sekondari. Tumekuwa na hizi Sekondari zilizoko katika Kata zetu. Sekondari hizi zimekuwa na upungufu wa Walimu na mbali na upungufu wa Walimu, kwa sababu mazingira kwa mfano ya Mkoa wa Shinyanga ambayo kielimu bado uko nyuma ningeomba Serikali ione uwezekano wa kuzijengea mabweni ili kuweza kuwasaidia watoto wetu wa kike ambao wanakuwa na mazingira magumu. Mtoto wa kike anapokuwa amepanga chumba chake asubuhi aamuke aende shule na baadaye arudi ajiandae kwa masomo anakuwa na kipindi kigumu kwa ajili ya vishawishi mbalimbali ambavyo vinapelekea wanafunzi wengi wananshindwa kumudu na hatimaye kushindwa kumaliza masomo kwa kupata mimba na ukizingatia hali ya sasa kuna huu ugonjwa wa UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, ningeiomba sana Serikali itizame hili suala kujenga mabweni na pengine kuboresha hali ya hawa watoto, kwa sababu mtoto ameanza darasa la kwanza katika shule ya Msingi Ikungwiliu. Ikungwiliu hiyo hiyo amemaliza darasa la saba akaingia Itilima Sekondari iliyoko Kata hiyo hiyo ya Wilaya ya Bariadi. Sasa mtoto huyu anakuwa kijiografia amedidimia kutokana na kwamba wanadamu tumeumbika katika uwezo mbalimbali na kwa hali hiyo kama tutakuwa na mabweni tutaleta na wanafunzi wengine wa Mikoa mbalimbali ambao watatia changamoto katika watoto hawa wa kabila moja ili wakapata uwezo wa kielimu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niongelee suala la kilimo. Katika Mkoa wa Shinyanga na nimwombe Waziri mhusika afanye juhudi pengine za kuitembelea Wilaya hii ya Bariadi ambayo natoa mfano halisi. Kumekuwa na tabia chafu ya Mabwana Shamba, unapofika wakati wa kilimo hawawajibiki kutoa elimu nzuri ya namna wananchi walimaje. Lakini inapofikia mahali kwa mfano zao la pamba na mahindi mwananchi amechanganya inafika mahali vyote vimekuwa na hali ya matumaini anasema ukate pamba ama mahindi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa hali hii imekuwa ikileta kero katika vijiji vyetu. Kwa hiyo nilikuwa naomba Serikali ilitizame hilo ili kuweza kuboresha hali za wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika mwisho nikuombe kabisa na niiombe Serikali kwa maksudi mazima kwa kuwa Mkoa huu wa Shinyanga uko chini kielimu niiombe Serikali ifanye uwezekano wa kujenga Chuo cha Walimu ili tuweze kuboreka katika shule zetu ambazo zimekuwa na upungufu wa Walimu.

Mheshimiwa Spika, namaliza kwa kuiunga mkono hoja ya hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa asilimia mia moja asante sana. (*Makofi*)

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge nimepewa taarifa hapa kwamba; Waheshimiwa Wabunge wananwake wote, wamealikwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu

nyumbani kwake mara baada ya kuahirishwa Bunge jioni hii. Nimetoa taarifa mapema kwa sababu wengine wamesema ni saa moja na nusu sivyo. Kwa sababu tutakuwa bado tunaendelea, lakini pia nimetumia muda huu kwa kuingilia ambayo isivyo kawaida. Kuingilia mjadala kwa sababu naelewa akina mama inabidi uwape nafasi. Ningetangaza mwisho ningekuwa siwatendei haki. (*Makofi*)

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi ningependa kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa ushindi wake mkubwa aliopata na imani kubwa aliyopata kwa wananchi wa Tanzania.

Pili ningependa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuteuliwa kuwa msaidizi mkuu wa Rais katika kusuma gurudumu la maendeleo.

Tatu napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kama wasaidizi wake katika kumsaidia kazi ya kuiongoza nchi hii hususani kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia nikupongeze wewe pamoja na Naibu Spika kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuliongoza Bunge hili Tukufu kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Napenda kuwapongeza Wabunge wenzangu kwa kupewa imani kubwa na wapiga kura wao ili waweze kuwaongoza katika kujiletea maendeleo yao namwomba Mwenyezi Mungu awape afya njema na baraka katika kutimiza wajibu huu mkubwa tuliopewa na wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa njia ya pekee mimi naomba nichukue nafasi hii niwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Morogoro kwani wameonyesha mapenzi makubwa kunirudisha tena hapa na mimi ninaamini kwamba kwa nguvu za Mwenyezi Mungu nitafanya kazi kwa pamoja nao kuwakomboa katika tatizo kubwa la umaskini maradhi na manyanyaso mengine.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza wananchi wote wa nchi hii kwa kukichagua Chama cha Mapinduzi kwa kishindo ninaamini kwamba wanatuamini kwamba tutawaletea maendeleo na tutawafikisha pale ambapo wamekuwa wanaota siku zote.

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu, Dr Harisson Mwakyembe nimetangaza asubuhi kwamba ni marufuku kama kuna msemaji anachangia ni marufuku kusimama kati yake na Spika. Kwa sasa niliache hivyo asante.

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, ningependa sasa kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Rais katika maeneo machache pamoja na kwamba hii hotuba kwa kweli kwa sisi ambao tumemsikiliza na kuisoma inatosheleza. Lakini mimi ninaamini kwamba tunachangia ili na sisi tuweze tukaangalia ni sehemu gani ambayo imegusa kero za wananchi wetu kule tulikotoka.

Mheshimiwa Spika, hivyo nitazungumza kwa ujumla halafu nitarudi kwenye Mkoa wangu wa Morogoro, naomba nizungumzie tatizo la usalama wa raia.

Mheshmiwa Spika, usalama wa raia tunafikili majambazi tu pamoja na mali zetu lakini ningependa niwakumbushe Wabunge wenzangu kwamba usalama wa raia ni pamoja na kusafiri na kufika salama bila ya kupata tatizo ukiwa majini, barabarani au hata angani.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nikumbushe tu kwamba kwenye mwaka wa 2003 lilitokea tatizo moja kubwa sana katika Mkoa wetu wa Morogoro. Kivuko cha Mto Kilombero kilizama, kikazama na abiria wengi wakiwemo wanawake na watoto na mali zao hata waume zao pia walizama.

Mheshimiwa Spika, miezi miwili baada ya hapo kile kivuko tena kilicholetwa kikazolewa kikatembea kwa umbali wa karibu nusu kilomita kikiwa kimebeba raia. Kwa sasa hivi naomba niseme kwamba wananchi wengi wanaotoka Wilaya ya Ulanga wanapovuka pale wanakuwa na wasiwasi mkubwa sana. Kero na kilio cha wananchi hawa wanaomba Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano iangalie uwezekano wa kutujengea daraja katika kivuko cha Mto Kilombero.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukilipata hili daraja naamini kwamba litachangia sana kuondoa umaskini ambao unakuwa kwa haraka sana katika Wilaya yetu ya Ulanga. Wananchi wa Ulanga sio wavivu, wanalima, lakini inasikitisha pale ambako wewe unalima kwa sababu mtu ana gari na uwezo wa kuja kununua anakuja anakupangia bei kwa sababu huna namna nyingine. Huwezi kusafirisha kupeleka kwenye soko kwa sababu ya matatizo ya usafiri.

Kero siyo hilo daraja tu, kero ni barabara pia. Barabara ya kutoka Lupilo Kwenda Malinyi mahali ambako mtu angesafiri kwa muda wa saa moja hadi moja na nusu, mtu unasafiri kwa masaa sita. Ukifika kule ukirudi kama gari yako inarudi salama basi unashukuru Mwenyezi Mungu.

Mimi ningeomba kwamba barabara ya Lupilo kwenda Malinyi iwekewe kipaumbele kwa sababu wale wananchi ni kwa muda mrefu wamekuwa na hiyo kero mpaka hata wanashindwa kuja kwenye Hospitali pekee ya Rufaa ambayo ipo katika Wilaya ya Kilombero.

Mheshimiwa Spika, ningependa nizungumzie barabara za Wilaya ya Morogoro Vijijini. Morogoro Vijijini kwa bahati mbaya hata Hospitali ya Wilaya haina. Maana yake ni kwamba panapotokea matatizo ya ugonjwa ambao unahitaji kwenda kwenye Hospitali ya Mkoa ni lazima usafiri. Ikipita muda wa saa 12 jioni inakuwa ni matatizo kumsafirisha mgonjwa aliyezidiwa kutoka Kisaki, kutoka Mtombozi kumleta Mjini Morogoro. Ni matatizo makubwa.

Mimi naomba Serikali iangalie kabisa kwa makusudi katika kuimarisha miundo mbinu katika haya maeneo ambayo mpaka sasa hivi wananchi wana ari ya kufanya kazi

lakini tatizo ni usafiri wa kile wanachokipata. Wananchi wana ari ya kiuweza kutumia huduma ambazo Serikali yao inawapa, lakini tatizo ni usafiri wa kwenda na kuzifikia zile huduma.

Mheshimiwa Spika, nizunguzie sasa, elimu. Nasikitika kusema kwamba katika huu mtihani wa darasa la saba mwaka jana, Mkoa wetu wa Morogoro umekuwa wa mwisho sio kwa sababu wananchi wa Morogoro tunazaliwa wajinga hapana ni kwa sababu tunakosa Walimu amabao wanamoya wa kufanya kazi; na watoto wengi wanatembea umbali mrefu kwenda mashuleni. Pamoja na wananchi wameweka juhudi kubwa sana katika kujenga shule.

Mheshimiwa Spika, kuna eneo ambalo unakuta Walimu wawili tu na watoto wengi sasa hawa Walimu wawili wafundishe darasa la kwanza pamoja na chekechea mpaka darasa la saba unajiuliza inakuwaje. Halikuishia hapo tu tumejitahidi tumejenga shule za kutwa, lakini nasikitika kusema kwamba hizi shule za kutwa nyingi hazina wanafunzi wa kutosha.

Kuna shule moja iko kijijini walifanya mtihani wa *form four* wanafunzi kumi tu. Kwa sababu wanafunzi wanatembea mbali hawapati chakula wananchoka na Walimu hawapo wanakata tamaa. Ninaomba Wizara ya Elimu itupie jicho la maksudi kabisa maeneo mengi ya vijijini katika Mkoa wetu wa Morogoro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie pia tatizo la watoto wa kike wanaopata mimba. Bahati mabaya kwenye Mkoa wetu wa Morogoro wanaosoma shule za kutwa wanapata mimba kwa sababu za kiuchumi, kwa sababu wanatembea mbali. Sasa hawa watoto wanapofukuzwa shule basi maisha yao ndiyo yamefikia mwisho.

Mimi naomba Serikali yetu na Wizara husika iangalie kwamba kama kutakuwa na uwezekanao wa kuweza kuwarudisha watoto shuleni au kuwe na shule maalum ya kuwapeleka hawa watoto waweze kumalizia shule kwa sababu ni wanawake na raia wa kesho.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze tena pia kuhusu suala la Polisi na ulinzi wa raia. Polisi wengi wanapenda kufanya kazi hususani katika Mkoa wetu wa Morogoro. Lakini kuna matatizo ya vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, wafanya kazi hususan Morogoro mjini kama kuna ambao wamekuja pale kuna polisi anaitwa saba siti. Saba sita anaanza kazi saa kumi na moja asubuhi mpaka saa sita ya usiku.

Lakini kinachosikitisha anapita anakamata vibaka, kwa sababu hana gari anarudi nao mpaka kwenye daraja la mto Morogoro pale Shan sinema, anawafunga pingu pale anaendelea kukusanya wengine kusudi aje akawaswage kama mbuzi kuwapeleka kituoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sio kwamba anawakosea haki zao za kibinadamu, lakini anafanya kazi. Ukifika pale kwenye kituo cha Polisi, nafikiri hata mtu asiombe kwenda pale hata kiti cha kukalia wewe uzungumze ukikaa vibaya wewe unadondoka chini. Hao ni wanadamu kama sisi. Wengi wetu tuna Ofisi nzuri tunafanya kazi. Kwa nini hawa ndugu zetu wanaotulinda wasipate Ofisi nzuri za kufanyia kazi. Jengo la enzi za mkoloni, ndiyo wana matatizo yao lakini matatizo mengine tumewatengenezea sisi wenyewe kwa kutokuwajali.

Mheshimiwa Spika, nafikiri kwenye sheria za Polisi na Jeshi la Wananchi Askari wengine wanastaafu wakiwa vijana mno. Halafu ukiangalia maslahi wanayotoka nayo hayawatoshelezi kuweza kujenga maisha yao na kuishi kama raia wema. Sisi tunachangia hao watu kuingia na kushawishika kusaidiana na majambazi. Naomba Serikali yetu iangalie namna ya kuwasidia wastaafu wetu wa Majeshi yote ili wasiwe kwenye hali ambayo kwa Kiingereza wanasema *desperate state* inayomsukuma mtu kuwa mhalifu bila kupenda. Naomba hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa elimu: Kuna Mpango wa *MEMKWA*, huo mpango wa *MEMKWA* ulikuwa unasaidia sana watoto wetu walio wengi wanaishi kwenye mazingira magumu ambao kwa sababu ya kuishi kwenye mazingira hayo wanashindwa kwenda shule. Sehemu nyingi zimeanzishwa hizi shule za *MEMKWA*. Lakini, ni kama kwamba zinakuwa zipo zipo tu, wale watoto wasome kama elimu ya watu wazima, basi ifike mahali wasahaulike.

Mheshimiwa Spika, naomba kusema kwamba pale Morogoro kuna kituo cha kwanza kabisa cha *MEMKWA* kiliazishwa na Shirika la Faraja. Watoto wote katika hili Shirika wanasoma miaka miwili, wakifanya mtihani wa darasa la nne wanafaulu. Kwa nini wanafaulu? Wanatoka kwenye mazingira magumu, wanapata chakula cha mchana na walimu wanatosheleza. Sasa hivi vituo vinavyoendeshwa na Wizara ya Elimu, kwa nini hao watoto wasichukuliwe na wametoka kwenye mazingira magumu wapate angalau uji na walimu wa kutosha. Wale watoto hata *uniform* hawana. Nafikiri Halmashauri zao kama wanaweza wakapata hela za kufanyua vikao vingine, basi washauriwe waweze kutoa *uniform* kwa hawa watoto ili waweze kujiona kwamba na wao ni watoto kama watoto wengine. Wengi wao ni watoto yatima na wengi wao wanatoka kwenye *single parenthood*. Wanatoka kwa akinamama tu, hawana baba, wamezaliwa na baba zao ambao wamewakimbia.

Mheshimiwa Spika, nizungumze kidogo kuhusu mazingira. Mkoa wa Morogoro ulikuwa na mito mingi sana. Sasa hivi ¾ ya hiyo mito imeishakauka kwa sababu ya mazingira yameharibika.

Mheshimiwa Spika, Mto Morogoro unakauka, Mto Wami unakauka, Mto Ngerengere umekauka kwa sababu mazingira yameharibika. Kuna *NGOs* nyingi zinazofanya kazi ya mazingira Morogoro, lakini hakuna *Impact*. Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Tunazingatia, Spika anapoingilia kati; *time ina-stop*. Ahsante sana. Mheshimiwa Eustace Katagira atafuatiwa na Mheshimiwa Said A. Arfi na Mheshimiwa Rished Abdallah ajiandae. Mheshimiwa Katagira hayupo, kwa hiyo namwita Mheshimiwa Said A. Arfi.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda niungane na wenzangu katika kukupongeza wewe binafsi kwa kupata nafasi ya Uspika wa Bunge hili tukufu, Naibu Spika. Kadhalika napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, niwapongeze Mawaziri na Manaibu Waziri. Baada ya hapo napenda pia nichukue nafasi hii kuwashukuru wapiga kura wa Jimbo la Mpanda kati kwa kunichagua kuwa Mwakilishi wao katika Bunge hili tukufu. Najua na naamini walikuwanazo sababu na kwa nini wamefanya hivyo. Kwa hiyo napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo napenda nami nichangie hoja ya Serikali kuhusu hotuba ya Mheshimiwa Rais. Hotuba ya Mheshimiwa Rais kama alivyoiwasilisha katika Bunge hili Tukufu tarehe 30/12/2005, ilikuwa ni dira na dhamira ya Serikali ambayo atakayoiunda. Suala ambalo lililokuwa nimelitizama niliona kwamba; Je, dhamira hii itabebwa na Serikali yake? Je, hao atakaowapa dhamana ya kumsaidia, watamsaidia? Kwa sababu katika hotuba yake Mheshimiwa Rais, alijaribu kutukumbusha Watanzania kwamba Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikuwa na dhamira ya kutaka kuweka uchumi umilikiwe na Watanzania kupitia Mashirika ya Umma. Lakini wale waliopewa dhamana walishindwa kumsaidia Baba wa Taifa na leo Mashirika yote hatunayo tena. Hofu yangu ni kwamba Je, hawa ambao wamepewa dhamana hii, watakuwa na dhamira ambayo anayo Rais wetu ili waweze kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, wasi wasi wangu hasa umezingatia sana… nimepata kupitia taarifa za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Taarifa za Mkaguzi Mkuu wa Serikali ambazo nimepata kuzipitia, nyingi zimeonyesha ni namna gani matumizi mabaya ya fedha za wananchi. Lakini hoja zinazotolewa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali pamoja na kuonyesha mapungufu mbali mbali ya ndani ya Serikali kutokana na matumizi mabaya ya fedha za Umma, lakini hakuna hatua zozote zilizochukuliwa. Wasi wasi wangu kwamba ili tuweze huko tunakotaraji kufika, kwanza kabisa ni lazima tujenge nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais katika hotuba yake ametueleza kwamba ana hofu kwamba yameanza kujengeka matabaka katika jamii yetu. Ni kweli matabaka yameanza kujengeka na si matabaka ya kiuchumi tu. Ya walionacho na wasiokuwa nacho, tabaka la matajiri na maskini sasa hivi linaonekana wazi katika nchi yetu. Kibaya zaidi ambacho mimi nina hofu nacho zaidi ya hilo la matajiri na maskini, ni tabaka katika elimu. Ifikie mahali sasa hivi tuanze kuliangalia suala la tabaka katika elimu. Leo, zipo shule ambazo watoto wa maskini hawawezi kwenda katika shule hizo na ziko shule kwa ajili ya watoto wa makabwela. Shule za watoto wa makabwela ni vyumba viwili vya darasa kwa ajili ya darasa la kwanza mpaka darasa la saba. Sasa katika hali hii ni kwamba Watanzania wengi walio maskini hawataweza kupata elimu. Sekta ya watu binafsi ambayo imeambiwa ishiriki katika kuchangia elimu, wamejenga shule,

tunawapongeza na tunawashukuru. Lakini shule zao hazifikiki kwa sababu ya suala la karo. Leo ziko shule za watoto wa chekechea, shilingi 800,000/=. Kiwango hiki ni kikubwa kabisa kwa Mtanzania wa kawaida maskini kuweza kumsomesha mtoto wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais katika hotuba yake ameonyesha hofu yake kuhusu matatizo yatokanayo na ujenzi holela katika miji yatu. Tatizo la ujenzi holela katika miji yetu, hilo ni moja. Lakini pia limeathiri huduma za jamii katika miji yetu. Miji imepanuka, idadi ya wakaazi katika miji yetu imeongezeka, lakini huduma za jamii kama maji na hospitali hazijapanuka. Leo, pamoja na kupanuka kwa miji, lakini hakuna mitandao ya bomba ambayo inafikishwa katika makazi mapya ya watu isipokuwa watu wanaendelea kuunganisha nyumba hadi nyumba, nyumba hadi nyumba. Mifumo ya maji katika miji yetu ni ile ile ambayo tumeirithi chakavu imechoka na bado mzigo huu zinaachiwa Halmashauri ambazo hazina uwezo kwa sababu hazina vyanzo vya mapato ya kutosheleza kuweza kubadilisha mifumo ya maji katika miji yao.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika katika hospitali, bado tatizo la msongamano wa wagonjwa ni kubwa sana. Kwa mfano hospitali ya Wilaya ya Mpanda pamoja na idadi ya wakaazi kuongezeka, lakini idadi ya vitanda imebakia kuwa ni ile ile. Vitanda 96 ambavyo vipo katika Hospitali ya Wilaya. Wodi ya wagonjwa wanaume ina vitanda 14 kwa maana kwamba kila siku utakayokwenda hospitali ni lazima utakuta watu wamelala wawili wawili kila kitanda. Mbali na magonjwa ambayo sasa hivi yamejitokeza na mchanganyo wa kuchanganya wagonjwa katika wodi, unaweza ukaenda umepelekwa kwa ajili ya maradhi ya malaria, ukatoka na kifua kikuu. Hii ndiyo hali katika hospitali zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo ambalo ninapenda pia nichangie, ni kuhusu Nishati, nishati hususani ya Umeme. Inasikitisha, lakini ndiyo kawaida katika nchi yetu; maeneo ambayo yamesahaulika, yanaendelea kusahaulika na wala hayakumbukwi na kutazamwa. Karibu sehemu kubwa ya nchi yetu imeunganishwa katika gridi ya taifa na juhudi zinaendelea kufikisha umeme Kigoma na Ruvuma kama alivyosema Mheshimiwa Rais katika hotuba yake. Lakini, mikoa ya Kagera na Rukwa haimo katika Mpango wa kupata umeme kutoka katika gridi ya taifa. Mikoa hii itaendelea kupata umeme kutoka kwa majirani zetu Uganda na Zambia na tutatarajia kupata huruma ya majirani zetu. Leo hii Sumbawanga, usiku unaanza saa tatu, hawapati umeme isipokuwa saa tatu ya usiku Wazambia wakifurahi, ndiyo wanawawashia umeme Sumbawanga. Sasa ni lazima tuangalie kwamba na mikoa ya pembezoni nayo itazamwe. Labda nimalizie tu katika hili ambalo nilikuwa nafikiri kuwa nalo ni muhimu. Suala la Utalii na Madini. Madini nayo pia yamepuuzwa, Utalii kwa kule Mpanda ungeweza kuchangia kabisa katika pato la taifa lakini hatuna miundombinu ya kuweza kuwafikisha watalii au wawekezaji katika sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache nimalizie tu kwa kusema kwamba Serikali sasa nadhani ipo haja ya kutamka bayana kwamba bado wana mpango wa kuendelea kujenga Makao Makuu ya Dodoma au wameacha, kwa sababu Serikali imeuza nyumba za Mawaziri na leo inajenga nyumba za Mawaziri Dar es salaam badala

ya Dodoma. Mpango huu ni wa muda mrefu, umeanza kwenye miaka ya sabini, lakini mpaka sasa Makao Makuu hayajahamia Dodoma. Ni vyema Serikali ikatamka wazi kwamba ina dhamira na ina utashi wa kweli kweli wa kuhamishia Makao Makuu Dodoma, vinginevyo gharama za kuhamishia Makao Makuu Dodoma zitakuwa ambazo hazibebeki na ni mzigo kwa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, napenda kuzungumzia kuhusu chakula. Pamoja na Mkoa wetu ni Mkoa ambao unazalisha chakula na pengine hatuna matatizo makubwa sana, lakini bei za soko ni kubwa. Wale wanaozalisha chakula wanapaswa pia watizamwe wanapokuwa na upungufu wa chakula na wao waweze kusaidiwa. Hali itakapojitokeza hivyo, naamini kabisa Serikali yetu haitaacha kututazama na kutuonea huruma na kutuletea chakula.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. Ahsante sana , naunga mkono hoja. (*Makofi)*

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba ambayo aliitoa Rais tarehe 30 Desemba 2005. Kwanza, nakuomba radhi kwamba sauti yangu kidogo ina matatizo kwa hiyo naomba uniwie radhi.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda niunge mkono hotuba ya Rais, lakini kabla sijachangia naomba na mimi niseme maneno machache ya utangulizi. Naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Kondoa Kusini kwa kunirudisha tena katika Bunge hili Tukufu. Kama nilivyowaahidi wakati matokeo yalipotolewa, nitahakikisha kwamba sitawaangusha.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nitumie nafasi hii kumpongeza sana Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete ambaye alishinda kwa kishindo katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka jana. Napenda nitumie nafasi hii pia nikupongeze wewe Mheshimiwa Spika pamoja na Naibu wako kwa kuchaguliwa kushika Nyadhifa zenu.

Aidha nimpongeze ndugu yangu Mheshimiwa Edward Lowassa kwa kuteuliwa na Rais na kuthibitishwa na Bunge hili Tukufu kuwa Waziri Mkuu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia nitumie nafasi hii kuwapongeza Wabunge wenzetu waliopewa nyadhifa mbali mbali na Rais. Nikianza na Mawaziri, Manaibu Waziri na Wakuu wa Mikoa. Napenda niwapongeze sana na niwatakie kila la heri katika nafasi hizo ambazo Rais amewakabidhi. Mwisho, siyo kwa umuhimu lakini, napenda nitumie nafasi hii pia niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote tuliopo hapa. Wale tuliochaguliwa na wale tulioteuliwa kuingia katika Bunge hili Tukufu. Napenda niwapongeze na niwatakie kila la heri.

Mheshimiewa Spika, baada ya maneno haya ya utangulizi, na mimi nitumie muda mfupi sana kuchangia hotuba ya Rais wetu. Kwanza, nianze na kuzungumzia hali ya chakula katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hali ya chakula katika nchi yetu ni mbaya na hii inatokana na ukame wa mara kwa mara unaotokea katika nchi yetu. Wakulima wetu wanalima sana na wanalima maeneo makubwa lakini tatizo kubwa ambalo linasababisha upungufu wa chakula mara kwa mara ni tatizo la mvua. Kwa hiyo, kama tunataka kutatua tatizo la njaa katika nchi yetu, lazima tuangalie ni namna gani tunawasidie wakulima wasiendelee kutegemea mvua peke yake katika kilimo chao. Maana yake kwamba waende katika kilimo cha umwagiliaji maji mashamba.

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze sana Rais. Katika Hotuba yake ametoa ahadi kwamba atahakikisha fedha za kutosha ama fedha nyingi zaidi zitatengwa ili kilimo cha umwagiliaji kipanuliwe. Pia ameahidi kwamba atapeleka wataalam zaidi katika kilimo ama katika sekta hiyo ya umwagiliaji. Bila shaka Rais ana nia njema kabisa ya kutusaidia tuweze kujikwamua katika tatizo hili la njaa.

Kwa hiyo napenda nimpongeze sana na mimi napenda nikubaliane naye kwamba hatua peke yake ama mojawapo ya kuweza kusaidia kutatua tatizo la njaa katika nchi yetu ni kuanzisha kilimo cha umwagiliaji maji katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia niseme hivi kwamba, wakati tunapoangalia maeneo ya kumwagilia maji ama maeneo ya mabonde ya kumwagilia ama kuanzisha kilimo cha umwagiliaji maji, tusikimbilie tu yale mabonde makubwa makubwa ambayo tunayafahamu: Rufiji, Pangani na kwingineko. Tuna maeneo ama mabonde mengi mazuri sana katika maeneo yale kame ambayo yanaweza kumwagiliwa na yanaweza kutoa chakula cha kutosha ama mazao ya kutosha ya chakula na ya biashara na kuweza kukwamua tatizo hili la njaa katika eneo letu ama katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe mfano wa eneo moja ambalo liko katika Mkoa wa Dodoma. Ni eneo ambalo limefanyiwa utafiti wa muda mrefu na imethibitika kwamba ni eneo zuri sana la umwagiliaji na ningependa na niwaombe Serikali walitupie macho eneo hilo. Eneo hilo ni lile la bonde la Mto Bubu. Limefanyiwa utafiti mara nyingi sana na imethibitika kwamba maji yanayopita katika Mto huo wa Bubu katika Wilaya ya Kondoa yanatosha kwa umwagiliaji wa hekta 10,000 endapo Bwawa litajengwa katika kijiji cha Farukwa na Mpendo katika Wilaya ya Kondoa. Matokeo kutokana na utafiti, imedhihirika kwamba endapo hekta hizo 10,000 zitalimwa kwa utaratibu huo wa kumwagilia, kuna uwezekano wa kuzalisha tani 24,000 za mazao mbali mbali yakiwemo na mazao ya chakula. Kwa hiyo, mimi naomba sana Serikali wakati inapoanzisha mpango kabambe wa umwagiliaji maji mashamba, basi Bonde hili nalo lipewe kipaumbele katika maeneo yetu.

Nitashangaa sana Serikali kukimbilia mabonde yale makubwa kwenye mito mikubwa na kuacha mabonde mazuri ambayo yako katika maeneo kame. Hatuna mpango wa kuhama kutoka Dodoma sisi wananchi wa Dodoma, kwa hiyo lazima mtusaidie kama Serikali tuweze kujitegemea. Kama hamtatusaidia, tutaendelea kuomba chakula na leo baada ya kuzungumza haya, nitaomba chakula tena lakini naomba mtusaidie tusiombe chakula tena kwa kulishughulikia bonde hili la Mto Bubu. Kwa hiyo, ombi langu la kwanza ni kwamba katika mradi wa umwagiliaji maji ambao Rais ameahidi kwamba

atatoa fedha nyingi na wataalam, basi suala la umwagiliaji maji katika Bonde la Mto Bubu lizingatiwe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa kuwa muda ni mfupi, naomba sasa niombe msaada wa chakula. Mheshimiwa Spika, Serikali yetu inajitahidi sana kutatua tatizo la chakula ama njaa katika nchi yetu. Lakini, nina wasi wasi na takwimu zinazotumika katika kutoa hicho chakula. Takwimu siyo sahihi. Matokeo yake msaada wa chakula tunaopata toka Serikalini ni mdogo sana. Nitoe mfano wa Kondoa, Ofisi ya Waziri Mkuu inatuambia kwamba wenyewe Takwimu zao zinasema kwamba watu ambao wana upungufu wa chakula ni takribani 59,000. Sisi Takwimu zetu za Wilaya zinasema ni watu 131,000. Kwa hiyo tofauti ni kubwa mno. Maana yake ni nini, maana yake kama utatoa chakula cha watu 59,000 wengine watakufa njaa. Napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, hata leo katika hotuba yake aliahidi kwamba atahakikisha kwamba hakuna Mtanzania atakaye kufa njaa. Sasa naomba basi takwimu sahihi zitumike ili tuhakikishe kwamba hakuna Mtanzania atakayekufa njaa katika nchi yetu. Naomba sana na naomba Ofisi ya Waziri Mkuu tuwasiliane ili niweze kuwapa takwimu sahihi za tatizo la chakula katika Wilaya ya Kondoa. Baada ya kusema hayo, kwa kuwa kengele ya kwanza imegongwa, naomba nitaje maeneo machache ambayo ningependa kuchangia. Kwanza, eneo la sekta ya elimu. Tumejitahidi sana katika sekta ya elimu, kuboresha elimu kwa maana ya majengo lakini tuna tatizo kubwa sana la walimu. Elimu haiwezi kupatikana kwa kukusanya wanafunzi katika shule ama mazingira ya shule. Elimu inapatikana kutoka kwa walimu. Kwa hiyo tunaomba tuhakikishe kwamba walimu wanapatikana katika shule zetu za msingi na shule za sekondari. Hivi sasa kuna sekondari zinazoendeshwa na mwalimu mmoja ama wawili. Pale hakuna elimu inayotolewa. Mimi naomba sana, tutaendelea kujidanganya natakwimu zetu lakini haisaidii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Rais. Naunga mkono hotuba hiyo. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Rais na pia kuwapongeza wale wote ambao wamechaguliwa katika nafasi mbali mbali za uongozi wa taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kutoa shukrani za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Kigoma Kaskazini kwa kunichagua kuwa Mbunge wao. Naamini kabisa imani waliyonipa, nitairejesha kwa kuwatumikia kwa uaminifu mkubwa na kuhakikisha kwamba yale yote ambayo tuliahidiana wakati wa kampeni, yanatekelezwa.Uchaguzi ulikuwa ni mgumu sana. kama unavyofahamu, kampeni ni ngumu sana, lakini licha ya umri wangu mdogo na licha ya kuwa nimetoka tu shuleni, mwaka uliofuata mwaka wa Uchaguzi, nimefanikiwa kushinda na kupata heshima ya wananchi Jimboni. Pili, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa chama changu, Chama cha Demokrasia na Maendeleo na hasa Mwenyekiti wangu wa Taifa Mheshimiwa Freeman Mbowe. Amefanya kazi kubwa sana ya kisiasa, Chama chetu kimekua. Chama chetu wakati vyama vingi vinaanza kilikuwa na Wabunge watatu, sasa hivi tuna Wabunge 11. Tulikuwa na asilimia 3 tu ya kura za Wabunge mwaka 1995, sasa hivi tuna

asilimia 8 ya kura. Kwa hiyo kwa kweli ni chama ambacho kinaleta matumaini makubwa kwa Watanzania, na mimi napenda kuwahakikishia tu wanachama wa CHADEMA kote Tanzania kwamba tutafanya kazi yetu kwa bidii kuhakikisha kwamba tunaifanya Serikali inatekeleza wajibu wake kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, la kwanza ambalo nataka kulizungumzia mimi katika hotuba ya Rais ni suala la mishahara ya wafanyakazi wa Umma. Jambo hili limekuwa likilalamikiwa muda mrefu sana. Jambo hili limekuwa likiwafanya wafanyakazi wa Umma wafanye kazi katika mazingira magumu na imefikia wakati sasa kwa kweli Serikali iangalie kwa moyo mkunjufu kabisa, uwezekano wa kuweka hali maalum ya jinsi gani ambavyo mishahara ya wafanyakazi itakuwa inakuwa, Mheshimiwa Rais ameahidi kuunda tume ya kuangalia jinsi gani ya kuboresha maslahi ya wafanyakazi wa Umma. Mimi pendekezo langu, ni pendekezo kwa Waziri wa Fedha na kwa Waziri wa Utumishi, kwamba tuangalie uwezekano wa kuweka asilimia maalum ya pato la taifa kwenda kwenye mishahara ya wafanyakazi. Hivi sasa mishahara ya wafanyakazi ni asilimia 4.2 ya *GDP* ya Tanzania. Mimi ninashauri, iwapo tutafikia hali ambayo mishahara ya wafanyakazi wa umma ikafikia asilimia 6 ya *GDP*, wafanya kazi wetu watakuwa na moyo sana wa kufanya kazi hasa ukizingatia kwamba pale ambapo uchumi utakuwa unakua, vile vile mishahara ya wahfanyakazi itakuwa inakua bila kuhitaji Waziri kila mwaka kuja kutangaza nyongeza za mishahara. Katika hili la mishahara ya wafanyakazi, nataka kuliongelea kwa uchungu kabisa suala la mishahara ya Madiwani.

Mheshimiwa Spika, Madiwani wetu wanalipwa posho ndogo sana. Shilingi 30,000/= kwa mwezi kwa kiongozi kama Diwani ambaye anafanya kazi zaidi kwa wananchi kwa sababu yeye ndiye yuko na wananchi kila siku, ni pesa ndogo sana. Ninaishauri Serikali iangalie uwezekano wa kupandisha posho za Madiwani za kila mwezi ili na wao pia waweze kuboresha ufanisi wao wa kazi. Hili ninaiomba kwa kweli Serikali ilichukulie umuhimu wake. Angalau wafikie shilingi 100,000/= maana wako Madiwani karibu 3,000 tu nchi nzima. Siyo pesa nyingi sana hii iwapo tukiweka dhamira ya dhati. Bado kuna maeneo mengi sana ambayo Serikali inaweza ikahakikisha kwamba inaziba mianya ya matumizi mabovu. Mimi nakumbuka wakati nipo shuleni, wakati wa Mwalimu kulikuwa kuna *standardization* ya magari ya Serikali. Ilikuwa *Landrover* ndiyo gari za Serikali, hata matairi ya gari yanapoagizwa kutoka nje yanawekwa mhuri wa *GT*.

Sasa hivi kila Waziri anaamua gari gani ya kununua kwenye Wizara yake. Nadhani hili tuliangalie. Serikali *i-standardize*, kama inaamua *Landcruiser VX* ndiyo gari za Mawaziri, iwe ni hizo ili kuweza kuhakikisha kwamba tunakuwa na mfumo mzuri, mtu ukiona gari barabarani unajua kwamba hii ni gari ya Waziri fulani, hii ni gari ya Waziri fulani. Siyo kila Waziri huyu anapanda *Nissan*, huyu anapanda *Prado*, huyu anapanda hivi na inakuwa ni vigumu sana kwa Serikali kuweza kudhibitihaya mambo.

Kwa hiyo, nashauri tuangalie uwezekano wa ku-*standardize* na hii itasaidia kuweza kudhibiti. Lakini la muhimu zaidi, ukipita kwenye ofisi zote za Serikali unakuta *furniture* zinazoagizwa kutoka nje. Ni lini tutawawezesha watu wetu, hawa maseremala wetu wakaweza kuzalisha bidhaa bora zikatumika kwenye ofisi zetu za Serikali? Ninaomba Serikali iliangalie suala hili. Serikali ipige marufuku ofisi zake kuagiza

fenicha kutoka nje, kwa sababu hii siyo *pro-poor policy.* Hii haiwawezeshi Watanzania kuweza kuzalisha wao wenyewe na wakawa wanapata soko la uhakika kutoka Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo napenda kulizungumzia ni suala la utaifa. Mheshimiwa Rais amezungumzia suala zima la Taifa kumomonyoka na kuna baadhi ya maeneo amezungumzia kwa uwazi kabisa, kwamba imefikia wakati sasa mtu anaweza akaomba uongozi wa nchi kwa kutumia *statements* za ubaguzi wa rangi, na hii tumeiona, hii ni mbaya sana. *(Makofi)*

Mtu anaweza akaondoka tu mwandishi wa habari, akaenda akaandika kwenye gazeti kwamba huyu fulani siyo Mtanzania, huyu ni Mwarabu. Kuna watu ambao wameitumikia hii nchi kwa umri mrefu sana. Kuna watu ambao wamejenga heshima katika nchi hii, wanavuliwa heshima kwa kalamu tu ya mwandishi wa habari! Hii ni *very dangerous* na ni lazima tuliangalie. Tuepuke sana ubaguzi wa rangi katika nyadhifa za kiuongozi na hili tulikemee kwa sababu Mwalimu Nyerere alisema ubaguzi ni sawasawa na kula nyama ya mtu, ukiishaila huiachi! Tukishaanza tatizo la kubagua watu kwa sababu ya walikotoka, kwa sababu ya rangi zao, tutafika pabaya sana kwenye Taifa letu. Kwa hiyo, naomba suala hili liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo naomba liangaliwe kwa mujibu wa hotuba ya Rais ni suala la rushwa. Rais amependekeza na ninaamini kwamba hili Serikali italichukua. Kuwe na mjadala wa kitaifa kuangalia jinsi gani ya kushughulikia suala la *campaign financing. This is extremely important.* Ni muhimu sana kwa sababu tusipokuwa na sheria inayo-*regulate* matumizi ya fedha katika kampeni, tutakuwa na viongozi ambao ni wenye pesa tu. Wale wachache kama sisi tuliokuwa tumetoka shuleni lakini tuna kipaji cha uongozi tutajikuta tunashindwa kuingia katika nyadhifa za uongozi kwa sababu ya ukosefu wa pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa dakika chache zilizobakia napenda kuzungumzia suala hili la Ushirikiano wa Kimataifa. Mheshimiwa Rais amezungumzia suala la ushirikiano wa Kimataifa. Amezungumzia kuimarisha Jumuiya ya Afrika Mashariki, amezungumzia kuimarisha *SADC* na pia suala zima la uanachama wa Tanzania katika *African Union,*

Mheshimiwa Spika, napenda sana kukazia katika suala la Jumuiya ya Afrika Mashariki na uanachama wetu katika *SADC* na kujitoa kwenye kwenye *COMESA.* Ninaamini kabisa kwamba Tanzania ilifanya makosa kujitoa *COMESA.* Ilifanya makosa kwa sababu tunafanya biashara zaidi na nchi za *COMESA* kuliko nchi za *SADC.* Kwa nchi za *SADC, the biggest economy is in South Africa*, lakini kwetu sisi South Africa kwa kiasi kikubwa sisi ni soko badala ya sisi kuuza bidhaa za kutosha huko.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa nchi yetu inafanya majadiliano na nchi za Jumuiya ya Ulaya kuingia katika *Free Trade Area,* kuna kitu kinaitwa *Economic Partnership Agreement*. Mkataba huu utakaposainiwa mwezi Desemba mwaka 2007, bidhaa za kutoka nchi za Ulaya zitakuwa zinaingia nchini kwetu bila kodi. *96 percent* ya *products* za Ulaya zitakuwa zinaingia nchini kwetu bila kodi. Hivi sasa sisi tuna-*enjoy EBA*

(*Everything But Arms*) ambayo na sisi tuna-*export* bila kodi katika nchi za Ulaya, lakini watu wa Ulaya nao wanataka sasa hizi *concessions*.

Sisi tumeamua kujadili hili jambo kupitia *SADC* na nilimuuliza Waziri wa Viwanda na Biashara wakati tuko kwenye semina Dar es Salaam. *SADC* kuna nchi nne tu ambazo tuna uwezo wa ku-*negotiate EPA,* lakini bado sisi kama nchi tumeamua ku-*negotiate* na hizi nchi na bahati mbaya sana hizi nchi hatufanyi nazo biashara. Hatufanyi biashara kubwa na Angola, hatufanyi biashara kubwa na Msumbiji, hatufanyi biashara kubwa na Lesotho, hatufanyi biashara kubwa na Swaziland, naamini kabisa kwamba Serikali inabidi iangalie upya, tuweze ku-*negotiate* EPA hizi na *club* kubwa ya nchi 16 ya nchi za *COMESA.* Inawezekana tuka-*negotiate EPA through COMESA* bila kuwa wanachama wa *COMESA.* Kwa hiyo, ninaomba Waziri wa Viwanda na Biashara na Waziri wa Uchumi, Mipango na Uwezeshaji na Waziri wa Fedha, kwa sababu haya mambo yako chini yao, waliangalie hili ili kuweza kuhakikisha kwamba tunakwenda katika umoja ambao utalifaidisha taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, ni kuhusu suala la Chuo Kikuu kipya. Mheshimiwa Rais ameahidi kwamba angalau tuwe na Chuo Kikuu kipya. Nina tatizo na hii ahadi ya Rais kwa sababu mpaka sasa hivi kuna matatizo makubwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, hakuna vyumba vya kutosha vya mihadhara na hakuna mabweni ya kutosha. Ninashauri kwamba badala ya sasa hivi kwenda kufungua Chuo Kikuu kipya, tuimarishe Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, tuondoe matatizo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, tuwaimarishe wanafunzi wa chuo hicho. Sasa hivi wanafunzi wanasoma wanachungulia nje badala ya kuingia kwenye *lecture rooms.* Kwa hiyo, ninashauri kwa hii miaka mitano ya mwanzo ya utawala wa Rais Kikwete tuangalie uwezekano wa kuimarisha zaidi vyuo vilivyopo ili viweze kutoa elimu ambayo inastahili.

Mheshimiwa Spika, nimemaliza hoja zangu ambazo nilitaka kuzizungumzia na ninashukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Nadhani Mheshimiwa Beatrice Shellukindo atakuwa mzungumzaji wa mwisho.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, kabla sijazungumza naomba tu nitoe rai yangu kwako na kwa Bunge hili Tukufu. Nina makubaliano. Moja ya masharti wakati wa uchaguzi wananchi wangu walisema tunaomba pindi utakapoanza kuzungumza Bungeni tukuone kwenye *TV,* tukusikilize kwenye redio. Sasa ninavyoona hapa, vyote hivyo kama sivioni. Kwa ruhusa yako kama utakubali naomba nizungumze kesho asubuhi, kama inaruhusiwa na kanuni zinavyosema. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Kwa taarifa yako Mheshimiwa Mbunge, kila anayeongea anaonekana *live* kwenye *TV*. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, hata kama *TV* imegeukia kwingine lakini naonekana, hamna neno. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana. Nianze kwa kusema kwanza ninakupongeza wewe kwa dhati sana kwa kuchaguliwa kuwa Spika. Hali kadhalika ninampongeza sana Waziri Mkuu naye kwa kuchaguliwa kuchukua nafasi hiyo. Niwapongeze wenzetu wote waliochaguliwa katika Baraza la Mawaziri na Wakuu wa Mikoa. Wabunge wenzangu pia ninawapongezeni sana. Najua wengi mlikuwa na mchakato, lakini nadhani wachache walikuwa na mchakato mgumu kama uliofanana na wa kwangu, ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nichukue fursa hii kusema kwamba, nilikuwa nimeandaa mazungumzo ya jumla na ambayo yanalenga kwenye Jimbo langu ili wanajimbo wangu waweze kusikia. Lakini kwa sababu ya muda nitazungumza kwa ujumla kidogo halafu zaidi nitakuwa nalenga kwenye Jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, mimi natoka Jimbo la Kilindi. Wabunge wengi ukiwaambia Kilindi wanakuuliza ni wapi, wanafikiria ni Kusini. Hapana, ni Mkoa wa Tanga. Ni moja kati ya majimbo mazuri sana, ni yenye raslimali nyingi sana. Kuna madini mpaka unashindwa mwenyewe na mengine hatujayagundua mpaka leo. Kuna misitu, wanyamapori, ardhi, kila kitu kipo na umaskini uliopindukia vile vile upo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kwanza kabisa niwapongeze sana na niwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Kilindi kwa imani waliyonipa. Kama mnavyoelewa, ndani ya Mkoa wa Tanga mara nyingi majimbo yetu yanakuwa yanaongozwa na wanaume. Lakini mimi nilivunja mwiko na ninawashukuru sana wananchi wa Kilindi kwa kunikubalia kufanya hilo. Aidha, nichukue fursa hii kukishukuru sana Chama changu cha Mapinduzi (CCM) kuanzia Taifa, Mkoa, Wilaya, hadi chini kabisa kwa misaada yote waliyonipa. Hapa sisiti kumtaja msimamizi wangu wa kampeni *(Campaign Manager)* anaitwa Fikirini Wasokola. Nakumbuka tulilala naye porini maana sisi tulikuwa tunalala pale tunapomalizia. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tunalala pale ambapo tunamalizia kampeni kwa siku hiyo. Tukimalizia Umasaini porini, huko huko. Tukimalizia kokote milimani, huko huko. Kwa hiyo, ninamshukuru sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mnyimi wa fadhili nisipomshukuru sana Spika na Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Hawa walinipa ushirikiano mkubwa sana hasa kwa safari ambazo walikuwa wanapokezana kila mara kuja kule kunipa ushirikiano. Kwa kweli ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema itabidi tu nizungumzie zaidi hotuba ya Mheshimiwa Rais, lakini kwa kulinganisha na hali ilivyo kule kwangu na ambavyo nimeifurahia hotuba hiyo. Namshukuru sana na ninampongeza

sana Mheshimiwa Rais Kikwete kwa hotuba yake nzuri ambayo kwa kweli mambo mengi yalilenga katika ufanisi na maendeleo ya Jimbo letu la Kilindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sentensi ya kwanza ambayo ilinifariji na ninanukuu hapa alisema : "Ninyi Waheshimiwa Wabunge ndiyo macho na masikio ya wananchi." Kwa kweli nilifurahi, maana alinipa nguvu.

Mheshimiwa Spika, nilivyokuwa katika Bunge la Afrika Mashariki, kulikuwa na vitu vingi tunafanya, maana tulikuwa ni Wabunge wa Afrika Mashariki. Nilikuwa ninaruhusiwa kufanya chochote kile ili mradi nazingatia kanuni na taratibu na ni kwa ajili ya maendeleo ya watu wa Afrika Mashariki. Lakini sasa nilivyoingia kwenye Jimbo, pale kuna wakati ukifanya kitu watu wanasema anaingilia. Sentensi hii imenipa nguvu na sisi wote tumepewa nguvu ndugu zangu. Waheshimiwa Wabunge, kinachohitajika ni sisi kuhakikisha kwamba sasa tunafanya kazi yetu bila woga wala hofu, vitu ambavyo sina.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la njaa, kuna maeneo msimu uliopita hawakuvuna hata gunia moja! Kwa hiyo, hili suala kwa kweli limefanya hata nisitishe ziara yangu ya kushukuru wananchi kwa sababu ni kubwa sana. Imefika mahali watu hawana kabisa chakula na cha kusikitisha zaidi hata mbegu hawana. Mvua sasa zinaanza kunyesha na hawajui hata msimu ujao watakula nini.

Mheshimiwa Spika, nilipoongozana na wananchi wangu na viongozi kwenda kule kwenye Idara ya Maafa, Ofisi ya Waziri Mkuu, tulipata ushirikiano sana kwa Mkurugenzi wa maafa Mama Beatha Swai. Kwa kweli alinisaidia maana wale wazee waliondoka wameridhika kabisa. Ninashukuru pia hatua ambazo Serikali inaendelea kuchukua na ninawahakikishia wananchi wa Kilindi kama walivyosema viongozi wakuu wa nchi hii. Sasa hivi mtahakikishiwa kwamba matatizo yenu yanakwisha, hususan kwa upande wa chakula.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la maji, nimefurahi sana Mheshimiwa Rais aliposema atalipa msukumo. Nimekaa sana Dar es Salaam, nilikuwa ninaona yale matatizo ya maji na nilikuwa ninalalamika, lakini Kilindi ni habari nyingine kuhusu maji. Watu wanakwenda kutafuta maji siku tatu, siku nne kwenye mashimo ambayo nilipelekwa kuyaangalia, machozi yalinitoka. Nyoka wamo ndani na kadhalika na wanasubiri kwa sababu maji yanatiririka kidogo kidogo, inabidi wasubiri. Kwa kusema kwamba suala hili lipewe msukumo, nilishukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, pia barabara ni tatizo letu kubwa sana kule. Kwa hiyo, nilifurahi nalo lilivyozungumzwa. Nasema kweli nchi nzima inahitaji barabara, lakini ndugu zangu Kilindi tunahitaji kwani tunalima mazao mengi sana, lakini hatuna jinsi ya kuyasafirisha ili kuyafikisha kwenye soko. Kuna mahali nilikwenda kwenye milima ya Lulago huko, hiriki imejaa inaozea kwenye mashamba ambapo tungeweza kuisafirisha hata nje. Kwa hiyo, naomba niseme kwamba hilo nalo ni ni moja ya tatizo.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa sababu ya muda, labda nizingatie yale ya muhimu tu. Mheshimiwa Rais alizungumzia Makao Makuu ya Wilaya kuwa na hadhi. Naomba basi jamani pale Songe, Makao yetu Makuu ya Wilaya, tuwekewe hata lami, hata umeme, hata basi chochote kile cha kuonyesha ni Makao Makuu ya Wilaya. Mahakama pia haipo, kituo cha Polisi ni *police post* tu! Nasema kwamba hapa nitahitaji ushirikiano sana sana. Kilimo, elimu na afya, vyote vina matatizo tunahitaji pembejeo.

Mheshimiwa Spika, lakini makubwa mawili aliyosema ambayo ni muhimu sana ni mikataba. Mikataba siyo ya juu tu. Kule kuna mikataba mingine ambayo ni lazima tuizingatie hususan wa Mafulira, wa machimbo ya madini ambayo walikabidhiwa wachimbaji wadogo wadogo. Bila kushirikishwa, walienda kuingizwa mkataba na Ashanti. Sasa hivi wale wamewekwa kando, Ashanti wanaendelea. Hii mikataba ukiuliza wananchi hawajawahi kuiona. Kwa hiyo, suala la mikataba lilinifurahisha kwa sababu litanisaidia kutatua mambo makubwa sana jimboni Kilindi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine la mwisho ni kwamba, jamani nimetoka Bunge la Afrika Mashariki. Wote mnajua Bunge lile lilivyo na neema. Nimekuja kwa sababu maamuzi yote kama alivyouliza swali Mheshimiwa Mwakyembe asubuhi, yanafanyika kwenye Bunge la Nchi Wanachama kama hapa Dodoma, kule ninyi ni kukusanya na kuunganisha. Nimeona nitoke kule nije huku tushirikiane kwa sababu tayari nimepata uzoefu. Ninajua wenzetu wanafanya nini, nimepata nguvu na elimu. Nitashirikiana nanyi na Bunge lako kuhakikisha mengi ambayo yako kwenye mlolongo, ambayo yako katika Jumuiya ya Afrika Mashariki tunaweza kuyatatua.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa ninaomba niseme kwamba Jimbo la Kilindi na Wilaya ya Kilindi ni ya wakulima na wafugaji. Mheshimiwa Rais ameongelea matatizo ya wakulima kwamba maeneo yatengwe.

Tumefikia hatua mbaya sasa hivi kule Kilindi. Eneo hili mimi nimelifurahia na ninasema ninaomba ushirikiano wenu na wengine ambao wana matatizo kama hayo ya kwangu, tuungane pamoja tuone tunaweza kufanya nini ili kuwasaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru, nadhani nitaendelea kuchangia siku hadi siku, lakini naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kesho asubuhi Spika atakwenda kuhudhuria sherehe ya kuapishwa Wakuu wa Mikoa kule Chamwino. Kwa hiyo, Naibu Spika atakuwa kwenye kiti hapa. *(Makofi)*

Sasa kwa kuwa tumefikia mwisho, naona imebaki dakika moja tu, sina haja ya kumsumbua Mheshimiwa Waziri kutoa Azimio la Kuahirisha Bunge. Kwa hiyo, naliahirisha Bunge hadi kesho asubuhi saa tatu. *(Makofi)*

*(Saa 01.44 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa Tarehe 10 Februari, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*